Maduka holela ya dawa yanavyohatarisha afya

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Na Albano Midelo

UCHUNGUZI umebaini kuwa maduka ya dawa baridi bado yanaendelea kuwepo katika maeneo mbalimbali nchini licha ya kwamba maduka hayo yalifutwa kisheria mwaka 2009.

Imebainika kuwepo maduka hayo na mengine yanayoendeshwa kinyume cha sheria. Matokeo yake, kunakuwa na matumizi ya dawa yasiyo sahihi hali ambayo inasababisha usugu katika ugonjwa alionao mtu.

Hali hiyo imesababisha Mamlaka ya Udhibiti wa Chakula na Dawa(TFDA) chini ya Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma kufungia leseni maduka 48 ya dawa muhimu kutokana na kushindwa kukidhi vigezo vya uendeshaji kisheria.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Songea Dk Mameritha Basike anasema idara ya afya imefanya kazi ya utambuzi wa maduka ya dawa muhimu ili kubaini iwapo maduka hayo yanakidhi vigezo kulingana na mwongozo wa uendeshaji wa maduka ya dawa muhimu nchini.

Alisema kati ya maduka hayo yaliyofungiwa, maduka sita yamegundulika yanaendeshwa bila kibali na maduka 12 hayafanyi kazi kwa zaidi ya mwaka mmoja licha ya kuwa na vibali vya kuendesha ya dawa muhimu.

Kwa mujibu wa Dk Basike, katika operesheni hiyo wamebaini maduka nane hayajahuisha vibali vya dawa muhimu kwa zaidi ya mwaka mmoja na maduka 22 yamefunguliwa katikati ya mji wa Songea kinyume cha muongozo wa maduka ya dawa muhimu.

Hata hivyo anasema imebainika maduka 23 hayajapata kibali cha [illegible] barua

> "Kati ya maduka ya dawa muhimu 222 yaliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea, maduka 146 ndiyo yana vibali vya kuendeshea biashara ya maduka ya dawa muhimu."

Halmashauri ya Manispaa ya Songea ya kuruhusiwa kuendesha biashara ya duka la dawa muhimu.

"Kati ya maduka ya dawa muhimu 222 yaliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea, maduka 146 ndiyo yana vibali vya kuendeshea biashara ya maduka ya dawa muhimu",anasema Dk Basike.

Anasema kuwa katika operesheni ya utambuzi huo, maduka nne yamefungwa kwa sababu wamiliki wake wamefariki, wamiliki 11 wamepewa miezi sita ili maduka yao kupandishwa hadhi kuwa maduka ya dawa moto (famasi) kwa kuwa maduka yalifunguliwa mwaka 2003 kabla ya sheria ya TFDA ya mwaka 2003.

Manispaa ya Songea imefanya utambuzi huo ili kutekeleza agizo la Katibu Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) wa kutambua maduka ya dawa muhimu na rejareja yaliyosajiliwa chini ya Baraza la Famasia yanayoendeshwa kisheria.

Katika agizo hilo, Katibu Mkuu ameagiza kuyaondoa kwa kuyafunga mara moja maduka yote ya dawa muhimu katika maeneo ya miji mikubwa yalioanzishwa kinyume cha sheria.

Uchunguzi umebaini kuwa licha ya kuwepo kwa sheria ya TFDA ya mwaka 2003 na baadaye sheria ya Famasia ya mwaka 2011 ya uanzishaji na usimamizi wa maduka ya dawa muhimu nchini, inayoelekeza maduka hayo kuwepo katika maeneo ya vijijini na miji midogo, bado maduka hayo yameendelea kuanzishwa na kuwepo katika miji mikubwa.

Ina maana yameanzishwa kinyume; bila mamlaka ya tawala za mikoa na serikali za mitaa zilizokasimiwa madaraka kisheria na Baraza la Famasi kuchukua hatua zozote za kisheria.

Uchunguzi umebaini pia kuwa maduka ya dawa baridi yanaendelea kuwepo katika maeneo mbalimbali licha ya kwamba maduka hayo yalifutwa kisheria mwaka 2009.

"Hali hiyo imeendelea kusababisha matumizi ambayo sio sahihi ya dawa na kusababisha usugu wa vimelea vya magonjwa hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa serikali katika uagizaji wa kiwango kikubwa kisichoendana na uhalisia wa Taifa letu",anasema daktari wa binadamu, Dk Ntuli Kapologwe.

Dk Kapologwe anasisitiza kwamba kwa kuwa Tamisemi ndiyo msimamizi mkuu ,lengo lake kuu ni kuhakikisha kuwa huduma za afya zinaboreshwa na kuwafikia wananchi wote kwa usahihi na kwa wakati.

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com simu 0784765917

Kama Mzazi

Na Nicodemus Ikonko

Ajira ya wafanyakazi wa majumbani irasimishwe

KATIKA safu yetu ya Kama Mzazi wiki hii naomba nianze kwa kuwapa pole wazazi vijana kwa maana ya wale wanaojiunga katika kundi hili hivi sasa la kuwa wazazi na walezi wa watoto wetu.

Hakuna ubishi kwamba enzi zetu sisi za mwaka 47 kulikuwa na urahisi wa aina yake wa kuweza kupata watumishi wa ndani wa kuweza kuwalea watoto wakati wazazi wakiendelea na shughuli zao nyingine za kuwaingizia kipato cha kuendesha familia zao.

Wazazi waliokuwa wanahitaji huduma hii ni pamoja na wale walioajiriwa na wasioajiriwa kwa kuwa kuna wakati ambao hulazimika kuondoka nyumbani kwenda kutekeleza majukumu yao mbali na wanapoishi au hapohapo wanapoishi lakini wasingeweza kutekeleza majukumu hayo wenyewe bila kuwa na wasaidizi wa kuyashughulikia masuala ya ndani ya familia zao ikiwa ni pamoja na usafi, uandaaji wa chakula na utuzaji watoto.

Upatikanaji wa watoto wa kazi kama wanavyoitwa siku hizi ni kinyang'anyiro kikubwa kiasi kwamba baadhi ya wazazi vijana hivi sasa wanaona ni kama adhabu ya aina yake kuzaa au kuanzisha familia.

Wakazi katika mitaa, miji na majiji yetu mbalimbali hususan wazazi vijana, hivi sasa wanafikia hatua ya vuta nikuvute kati ya mmoja wao kubaki nyumbani au kuacha kazi kwa ajili ya kukosa msichana wa kazi.

Mmoja wa wazazi vijana ambaye ni mwanamama anayesoma shahada ya pili katika moja ya vyuo vikuu vya jijini Dar es Salaam nyakati za jioni anasema, ni muda wa miezi sita sasa tangu msichana wake wa kazi aondoke na hajapata mwingine wa kuchukua nafasi yake.

Mama huyo ambaye kutokana na miiko ya kazi siwezi kulitaja jina lake ana watoto wawili, mmoja kati yao ni msichana wa miaka 11 huku mdogo wake akiwa na miaka mitano.

"Sina jinsi. Hivi sasa wakirudi shuleni hujipikia wenyewe.

Nikirudi kutoka darasani ni majira ya kati ya saa 4 na saa 5 usiku. Wakati mwingine huwakuta wameshalala," alisimulia na kuongeza kwamba "wanakua kabla ya wakati wao lakini sina jinsi."

Alisimulia kuwa msichana wa kazi aliyeondoka alimfanyia vituko miezi miwili tu baada kuanza kazi, hivyo kulazimika kumwodoa. "Hali ni ngumu," alisema kwa kukata tamaa.

Ukipata wasaa wa kuzungumza na wazazi vijana watakuelezea kila mmoja wao madhila adimu ya watoto wa kazi.

Kuna ombwe na mahitaji makubwa ya huduma hii kwa sasa lakini pia upatikanaji wake hauna uhakika.

Pengine wakati umefika wa kuanzisha kwa makusudi mafunzo ya watoto wa kazi katika utaratibu rasmi na kisha watakaofuzu mafunzo hayo wajiunge katika kampuni ambayo itaweza kuweka matangazo ya ajira za wasichana wa kazi.

Yyombo husika, vichukue hatua mahususi kuwasajili rasmi, na kuwa ajira kama ajira nyingine kwa kufuata taratibu na sheria za kazi.

Scanned by CamScanner

Na Seleman Mayunga

Zaidi ya sh. milioni 188 kunufaisha wanawake na vijana Songea

Zaidi ya shilingi milioni 188 zimetengwa na Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa mwaka wa fedha 2017/18 kwa lengo la kuwakopesha wanawake pamoja na vijana ili waweze kujikwamua kiuchumi na kuondokana na wimbi la umasikini.

Manispaa ya Songea ambayo inakua kwa kasi kiuchumi imejizatiti kuwainua na kuwakwamua wanawake na vijana ili kuendana na kasi ya serikali ya awamu ya tano yenye dhamira ya kujenga Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati.

Kwa kipindi hiki cha robo ya mwaka 2017/18, Manispaa ya Songea imetoa jumla ya shilingi milioni 45 kutoka kwa mapato ya ndani ili kukopesha vikundi 49 na kati ya vikundi hivyo vijana ni 10 na wanawake vikundi 39.

Akisoma taarifa fupi ya utekelezaji wa shughuli za mfuko wa wanawake na Vijana hivi karibuni katika ukumbi wa Manispaa ya Songea, Mkuu wa Idara ya Ustawi na Maendeleo ya Jamiii wa Manispaa ya Songea, Naftari Sayoloi alisema kuwa Manispaa ya Songea ipo mstari wa mbele kuhakikisha kuwa wananchi wa manispaa hiyo wanajikwamua kiuchumi.

Sayoloi alisema kuwa, Manispaa ya Songea mwaka wa fedha 2014/15 ilikopesha zaidi ya shilingi milioni 126 na laki 9 kwa vikundi vya wanawake vipatazo 202 na shilingi milioni 55 na laki moja ilikopeshwa kwa vikundi vya vijana vipatavyo 115 jambo ambalo linamchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi.

"Manispaa ya Songea mwaka 2016/17 ilitoa zaidi ya shilingi milioni 92 kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya mfuko.

Kati ya fedha hizo shilingi milioni 3 na laki 2 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji, wakati shilingi milioni 88 na laki 8 zilikopeshwa kwa vikundi 126 vya wanawake pamoja na vijana", alisema Sayoloi.

Sayoloi aliongeza kuwa, sambamba na shughuli za kutoa mikopo pia Manispaa ya Songea hutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi vyote ili kuwapa mwanga jinsi ya kuiendeleza mikopo yao na kutengeneza faida kubwa.

Sayoloi alifafanua kuwa hali ya marejesho kwa vikundi vya wanawake pamoja na vijana yanaenda vizuri kwani mpaka sasa marejesho ya wanawake ni shilingi 53,525,850/=, ambapo marejesho ya vijana ni 9,847,000/=.

Kwa upande wake Meya wa Manispaa ya Songea, Alhaji Abdul Hassan Mshaweji alisema kuwa vikundi vya wanawake na vijana vinavyopata mkopo lazima ziwe na mpango kazi mzuri utakaoviwezesha kurejesha mkopo kwa wakati na kuisaidia Manispaa kuongeza mapato yake.

Mbunge wa Jimbo la Songea mjini Mhe. Leonidas Gama akikabidhi fedha kwa baadhi ya wanakikundi wanawake wa Manispaa ya Songea (Picha na Albano Midelo).

Mshaweji alisema kuwa changamoto kubwa inayovikumba vikundi vingi ni namna ya kurejesha mikopo yao ambapo kuna baadhi ya vikundi havina mpango kapambe wa maendeleo na mwisho wa siku hushindwa kurejesha mikopo yao.

Kwahiyo, Mshaweji alivitaka vikundi hivyo kuyatumia vyema mafunzo ya ujasiriamali wanayoyapata kwa lengo la kukuza uchumi wao binafsi na kwa maslahi mapana ya nchi.

"Kazi yetu sisi viongozi wenu ni kuhakikisha kuwa tunaisimamia na kuishauri serikali ili iweze kuwapatia mikopo kwa mujibu wa sheria za nchi ambazo zinasisitiza kuwa asilimia 10% ya mapato ya Halmashauri husika iingizwe kwenye mfuko wa wanawake na vijana, hivyo nawasihi mtumie fursa hii kujikwamua kiuchumi na hatimaye kuondokana na umasikini," alisema Mshaweji.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, Leonidus Gama ambaye alihudhuria kufunga mafunzo ya ujasiriamali alisema kuwa wanawake na vijana wanaokopeshwa na Manispaa hawana budi kufanya kazi kwa bidii ili kuinua vipato vyao.

Gama alisisitiza kuwa wanawake na vijana lazima wawe wabunifu hasa katika suala la ujasiriamali na kutumia malighafi na mazingira yaliyopo kuimarisha viwanda vidogovidogo na hatimaye kuondokana na wimbi la umasikini.

"Vikundi vyote naviomba viwe na mipango madhubuti ya kubuni viwanda vidogovidogo ambavyo vitasaidia kuinua uchumi wa nchi pamoja na kutengeneza ajira kwa watu wengine," alisema Gama.

Gama aliongeza kuwa vikundi vya ujasiriamali pale vinapokuwa na wazo la viwanda vidogovidogo lazima viwakilishe mawazo SIDO ambako wataweza kupata ushauri na msaada wa kutengeneza mashine mbalimbali za vitega uchumi.

Baadhi ya vikundi vya wanawake na vijana vya Manispaa ya Songea vinavyonufaika na mikopo ya serikali ni pamoja na Sayuni, Wanawake na Maendeleo Legele, Faraja Group, Kikundi cha Wanawake Tunaweza, Kikundi cha Busara, Tuganili UWT Vikoba, na Faith Group (VJ).

Kwahiyo, Manispaa ya Songea iwe mfano wa kuigwa na Manispaa nyingine kwa kuwa na mpango kabambe wa kuinua uchumi wa nchi kwa kuwawezesha vijana pamoja na wanawake. Rai yangu hapa ni kwamba, watanzania wasiwe watu wa kulalamika kwamba pesa ni ngumu kupatikana bali lazima wafanye kazi kwa bidii ili wafanikiwe kimapato.

Lakini pia, wanawake na vijana ambao hawajajiunga katika vikundi mbalimbali vya ujasiriamali hawana budi kufanya hivyo ili kuirahisishia serikali pamoja na taasisi za fedha kutoa mikopo kwao na hatimaye kujikwamua kiuchumi na kuondokana na wimbi la umasikini.

Pamoja na hilo, viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu wanashauriwa kuwa wazalendo na kusimamia vyema fedha za umma ili kuweza kufanikisha miradi yote ya maendeleo iliyopo katika jamii yetu.

Viongozi wa vikundi vya ujasiriamali pamoja na wanakikundi wanatakiwa kuwa waaminifu kwa mikopo wanayopewa na Manispaa ama taasisi za fedha ili kuwezesha vikundi vingine kuweza kupewa mikopo hiyo.

Pia, taasisi za fedha ambazo zilianzishwa kwa lengo la kukwamua wananchi kiuchumi zinashauriwa kuwa na masharti nafuu na riba ndogo ambayo itasaidia watu wengi zaidi kuweza kupata mikopo na hatimaye kufanya shughuli za uzalishaji pamoja na biashara kwa maendeleo ya nchi.

Kuna baadhi ya taasisi za fedha hapa nchini zimekuwa zikitoa mikopo yenye riba kubwa jambo ambalo linakwamishwa watu wengi kushindwa kupata mikopo na kukwamisha shughuli za maendeleo hapa nchi, hivyo havina budi kubadilika na kusaidia wananchi wa hali ya chini.

0759 388023

Scanned by CamScanner

Majimaji ni Kioo Cha soka Mkoani Ruvuma

Na Albano Midelo

Ukweli ni kwamba, timu ya Majimaji ya Songea Mkoani Ruvuma, imebakia tena kwa Msimu ujao wa ligi kuu Tanzania Bara, baada ya kuifunga Mbeya City 2-1 katika mchezo wake wake wa mwisho hivyo kuepuka mkasi wa kushuka daraja.

Timu ya Majimaji msimu huu kwa mara nyingine ilijikuta katika nafasi za kujinasua kushuka daraja kwa sababu ilikuwa katika nafasi mbaya kwenye msimamo wa ligi kuu. Hata hivyo ikafanikiwa kuruka hadi nafasi ya tisa baada ya kumaliza michezo 30 katika ligi hiyo.

Majimaji ni miongoni mwa timu maarufu za soka hapa nchini ambayo ina historia ndefu ukiachia timu za Simba na Yanga ambazo zimedumu kwa muda wote zikicheza ligi kuu bara na kuwa na wapenzi lukuki toka kila kona ya nchi yetu.

Hakuna ubishi Timu ya Majimaji inafuatia kwa kuwa na washabiki na wapenzi wengi hapa Tanzania. Hadi leo Majimaji imepitia mafanikio mafanikio pamoja na changamoto lukuki.

Licha ya kupata mafanikio makubwa katika mchezo wa soka hapa nchini, Majimaji pia imekumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo kukumbana na mkasi wa kushuka daraja mara kadhaa katika vipindi tofauti.

Historia inaonesha kuwa, Klabu ya Majimaji ilianzishwa mwaka 1977 na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma wa zamani na Katibu Mkuu Mstaafu CCM Dk Rawrence Gama ambapo Kikosi cha kwanza cha Majimaji kiliweza kuundwa kwa

kuichukua timu ya kombaini ya Mkoa wa Ruvuma na kupewa jina la Majimaji.

Kulingana na historia hiyo, Timu ya soka ya Majimaji ilipanda daraja na kucheza daraja la kwanza kwa wakati huo sasa ligi kuu Tanzania Bara mwaka 1982 ambapo walicheza msimu mmoja na kushuka kutokana na wachezaji wake wa wakati huo kutokuwa na uwezo wa kuhimiri mikikimikiki ya ligi hiyo ambayo ilikuwa na timu nane kwa nchi nzima katika kipindi hicho.

Mwaka 1984 Majimaji ilirejea tena kucheza ligi hiyo kwa kasi baada ya kujipanga na kuwa moja ya timu ambayo ilikuwa na sifa ya kuwalipa fedha nyingi na maslahi bora wachezaji wake, hali iliyosababisha baadhi ya wachezaji wa timu za Simba na Yanga kutoka Dar es salaam kutimkia Songea ili kujiunga na wanalizombe.

Wachezaji ambao walikuwa wakiwika kwa wakati huo kwa timu za Simba, Yanga na Pan African ambao walikuja kujiunga na timu hiyo yenye makao makuu yake mjini Songea baadhi yao ni Peter Tino, Zamoyoni Mogela, Malota na Inocenti Haule.

Baadaye mchezaji Innocent Haule aliamua kuachana na Majimaji na kutimkia nchini Kenya kucheza ligi za huko baada ya uongozi wa Simba kudai wachezaji hao walikuwa wamehama bila kufuata utaratibu wa uhamisho kutoka katika vilabu vyao.

Katika kipindi hicho Timu ya Majimaji ilikuwa tishio kwa vilabu vingine vilivyokuwa vikishiriki ligi hiyo na hata kusababisha kuchukua ubingwa wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa miaka miwili mfululizo mwaka 1985 na 1986 ambapo ligi hiyo ilikuwa ikishirikisha timu sita kati ya hizo timu tatu kutoka Visiwani na tatu kutoka Bara.

Majimaji katika mchezo wake wa kwanza wa mashindano ya klabu bingwa barani Afrika mwaka 1986 ilipangiwa na timu ya Dyanamo ya Zimbabwe, mchezo ambao ulifanyika mjini Harare makao makuu ya nchi ya Zimbabwe, katika mchezo huo Majimaji ilifungwa mabao 5-0.

katika mechi ya marudiano mchezo haukuweza kufanyika kwa sababu Timu ya Majimaji ilijitoa baada ya kupata ajali (kwenye kona za Maji Maji kabla ya kufika Njombe) wakati ikitokea Songea kuelekea Dar es Salaam na baadhi ya wachezaji wake waliumia vibaya akiwemo Athumani Maulid na ikawa mwisho wake wa kucheza mpira.

Historia inaonesha kuwa, Mwaka wa pili Timu ya Majimaji ilipochukua ubingwa wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ilipangiwa mchezo wake wa kwanza kucheza na timu ya Shirika la Kilimo la nchi ya Madagasca (BTM) na kushinda bao 2-1. Katika mchezo wake wa marudiano uliochezwa katika uwanja wa Taifa (Uhuru) Jijini Dar es Salaam, Timu ya Majimaji ilishinda tena mabao 2-1 hivyo kusonga mbele, na kutolewa na FC Leopard ya Kenya kwa jumla ya mabao 2-0. Timu ya Majimaji ilianza kuyumba baada ya Dk. Gama kuhama Mkoa wa Ruvuma na kuhamia Mkoa wa Tabora, baada ya viongozi wa Serikali ya Mkoa kushindwa kuchangia masuala ya michezo.

Dk.Gama alipenda michezo na alikuwa mstari wa mbele kushughulikia changamoto zilizokuwa zinawakabili wachezaji. Hata hivyo Dk. Gama akiwa Tabora aliweza kuusaidia Mkoa wa Tabora kuunda timu ya Mirambo iliyokuwa tishio katika ligi kuu Tanzania Bara.

baada ya Gama kuhamishwa miaka ya 1990 timu ilianza kuteteleka ilikuwa chini ya mkuu wa mkoa mwinginel Mh. Nicodemus Banduka ambaye licha ya kufuata misingi ya Gama kuna kipindi lilitoka Tamko kuhusu timu hiyo kujiendisha yenyewe ombi ambalo lididimiza timu ingawa aliisaidia kupata kibari cha Biashara ili kuuza bidhaa mbali mbali kama mbolea, bia sukari n.k.

Mwaka 1995 Banduka alihamishwa, akaja Mama Anna Makina. Makinda aliikuta maji maji ikiwa ICU (chuma cha wagonjwa mahututi), ambapo viongozi wa timu wakamfuata na kumueleza kuhusu Azimio la Mlale lililoanzishwa na Gama; makinda aliguswa na kulifanyia kazi toka chini ya sakafu ya moyo wake.

Inaendelea Uk. 16

PERAMIHO PUBLICATIONS MBALI NA UCHAPISHAJI WA MAGAZETI, INAJISHUGHULISHA PIA NA UANDAAJI NA UCHAPISHAJI WA MISWADA MBALIMBALI YA VITABU, KALENDA NA MACHAPISHO MENGINE KWA GHARAMA NAFUU KABISA. KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA SIMU NAMBA: 0767 57 32 87 au 0746 753 688

Scanned by CamScanner

Manispaa ya Songea kuinua taaluma shule za msingi

Na Albano Midelo

Sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 inaeleza kumwezesha Mtanzania aliyeelimika, mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa.

Dhima ya sera hiyo ni kuinua ubora wa elimu na mafunzo na kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa letu.

Katika kuhakikisha sera hiyo inatekelezwa kwa vitendo, Manispaa ya Songea iliyopo katika Mkoa wa Ruvuma imedhamiria kuhakikisha inatoa elimu inayokidhi malengo ya Taifa.

Afisa Elimu Msingi wa Manispaa hiyo Edith Kagomba amesema Idara ya Elimu Msingi ina jumla ya shule za Msingi 81 Kati ya shule hizo, shule 76 ni za Serikali na shule tano ni zile zisizo za Serikali.

Kwa mujibu wa sera ya Elimu na mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2014, Elimu ya Msingi inajumuisha elimu ya Awali, darasa la kwanza hadi darasa la saba. Hivyo basi kila shule inatakiwa iwe na darasa la Awali ili kuwa na mfululizo mzuri wa usomaji.

"lengo kuu la madarasa ya Awali ni kuwaandaa watoto ili waweze kujifunza vema wanapoingia darasa la kwanza kuwa na umri wa miaka sita hadi saba, katika Manispaa yetu, shule za Msingi zote 81 zina madarasa ya Awali", alisisitiza Kagomba. Idara ya Elimu Msingi ina Jumla ya vitengo vitano ambavyo ni Taaluma, vifaa na Takwimu, Elimu ya watu Wazima, michezo na utamaduni ambapo Vitengo vyote hufanya

kazi kwa ushirikiano na kutoa taarifa katika maeneo mbalimbali.

Katika kutekeleza agizo la Rais la kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayekaa chini ifikapo Juni 2016, Halmashauri ya Manispaa imefanikiwa kufikia lengo hilo kwa kuwa na madawati 16,338 kati ya madawati 15,711 yaliyohitajika na kwamba hadi sasa hakuna mwanafunzi anayekaa chini.

Katika kipindi cha kuanzia Januari 2016 hadi Desemba 2016, Halmashauri ya Manispaa Songea ilipokea zaidi ya sh.milioni 246 ambazo ni fedha za Elimu bila Malipo.

Aidha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi una vipaumbele na mikakati yake kama vile ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi, kuinua kiwango cha ubora wa Elimu na kujenga uwezo wa ufundishaji kwa walimu.

"Manispaa ya Songea imekuwa ikiongoza kitaaluma shule za msingi katika Mkoa wa Ruvuma kwa miaka yote isipokuwa mwaka 2015. Baada ya kuona mapungufu yetu, na kuyarekebisha, wanafunzi wamefaulu vizuri mtihani wa mwaka 2016'', anasema Kagomba.

mambo yaliosaida kupandisha ufaulu mwaka 2016 ni kufanyika kwa tathmini kuanzia katika ngazi ya shule, Kata hadi Wilaya na mfumo bora wa ufundishaji kwa kutumia walimu bora, hali iliwezesha kusaidia kubaini mafanikio na mapungufu ambayo yalifanyiwa kazi na kuyaondoa mapungufu hayo hatimaye kuongeza mafanikio. Vile vile kutekeleza ushauri wa Afisa elimu Mkoa wa Ruvuma wa wanafunzi kujibu maswali 50 kila siku kabla ya kuanza masomo darasani hali iliwafanya wanafunzi kuwa wepesi katika kujibu maswali kwa muda mfupi.

Ili kuhakikisha Manispaa inaendelea kupata ufaulu mzuri, Idara inaendelea kutoa elimu kwa wazazi juu ya umuhimu wa mahudhurio mazuri kwa wanafunzi na kufanya mtihani, kwa sababu kulikuwa na baadhi ya wazazi waliwaelekeza wanafunzi wafanye vibaya siku ya mtihani ili wasifaulu; mfano ni shule ya Msingi ya Lupapila na Londoni.

Baada ya kupata uelewa mzuri, matokeo mazuri yametokea katika shule hizo, hivyo matokeo kwa mwaka jana 2016 Manispaa ya Songea imekuwa ya kwanza katika Halmashauri zote za Mkoa wa Ruvuma.

Hata hivyo licha ya mafanikio ambayo yamepatikana, changamoto za jumla zinazoikabili Idara ya Elimu Msingi katika Manispaa hiyo ni uhaba wa miundo mbinu kama vile uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule nyingi za Manispaa na vyoo.

Kutokuwepo kwa chakula cha mchana shuleni na baadhi ya Jamii kutozingatia masuala yanayohusiana na elimu kwa ujumla, utoro wa kudumu na wa rejareja ambao huathiri ujifunzaji na matokeo ya mitihani na ushirikiano mdogo wa wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni.

Changamoto nyingine ni walimu wengi kutolipwa madeni yao kama vile upandishwaji wa madaraja, kutolipwa 'Areas' baada ya kupandishwa madaraja na pia kutorekebishiwa mshahara baada ya kupandishwa madaraja na upungufu wa walimu katika baadhi ya shule.

"Tatizo la kudumu wanafunzi darasani ni asilimia 55 ukilinganisha na Wilaya nyingine, hii inaonesha mdondoko wa wanafunzi kutoka darasa moja kwenda jingine ni mkubwa, mahitaji ya walimu katika shule yanatakiwa kuwa kwa Mwalimu mmoja iwe kwa wanafunzi 35 hadi 50",anasisitiza.

Inahitaja mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo kama vile kushirikisha wazazi katika kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni na kuwezesha upatikanaji wa chakula cha mchana shuleni, ufundishaji wa masomo ya ziada hasa kwa madarasa ya mitihani, kushirikisha wazazi, jamii, Serikali ya Mtaa na Kata katika kudhibiti utoro na kusimamia walimu kufundisha kwa bidii ili kukamilisha mada.

Mikakati mingine ni kuinua kiwango cha ufaulu kwa kufuta alama D na E, kuhimiza wazazi na wananchi kupitia Serikali za Mitaa na Kata katika kupunguza uhaba wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo na Kufanyika mikutano ya kuwaelimisha wananchi maana na umuhimu wa sera ya Elimu Bure.

Hata hivyo Mamlaka za Ajira kuangalia upya vigezo vinavyotumika kugawa walimu, badala ya kutumika kanuni ya wanafunzi 45 kwa mwalimu mmoja, sasa Wizara iangalie kigezo cha vipindi kwa kuwa hali hiyo husababisha vipindi vingine kutofundishwa kikamilifu.

Alishauri Wizara ya Elimu, Sayansi,Teknolojia na TAMISEMI kuweka uwazi juu ya taarifa mbalimbali za madai ya walimu, kama ya likizo, matibabu, madaraja na Areas zao yalipwe kwa wakati ili walimu waweze kuboresha taaluma mahali pa kazi badala ya kuwaza namna ya kudai madai yao.

Scanned by CamScanner

Polisi na madereva wakiwajibika, ajali zinaweza kupungua

Na Mwandishi wetu

Ajali za barabarani ni moja ya vyanzo vikubwa vinavyosababisha vifo na kuongeza idadi ya watu wenye ulemavu hapa nchini.

Takwimu za ajali zilizotolewa na jeshi la polisi kikosi cha usalama barabarani kwa takribani miaka mitatu kuanzia mwaka 2013 hadi kufikia Desemba 2015 inaonesha kuwa watu 3444 walipoteza maisha, wakiwemo majeruhi 20,181.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, Kundi la watembea kwa miguu linafuatia kwa kusababishiwa vifo vya watu 3328, majeruhi 8256 kutokana na ajali za barabarani katika kipindi hicho.

Licha ya hatua ambazo zimekuwa zinachukuliwa na jeshi la polisi zinapotokea ajali, bado ukubwa wa tatizo umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka na kuleta hofu kubwa kwa wananchi wanaposafiri. hawana uhakika wa kufika salama mwisho wa safari.

Katika mkoa wa Ruvuma mwezi Juni mwaka huu Kampuni ya mabasi ya SUPERFEO katika kipindi cha saa 48 basi zake mbili zinazofanya safari toka mjini Songea hadi Jijini Mbeya zimepata ajali ya kusababisha vifo, majeruhi na kuharibu mali za watu.

Ajali ya kwanza basi la SUPERFEO likitokea jijini Mbeya kuja Songea lilipata ajali katika Kijiji cha Mbangamawe wilayani Songea takrbani kilomita zaidi ya 60 toka ajali hiyo ilitokea baada ya basi hilo kugongana na gari la mizigo lililokuwa limebeba makaa ya mawe na kusababisha kifo cha



dereva wa basi na majeruhi kadhaa.

Katika ajali ya pili ambayo ilitokea baada ya siku moja basi la SUPERFEO tena likitokea jijini Mbeya lilipata ajali katika kijiji cha Hangangadinda baada ya dereva kushindwa kukata kona akiwa katika mwendokasi huku akizungumza na simu. Ajali hiyo ilisababisha vifo na majeruhi 21.

Uchunguzi uliofanywa umebaini kuwa ajali zote mbili zimesababishwa na uzembe wa madereva kutofuata sheria za usalama barabarani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Songea ambaye ndiye Mkuu wa Wilaya ya Songea Pololet Mgema akizungumza mara baada ya kutembelea eneo la ajali na kuwa tembelea majeruhi ambao walikuwa wamelazwa katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma anasema madereva wengi hawasikii na wanandelea kuvunja sheria za barabarani kwa makusudi.

"Lakini madereva wamekuwa hawasikii, sasa jambo la kwanza naagiza vyombo vya dola katika wilaya ya Songea waanze kupima kilevi kwa madereva kila siku kabla hawajaanza safari, tutawasiliana na wenzetu katika wilaya nyingine, wafanye hivyo hivyo kwa kuwa wanaweza kufanywa wakiwa barabarani", anasisitiza Mgema.

Hata hivyo Mkuu huyu wa wilaya anasema sheria zilizopo zinaonekana kama zinatoa adhabu ndogo sana kwa madereva hali inayosababisha kuendeleza vitendo hivyo, kutokana na hali hiyo anapendekeza adhabu ya kuwanyang'anya leseni ya udereva kwa wale wote ambao watabainika wamesababisha ajali kwa uzembe.

"Ukimnyang'anya leseni ya udereva maana yake umemfuta kazi ya udereva hivyo akae benchi au atafute kazi nyingine badala ya kuendelea kuua kwa makusudi watu wasiokuwa na hatia, wengine kupata ulemavu wa kudumu na kuharibu mali za watu",anasisitiza Mkuu wa Wilaya.

Moja ya sababu ambazo zinachangia kuongezeka kwa ajali nyingi nchini ukiacha uzembe wa baadhi ya madereva, lakini pia baadhi ya watu waliopewa dhamana ya kusimamia usalama barabarani wameshindwa kuwajibika kwa kusimamia sheria zilizopo hali ambayo inachangia kuongezeka kwa ajali nchini.

Naomba nitoe mfano wa hali ya usalama barabarani kutoka nchi jirani ya Uganda ambapo, askari wa barabarani katika nchi hiyo wamejitahidi kusimamia sheria za usalama barabarani hali ambayo imesababisha hata madereva katika nchi hiyo kutii sheria bila shuruti.

Nimewahi kuishi katika jiji la Kampala nchini Uganda. Katika nchi hiyo abiria wote kwenye daladala wanakaa katika viti na kamwe huwezi kuona daladala ambayo imesimamisha abiria, hali hiyo imewezekana kutokana na askari wa barabarani kutekeleza sheria za usalama kwa vitendo.

Hapa nchini hali ni tofauti kabisa. Licha ya sheria kuwaagiza wenye mabasi ya abiria zikiwemo daladala kuhakikisha kuwa abiria wanaotakiwa kubebwa ni wale wanaokaa kwenye viti, ni jambo la kawaida kabisa katika mabasi na daladala kusimamisha abiria ambapo wakati mwingine idadi ya abiria waliosimama inazidi abiria waliokaa jambo ambalo ni hatari pale inapotokea ajali.

Askari wetu wa barabarani wanaona hali hiyo, wala hawashituki wanaruhusu mabasi yaliozidisha abiria kuendelea na safari hali ambayo inaweza kuleta madhara makubwa pale inapotea ajali.

Inaaminika moja ya sababu inayosababisha sheria kuvunjwa ni baadhi ya madereva na kondakta kudaiwa kutoa kitu kidogo kwa askari wa barabarani hivyo kuachwa kuendelea kuvunja sheria za usalama barabarani.

Tumeshuhudia katika ajali za mabasi ya abiria zinapotokea vifo na majeruhi idadi ya abiria waliokuwepo katika basi inazidi idadi halisi ambayo ilitakiwa kubebwa na basi hilo.

Haya yote yanadhihirisha wazi hali halisi ya baadhi ya Askari wa barabarani ambao wamepewa dhamana ya kusimamia usalama barabarani kushindwa kusimamia sheria kwa vitendo.

Jambo la kujiuliza hapa ni kwanini nchi jirani ya Uganda wameweza

UNA KIPAJI CHA KUANDIKA?
Tunapokea Kazi mbalimbali zenye kuelimisha na kuadilisha Jamii kutoka kwa Waandishi wa Makala, Mashairi, Hadithi na Hata Barua za Maoni.
Fika Ofisini kwetu, Peramiho Publications mkabala na Peramiho Bookshop.
Au wasiliana na Mhariri kwa simu namba 0767 57 32 87 au kwa barua pepe peramihopublications@gmail.com

(NYOTE MNAKARIBISHWA)

Scanned by CamScanner

Mbamba: Hifadhi nyingine ya asili iliyo mjini

Na Albano Midelo

MKOA wa Ruvuma unatarajia kupata hifadhi ya pili ya asili ya Mbamba (Mbamba Hill) ambayo ipo mjini Mbambabay, yalipo makao makuu ya wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.

Hifadhi ya asili ya Luhira iliyopo kilometa saba kutoka mjini Songea iliyoanzishwa mwaka 1974 ni hifadhi ya kwanza ya asili iliyopo Tanzania na hivyo Mbamba itakuwa ya pili.

Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe anasema Hifadhi ya Mbamba inajumuisha visiwa vya Lundo na Mbambabay (Zambia), milima ya Mbamba na Ndengere ikiwa na jumla ya eneo la hekta 597.

Kati ya hekta hizo, kilima cha Mbamba kina eneo lenye ukubwa wa hekta 40, kilima cha Tumbi hekta 110, kisiwa cha Mbambabay kina hekta 27 na kisiwa cha Lundo ni chenye hekta 20.

Anasema milima na visiwa hivyo vimejaaliwa kuwa na uoto unaovutia wa misitu ya miombo ambao ni maarufu duniani ambapo mawe yanayozunguka visiwa na milima kandokando mwa Ziwa Nyasa ni makazi na mazalia ya samaki wa mapambo aina zaidi ya 400.

Kwa mujibu wa Challe, hifadhi ya Mbambabay inaweza kuleta ushindani wa kibiashara hapa nchini kwa kuwa nchi yetu haina eneo linaloweza kutoa mchanganyiko mzuri wa huduma za kitalii kama ambazo zitatolewa katika hifadhi hii.

Taarifa kutoka Malawi, zinaonesha kwamba nchi hiyo ina hifadhi kadhaa za Taifa katika Ziwa Nyasa. Hifadhi hizo ni pamoja na Lake Malawi National Park na Cape Mcclear Nature Reserve zinazotoa huduma za utalii kwa kutumia rasilimali za Ziwa Nyasa.

Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma anasema kutokana na Malawi kupata mafanikio ya utalii kupitia Ziwa Nyasa upande wa Malawi, mkoa wa Ruvuma unatakiwa kuongeza ubunifu ili kuweza kutoa huduma ambazo ni tofauti na zile zinazotolewa katika nchi ya Malawi.

Hivyo anapendekeza Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania ifanye juhudi za kuzitambua huduma zinazotolewa katika hifadhi za Malawi zilizopo ndani ya ziwa na pembezoni mwa ziwa Nyasa ili kuboresha zaidi za kwetu.

Challe anabainisha zaidi kwamba katika ziwa Nyasa hivi sasa kuna huduma za kitalii kama uvuvi wa kitalii (sport fishing), kupiga mbizi (diving), kuogelea (swimming), kuendesha mitumbwi (canoeing), beach camping na yatching.

Hata hivyo, anasema eneo ambalo linapendekezwa kuwa hifadhi kwenye Ziwa Nyasa iwapo litahifadhiwa litatumika kama mazalia ya samaki, hivyo kuongeza kipato cha wananchi wanaotegemea shughuli za uvuvi.

Kwa mujibu wa Ofisa Maliasili huyo, maeneo yote yaliyopendekezwa kuongezwa katika mradi huo, hayatumiwi katika shughuli za kibinadamu, isipokuwa katika maeneo machache ambayo yanatumiwa na wavuvi kwa kiasi kidogo, hivyo kutoathiri uhifadhi huo.

Kutokana na udogo wa visiwa vya Mbambabay na Lundo, inapendekezwa katika maeneo hayo kusijengwe makazi ya kudumu na kwamba wafanyakazi wa kuhudumia watalii ni vema wawe na makazi nje ya kisiwa ili kuendelea kutunza uoto wa asili uliopo hivi sasa.

Ndege aina ya Fundimchundo

"Hii ni hifadhi ya pekee ya wanyamapori pamoja na samaki wa mapambo, itakuwa hifadhi ya Ziwa Nyasa ambayo itavutia watalii kufika kusini hivyo kutekeleza Sera ya nchi ya kufungua biashara ya utalii Kusini," anasisitiza Challe.

Anasisitiza kuwa hifadhi hiyo itasaidia kulinda mipaka ya Tanzania iliyopo kusini katika Ziwa Nyasa na kuitambulisha dunia kuwa Tanzania inamiliki sehemu ya ziwa Nyasa tofauti na nchi jirani ya Malawi inavyodai.

Mtaalamu huyo wa Maliasili na Utalii wa mkoa wa Ruvuma anashauri milima ya Mbamba, Tumbi na visiwa vya Lundo na Mbambabay vikabidhiwe mapema kwa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) ambao hivi sasa ndiyo waliokabidhiwa dhamana ya kutunza hifadhi za wanyamapori kwa niaba ya serikali na wananchi kwa ujumla.

Anasema Idara ya Maliasili na Utalii mkoani Ruvuma wamekusudia kutekeleza azma ya serikali kwa vitendo kwa kuharakisha mchakato wa kukuza biashara ya utalii na kuifanya Mbambabay ambayo ndiyo makao makuu ya wilaya ya Nyasa kuwa kitovu cha utalii katika mkoa wa Ruvuma.

Mwambao mwa Ziwa Nyasa katika hifadhi ya Mbamba pia kuna kivutio kingine ambacho ni ndege anayejenga nyumba na kupangisha kwa viumbe wengine wakiwemo ndege na mijusi.

Kama ulidhani ni binadamu pekee anajenga nyumba na kupangisha utakuwa unajidanganya kwa kuwa mwambao mwa Ziwa Nyasa, kuna aina ya ndege anayeitwa Fundichuma (Hamerkop) ambaye anajenga kwa ndege na kupangisha kwa ndege na viumbe wengine kama mijusi.

Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe ambaye pia ni mzaliwa wa mwambao mwa Ziwa Nyasa anasema ndege huyo anapenda kuishi jirani na ziwa au mto kwa sababu chakula chake kikuu ni samaki.

Challe anabainisha kuwa fundichuma ni ndege wenye uwezo wa kujenga nyumba kubwa yenye vyumba vingi juu ya mti na kwamba ndege hao jike na dume huwa hawaachani hadi mmoja anapokufa.

Kwa mujibu wa Challe, ndege hao wanajenga nyumba kubwa na kukaribisha ndege wengine na viumbe wengine ambao hupenda kuishi katika nyumba hizo kutokana na ulinzi wa ndege hao.

Hata hivyo, Challe anasema kwa utamaduni wa makabila ya watu wa mwambao mwa Ziwa Nyasa ndege huyo wanamheshimu sana kutokana na ustaarabu wake hivyo wanalinda makazi yake ili yasiharibiwe na kwamba Wanyasa wanaamini ukimuua ndege huyo utapata laana au mikosi.



Hifadhi ya Mlima Mbamba iliyopo mjini Mbambabay wilayani Nyasa.

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili, mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917

Scanned by CamScanner

Fukwe za kuvutia na visiwa mwambao mwa Ziwa Nyasa.

Nyasa ni ghala la vivutio lukuki vya utalii

Na Albano Midelo

WILAYA ya Nyasa bado ina fursa za maliasili lukuki zikiwemo misitu, wanyamapori, samaki, mito, ziwa, fukwe na mali kale ambazo hazijaharibiwa na ndiyo maana tunasema wilaya ya Nyasa ni ghala au benki ya vivutio vya utalii na uwekezaji.

Fursa hizo zinaweza kutoa mchango mkubwa kwenye pato la Taifa na wananchi wa wilaya ya Nyasa, mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla kupitia utalii wa kiutamaduni na ikolojia.

Makao makuu ya Wilaya ya Nyasa yapo katika Mji wa Mbambabay. Ofisa Maliasili na Utalii wa wilaya ya Nyasa, Bugingo, anasema wilaya utalii katika wilaya ya Nyasa ni uwepo wa Ziwa Nyasa ambalo linapatikana Kusini – Magharibi mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ziwa Nyasa ni la tisa kwa ukubwa duniani na ni la tatu kwa ukubwa barani Afrika.

Ziwa hilo lina kina cha kati ya mita 426 na 758 na hii ni kutokana na kupitiwa na bonde la ufa. Kwa upande wa Tanzania mito mingi inapatikana ikitokea wilaya ya Nyasa katika safu za milima ya Livingstone, mito hiyo ni Ruhuhu, Lumeme, Ruhekei, Lwika, Mbamba Bay, Likumbo na Chiwindi ambayo huingiza maji ndani ya Ziwa Nyasa.

Kwa mujibu wa Ofisa Maliasili na Utalii wa wilayani Nyasa, Ziwa Nyasa ni kuvutio kikubwa cha Utalii Kanda ya Kusini kwa kuwa limesheheni vitu vingi ndani yake [illegible] tofauti ukilinganimarefu ambayo yanajulikana kwa wenyeji kwa majina ya hia na mala yanayobeba sifa tofauti," anasema Bugingo.

Tabia nyingine za ziwa hilo kwa muda anazitaja kuwa ni mawimbi makubwa, fukwe nzuri na zenye sifa tofauti, mawe kuonekana kama sakafu eneo la Chiwindi, fukwe zenye udongo wa mfinyanzi, kina cha maji kuwa kifupi kwa umbali mrefu na mchanga mdogo ambao watu wa kale walitumia kusugulia meno ili yawe meupe hasa katika fukwe za Mtipwili.

Bugingo anayataja maeneo mengine ambayo ni kivutio katika wilaya hiyo kuwa ni yale ambayo huota nyasi ambazo zinaonekana kama zimefyekwa kwa ustadi, na fukwe za eneo la Mhalo ambazo zina mapango ambayo kuta zake ni kama zimesakafiwa.

Anasema ripoti ya utafiti wa mwaka 2011, inaonesha kwamba asilimia 15 ya aina za samaki wa maji baridi duniani wanapatikana Ziwa Nyasa ambapo kuna aina ya samaki tofauti zaidi ya 600, huku kukiwa na aina ya samaki wa mapambo zaidi ya 400 na viumbe wengineo ambao hawapatikani katika ziwa lolote duniani isipokuwa katika maeneo tofauti ndani ya ziwa Nyasa kutegemeana na aina na usalama wa maisha yao.

Jonathan Ruanda, mtaalamu wa kuzamia samaki wa mapambo katika Ziwa Nyasa na mfanyabiashara wa samaki hao anasema tangu mwaka 1960 samaki hai wa mapambo walianza kuuzwa katika nchi za Ulaya na Marekani.

Hata hivyo, anasema nchi nyingi kama vile Japan, Sweden, Uturuki, Denmark, Canada, Ufaransa, Uingereza na Ujerumani zilivutiwa na samaki wa mapambo kutoka Ziwa Nyasa kutokana na kuwa na sifa ya kipekee, yaani rangi nzuri za kupendeza na hakuna sehemu nyingine wanapatikana samaki wa mapambo wa aina hii.

Ofisa Maliasili wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe anabainisha kuwa Ziwa Nyasa pia limesheheni utajiri mkubwa wa viumbe hai wakiwemo fisimaji, mamba, nyoka na viboko ambao ni kivutio kikubwa cha utalii.

"Ndege wanaohamia kutoka Ulaya na baadhi ya nchi za Afrika wanapatikana maeneo ya mwambao mwa Ziwa Nyasa ambao ni kivutio kikubwa cha utalii. Ndege hao huja kwa ajili ya kujipatia chakula cha aina mbalimbali katika mwambao wa ziwa Nyasa wakiwa kwenye misafara yao," anasisitiza Challe.

Akizungumzia jina la Mbambabay, mji ambao ni makao makuu ya wilaya ya Nyasa, Challe anabainisha kuwa Mbamba ina maana ya radi na bay ikimaanisha ghuba na kwamba vyote hivyo ni vivutio vyenye historia ya kupendeza na kuvutia kwa wageni.

"Tafsiri hizi ambazo zilitolewa na wenyeji zinaonesha kwamba zamani, kulikuwa na radi kali za mara kwa mara zikipiga kwenye rasi iliyopo karibu na ghuba hiyo na ndipo eneo hilo likaitwa Mbamba bay," anasema Challe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Dk Oscar Mbyuzi anabainisha kuwa rasi hiyo ni kubwa na imefunikwa na uoto wa asili wa miti na nyasi, baadhi ya miti hiyo inatumika kama dawa za asili hadi sasa.

Dk Mbyuzi anabainisha zaidi kuwa watu pia hutumia msitu wa Mbamba kwa matambiko yanayoambatana na kupiga ngoma za kufukuza au kuita majini kwa imani zao na kwamba katika msitu huo kuna wanyama kama chui wanatokea milima ya Nangombo, Ukuli na Chinyemba ambao wanapatikana katika rasi hiyo, wakiwafuata wanyama aina ya ngedere waliopo kwa wingi katika msitu huo.

Kulingana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nyasa, maeneo mengine ya vivutio vya utalii kwa wilaya hiyo ni visiwa vya Mbamba, Lundo, Hongi na jiwe la Pomonda, ambavyo vyote vimekuwa na sifa na historia nyingi ambazo zikitangazwa vizuri zitachangia kukuza utalii kwa kuvutia watalii wa ndani na nje.

"Visiwa hivi kila kimoja kimekuwa na sifa ya pekee; kisiwa cha Mbamba kina sifa ya kuwa na mapango ambayo wavuvi hujihifadhi wakati wa dhoruba kali, samaki wa mapambo pia wanapatikana katika kisiwa hicho," anasema.

Anasema kisiwa cha Lundo kina historia ya kuishi wagonjwa wa ukoma waliotengwa na jamii na makaburi ya wagonjwa hao ambao walizikwa kwenye tope au kwa kubandikwa tope kwa imani kwamba wakifanya hivyo wangetokomeza ugonjwa huo.

"Kituo hicho baadaye kilihamishiwa kijiji cha Ngehe kata ya Kihagara wilayani Nyasa ambacho kipo hata sasa," anasema Dk Mbyuzi.

Kwa mujibu wa Dk Mbyuzi, kivutio kingine maarufu ni uwepo wa jiwe la Pomonda ambalo lina pango kubwa ambalo linaweza kuhifadhi watu zaidi ya 100. Jiwe hilo wakati huo lilitumika kujificha wakati wa vita na wavuvi kujihifadhi dhoruba inapozidi.

Anazidi kufafanua kwamba jiwe hili pia ni eneo zuri ambalo hutumiwa na waogeleaji kwa ajili ya kujirusha wakati wa mchezo wa kuogelea.

Kivutio kingine ambacho ni maarufu katika wilaya ya Nyasa ni kisiwa cha Hongi kilichopo Kata ya Liuli ambacho ni kidogo lakini chenye kilele ambacho kab ya uhuru wa Tanganyika, nchi y Malawi wakati huo ikiongozwa na Dk Ngwazi Kamuzu Banda "Wamuyaya" iliweka Rada ambayo ilijulikana kwa jina la "Taa ya Banda".

Itaendelea

Scanned by CamScanner

VETA Songea, ilivyopunguza tatizo la ajira kwa vijana

Na Mwandishi wetu

Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA Songea yalianza kutolewa mwaka 1984 kwa kutumia majengo yaliokuwepo katika viwanja vya Sabasaba vilivyopo Matarawe Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Katika kipindi hicho chuo kilikuwa na uwezo wa kutoa mafunzo kwa wanafunzi 60 tu katika fani tatu ambazo ni ufundi magari, ujenzi na useremala.

Mkuu wa Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA Songea Gideon Ole Lairumbe anasema ujenzi wa majengo ya kudumu ya chuo hicho katika eneo la Msamala Manispaa ya Songea ulianza mwaka 2003 na kukamilika mwaka 2005.

Lairumbe anabainisha kuwa ujenzi huo ulijumuisha karakana tisa za mafunzo, jengo la utawala, maktaba, madarasa, jengo la maliwato, uzio na chumba cha mitambo ya umeme.

Anabainisha kuwa katika ujenzi huo zaidi ya sh.bilioni 1.654 zilitumika kati ya fedha hizo, ujenzi wa majengo zilitumika zaidi ya sh.milioni 975, Mshauri elekezi zaidi ya sh.milioni 86.45 na ununuzi wa mitambo na vifaa vya mafunzo zilitumika zaidi ya sh.milioni 592.

Anasema baada ya ujenzi wa chuo hicho kukamilika, uwezo wa kudahili wanafunzi katika chuo umeongezeka toka wanafunzi 60 hadi 250 kwa mwaka.

Hata hivyo Mkuu huyo wa chuo anabainisha kuwa chuo hicho kina wanachuo 646 kati yao wanachuo wanaosomea hatua ya kwanza (level one) wanaume 253 na wanawake 88, wanaosomea hatua ya pili wanaume ni 176 na wanawake 67 na wanaosomea hatua ya tatu wanaume ni 55 na wanawake saba.

"Chuo kinatoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi, kwa kozi za muda mrefu mafunzo yanayotolewa ni katika fani za ufundi magari, uungaji vyuma, umeme wa magari, umeme wa majumba, useremala, uashi, ufundi bomba, ushonaji na uhazili na kompyta'', anasema Lairumbe.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo hadi sasa wanafunzi ambao wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ni 591 na kwamba chuo hicho bado kinaendelea kupokea wanafunzi wa mwaka wa kwanza na kwamba mafunzo yanatolewa katika awamu mbili tofauti asubuhi na mchana.

Mkuu huyo wa Chuo anayataja mafunzo ya muda mfupi yanayotolewa na VETA Songea kuwa ni fani za udereva wa magari daraja D, udereva wa magari ya abiria na uhazili.

Fani nyingine ni ukarabati wa kompyuta, utumiaji wa kompyuta, umeme wa majumba, umeme wa jua, ulimbwende(cosmetology), utengenezaji wa dawa za usafi, sabuni za maji, upishi na utengenezaji wa

Takwimu zinaonesha kuwa tangu kuanzishwa kwa chuo hicho hadi kufikia mwaka 2016 wahitimu wa mafunzo ya muda mfupi ni 3013 kati yao wasichana 523 na wavulana 2490.

Miongoni mwa walionufaika na VETA Songea ni wahitimu wa kwanza 20 wa fani ya ushonaji ambao walikabidhiwa vifaa vya ushonaji vyenye thamani ya sh.milioni 10 kwa ajili ya kuwajengea uwezo wahitimu wa fani ya ushonaji kabla ya hawajaingia rasmi kwenye soko la ajira.

"Chuo kiliamua kuanza na fani ya ushonaji kuwapa motisha ya vifaa kutokana na uzoefu kuonesha kuwa wanaojiunga na fani hii wengi ni wanafunzi wa kike ambao pi waathirika zaidi wa ukosefu wa ajira nchini", anasema Mkuu wa Chuo.

Anasema kuwa chuo hicho kimefanikiwa kupata jengo jipya ambalo linajumuisha maabara za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano(TEHAMA), madarasa na ofisi za walimu.

Sanjari na ufundishaji wa kozi fupi, Mkuu huyo wa chuo anasema chuo kinafundisha kozi fupi za udereva wa pikipiki, udereva wa magari, utengenezaji wa sabuni na

kuwafikia wahitaji wote mahali walipo ili kupunguza changamoto ya ajira.

Licha ya kutoa kozi hizo katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, Mkuu wa Chuo hicho anasema, VETA Songea pia imefanikiwa kufundisha kozi hizo katika wilaya za Njombe, Ludewa na Makete mkoani Njombe.

"Chuo pia kinatoa mafunzo kwa kushirikiana na viwanda na maeneo mbalimbali ya kazi, lengo likiwa ni kuwajengea uwezo zaidi wafanyakazi viwandani ili kuongeza tija", anasema Lairumbe.

Anasema VETA Songea inashirikiana na viwanda na kampuni mbalimbali zikiwemo UNILEVER ambayo ni kampuni ya kiwanda cha chai, Kampuni ya MANTRA ya mgodi wa uranium na kampuni ya Food Security ambayo wafanyakazi wake 31 wamepata mafunzo ya muda mfupi kupitia VETA.

Anayataja matarajio ya chuo hicho kuwa ni kuanzisha fani ya uandaaji wa vyakula (Food Production), utengenezaji wa vifaa vya kilimo(Agro Mechanics) na kozi ya

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano(TEHAMA).

Anatoa rai kwa serikali na wadau wengine kuiangalia VETA kama mkombozi wa ajira kwa vijana hasa katika kipindi hiki ambacho Tanzania na Dunia nzima inakabiliwa na janga la ukosefu wa ajira ambapo vijana ndiyo waathirika wakuu.

Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda wakati anafungua chuo cha VETA Songea mwaka 2013, pamoja na mambo mengine aliagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kusaidia kuongeza nafasi za mafunzo katika vyuo vya VETA ili vijana wengi wanaomaliza shule za msingi na sekondari waweze kupata nafasi ya kujifunza kozi mbalimbali ambazo zitawawezesha kuajiriwa na kujiajiri.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhandisi Stella Manyanya anasema kwa kutambua umuhimu wa elimu ya mafunzo ya ufundi stadi, serikali inaendelea kujenga vyuo vipya vya VETA katika mikoa na wilaya mbalimbali nchini.

Mhandisi Manyanya anasisitiza kuwa serikali itaendelea kusimamia mafunzo ya ufundi stadi nchini kama yalivyoelekezwa katika sera ili kusaidia kukuza uchumi kupitia mafunzo ya VETA huku uhamasishaji zaidi ukiwekwa katika ubunifu na ujasiriamali.

UNA KIPAJI CHA KUANDIKA?
Tunapokea Kazi mbalimbali zenye kuelimisha na kuadilisha Jamii kutoka kwa Waandishi wa Makala, Mashairi, Hadithi na Hata Barua za Maoni.
Fika Ofisini kwetu, Peramiho Publications mkabala na Peramiho Bookshop.
Au wasiliana na Mhariri kwa simu namba 0767 57 32 87 au kwa barua pepe peramihopublications@gmail.com

(NYOTE MNAKARIBISHWA)

Scanned by CamScanner

Ni vigumu kutenganisha Maendeleo na uharibifu wa mazingira

Na Albano Midelo

Kila mwaka kuanzia Juni mosi hadi Juni tano inakuwa ni kilele cha maadhimisho ya siku ya mazingira duniani ambapo utazamwa changamoto mbalimbali za mazingira na kutoa elimu ya namna ya kukabiliana na hali hiyo.

Sayari ya Dunia hivi sasa inakabiliwa na matatizo makubwa ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira ya majini, ardhini na hewani hali ambayo inasababisha changamoto nyingi zikiwemo za mabadiliko ya tabia nchi.

Shughuli za kibindamu zinachangia kuleta uharibifu wa mazingira, kadri binadamu anavyopiga maendeleo yake mbele kiuchumi ndivyo anavyosonga mbele hatua moja katika uharibifu wa mazingira.

Kwa hiyo sio jambo rahisi kumtofautisha binadamu katika masuala ya maendeleo na mazingira. Kwa mfano anapotengeneza barabara ni maendeleo, lakini wakati huo huo anaharibu mazingira kwa kupasua miamba ili apate kokoto, anakata miti na uharibifu mwingine ambao unaleta athari katika mazingira.

Vitu ambavyo vinachangia kuharibu mazingira ni shughuli mbalimbali zinazofanywa na binadamu ikiwemo kilimo, viwanda, uvuvi haramu, uchimbaji wa madini, utengenezaji barabara, ukataji miti ovyo na kazi nyingine za uzalishaji mali.

Wataalam wa mazingira wanasema kuwa sio rahisi kuzuia uharibifu wa mazingira isipokuwa kinachotakiwa ni kuzuia uharibifu mkubwa zaidi. Unapokata mti unakuwa umeharibu mazingira na mti ambao utapanda leo [illegible] kesho ndiyo maana wataalam wanahamasisha kubuni mbinu ambazo zitapunguza kasi ya uharibifu mkubwa wa mazingira.

Watanzania wengi wanatumia nishati inayotokana na mazao ya miti kama vile kuni, mkaa na kujengea mazao ya misitu ambayo ni mbao hivyo basi hapo moja kwa moja uharibifu mkubwa unafanywa kwa kuvuna mazao ya msitu ili kupata kuni, mkaa na mbao.

Katika kukabiliana na hali hiyo inatakiwa binadamu kubuni mbinu mbadala za nishati kama vile kutumia nishati inayotokana na jua, maji, kinyesi cha ng'ombe au nguvu za upepo nishati ambazo kitaalam zinaonekana hazina madhara katika mazingira.

Nishati ya jua ni nishati ambayo tumepewa bure na mwenyezi Mungu na ambayo inakuja moja kwa moja kama nishati mbadala ya kuni ambapo hivi sasa katika nchi nyingi ambazo zimeendelea tayari wameanza kutumia nishati ya jua. Kazi ya kuendesha mitambo mbalimbali kama magari haiwezi kutengwa na mazingira kwa sababu iwapo mitambo ni mibovu inachangia moja kwa moja kufanya uchafuzi wa mazingira ya hewa na moshi kuathiri afya ya binadamu.

Magari yana athari katika hewa na kusababisha hewa ya ukaa kuwa nyingi angani, katika kukabiliana na uharibifu wa hewa hiyo kinachotakiwa wafanyabiashara wote ambao wanaagiza magari wajitahidi kuingiza nchini magari mapya na ambayo yanakidhi viwango.

kuna wimbi la kununua magari ambayo yameshatumika nje ya nchi hivyo yanaingizwa hapa nchini kwa kufuata unafuu wa bei bila kuangalia namna magari hayo yanavyoathiri mazingira kutokana na kutoa moshi mwingi ambao una madhara makubwa kwa binadamu na anga.

Katika nchi ambazo zimeendelea magari yamewekewa muda maalum na baada ya kutumika katika muda fulani mmiliki haruhusuwi kuendelea kulitumia gari hilo tena na endapo atatumia anatozwa kodi kubwa ambayo inamshinda kulipa.

Hata hivyo watanzania walio wengi ni maskini na hawawezi kununua magari mapya badala yake wana uwezo wa kununua magari yaliyotumika na ambayo yana madhara makubwa katika mazingira.

Kinachotakiwa kwa wamiliki wa magari hayo chakavu watalaam wanashauri kutumia kichuja hewa ambacho kitasaidia katika kiwango kikubwa cha kupunguza hewa chafuzi.

Wataalam wanashauri kutumia magari ambayo yanatumia umeme au gesi asilia badala ya mafuta ili kusaidia katika suala la utunzaji wa mazingira, hata hivyo magari ambayo yanatumja umeme ndiyo kwanza yameingia katika nchi tajiri hapa Tanzania magari yanayotumia gesi asilia yapo machache bado hayajaanza kutumika rasmi.

Tukiangalia kazi nyingine ambayo anaifanya binadamu ni utengenezaji wa barabara ambapo wakandarasi wanachimba kokoto na udongo kwa lengo la kutengenezea barabara huku wakiacha mashimo makubwa hivyo kufanya uharibifu mkubwa wa mazingira.

Kutengeneza barabara ni maendeleo kwa kuwa wananchi wanaweza kusafiri na kusafirisha bidhaa mbalimbali hata hivyo inatakiwa kufanya tathmini ya mazingira na kuangalia athari zake kiuchumi .Ni muhimu kupunguza athari za mazingira mara baada ya mradi kumalizika zile sehemu ambazo zimefanyiwa uharibifu mkubwa wa kimazingira

zinarejeshwa katika hali yake ya kawaida. Ingawa katika hali halisi wawekezaji wengi wakishamaliza mradi wa madini wanaacha mashimo bila kufukia.

Kuna sheria mama ya mazingira ya mwaka 2004 ambayo inaongoza utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Sheria hii inaongoza sheria zote za mazingira kwa kutoa adhabu kwa mtu yeyote ambaye anachafua mazingira awe ni mtu binafsi kampuni, kiwanda au taasisi yeyote ambayo inajihusisha na uchafuzi wa mazingira.

Sheria hiyo imetoa mwongozo na kuzipa nguvu zile sheria nyingine kwa mfano sheria ya misitu, sheria ya uvuvi ya mwaka 2003, sheria ya ardhi ambayo pia ina vipengele ambavyo vinahusiana na masuala ya mazingira na kwamba sheria hizo moja kwa moja zinahadhibu pale ambapo taratibu ya masuala ya mazingira yamekiukwa.

Uchunguzi umebaini kuwa wengi wanafanya makosa ya uchafuzi wa mazingira lakini wanaokamatwa na kufikishwa mahakamani ni wachache, kwa mfano kutupa takataka hovyo ni kosa ingawa wengi wanafanya kosa hilo bila kujua sheria inasemaje.

Sheria inasema kila mwananchi anayo haki ya kuishi katika mazingira safi na salama na watu wanatakiwa kuyaona mazingira kuwa yana uhusiano na wao moja kwa moja hivyo mazingira yakiwa na afya bora na binadamu atakuwa na afya.

Uharibifu wa mazingira husababisha madhara mbalimbali ya kiasili yakiwemo matetemeko ya ardhi, ukame, mabadiliko ya tabia ya nchi na mafuriko. Nchi zenye viwanda vikubwa huko ulaya wanafanya uharibifu mkubwa wa mazingira lakini athari zake zinatokea kwa watu masikini wa Afrika na kusababisha mafuriko, ukame, ongezeko la joto, vimbunga na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Ongezeko la joto kitaalam lina mambo mengi mfano binadamu anapofyeka miti anasababisha ongezeko la hewa ya ukaa ambayo inakwenda angani ambako inachanganyika na gesi ambayo inasababisha

Itaendelea Uk. 16

Scanned by CamScanner

Saratani ikigundulika mapema, inatibika



Na Albano Midelo

Zaidi ya Wanawake 5000 katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma walijitokeza kuchunguza saratani ya mlango wa kizazi na matiti, zoezi lililoendeshwa na Chama Cha Madaktari wanawake Tanzania(MEWATA).

Zoezi hilo lilifanyika kwa siku tatu katika uwanja wa Majimaji na Kituo cha Afya Mjimwema Manispaa ya Songea ambapo uzinduzi wa zoezi hilo ulifanywa na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk.Hamis Kigwangalla.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Songea Dk.Mameritha Basike alisema lengo la MEWATA lilikuwa kuwafanyia uchunguzi wa saratani ya mlango wa uzazi na matiti wanawake 3000 ambapo idadi imezidi lengo hilo kutokana na uhamasishaji mkubwa uliofanyika hali iliyosababisha wengi kujitokeza.

Alisema zoezi hilo ambalo lilifanyika kwa siku tatu kuanzia Agosti 24 hadi 26 mwaka huu, limesababisha baadhi ya wanawake kukosa nafasi ya kuchunguzwa ambapo wameomba kuongezewa siku kwa kuwa wanawake wengi kutoka mkoa wa Ruvuma wamefarijika kupata nafasi ya kuchunguzwa jirani ya makazi yao badala ya kugharamia usafiri na malazi hadi jijini Dar es salaam.

Zoezi la uchunguzi wa saratani za mlango wa kizazi, matiti na magonjwa yasioambukiza limewashirikisha madaktari 100 wa MEWATA na kufanyika katika wilaya ya Songea kwa siku tatu.

Rais wa MEWATA Dk.Saraphina Mkuwa anasema kila mwaka hapa nchini wanawake 6000 wanagundulika na saratani ya mlango wa kizazi na matiti kati yao wanawake 4000 wanapoteza maisha kwa kukosa huduma za uchunguzi wa mapema.

"Ni asilimia kumi tu ya wagonjwa hao wanaopata huduma ambapo asilimia 90 ya wagonjwa wanabaki nyumbani na hawapati huduma hivyo wanapoteza maisha", anasisitiza Dk.Mkuwa.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dk.Gosbert Mutayabara alisema ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi na matiti kuwa ni miongoni mwa magonjwa kumi katika mkoa wa Ruvuma yanayoongoza kwa kusababisha vifo.

Takwimu za saratani za mlango wa kizazi na matiti katika mkoa wa Ruvuma zinaonesha kuwa mwaka 2014 kulikuwa na wagonjwa zaidi ya 12,000, mwaka 2015 wagonjwa zaidi ya 17,000 na mwaka 2016 wagonjwa wa saratani walikuwa zaidi ya 18,000.

Chama cha Madaktari Wanawake nchini (MEWATA) kwa kushirikiana na wadau wengine katika miaka ya karibuni vimekuwa mstari wa mbele katika kufanya kampeni kabambe ya kuhakikisha wanawake wanajitokeza kupima ili kutambua mapema iwapo wana saratani ya shingo ya kizazi na matiti ili waweze kupatia matibabu mapema.

Utafiti unaonesha kuwa akinamama zaidi ya 500,000 hupatwa na ugonjwa wa saratani ya uzazi na matiti kila mwaka duniani, kati ya hao akinamama 250,000 hufariki kila mwaka kutokana na ugonjwa huo.

Ugonjwa wa saratani umekuwa tishio katika nchi za Afrika zilizo chini ya Jangwa la Sahara ikiwamo Tanzania ambapo kwa mwaka 2010, takwimu zinaonesha ugonjwa huo uliua watu milioni 9.9 duniani.

Takwimu za shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonesha kuwa ugonjwa wa saratani ni hatari ukilinganisha na takwimu za magonjwa mengine.

Takwimu za WHO za magonjwa za mwaka 2010 zinazoonesha kuwa ugonjwa wa malaria uliua watu 500,000, kifua kikuu milioni 2.1, UKIMWI milioni 1.8 na Saratani iliongoza kwa kuua watu milioni 9.9.

Hata hivyo kwa mujibu wa takwimu hizo asilimia 75 ya watu waliokufa kwa ugonjwa wa saratani sawa na milioni 7.4,walitoka katika nchi zinazoendelea ukiwemo Tanzania.

Kulingana na wataalam, saratani ya matiti ni uvimbe usiokuwa na maumivu ambao mwanamke yeyote anaweza kuwa anao bila ya yeye mwenyewe kujijua na kwamba inashauriwa kila mwanamke awe na ufahamu kuhusu afya yake na mwili wake na kujenga tabia ya kujichunguza mwenyewe mara kwa mara.

Mameritha Basike ni Daktari Mkuu wa Manispaa ya Songea anasema licha ya saratani ya mlango wa kizazi kuongoza kwa kusababisha vifo vingi vya wanawake hapa nchini, hata hivyo saratani hiyo inatibika iwapo ugunduzi utafanyika mapema.

Anazitaja dalili za saratani ya mlango wa kizazi kuwa ni kutokwa na damu baada ya kujamiina, kutokwa na majimaji yenye harufu mbaya, kutokwa na usaha ukeni, kutokwa na damu isiyo ya hedhi na maumivu ya tumbo chini ya kitovu.

Hata hivyo Dk.Basike anabainisha kuwa matibabu ya saratani ya mlango wa kizazi hutolewa kulingana na hatua ya ugonjwa na hali ya mgonjwa ambapo huduma za matibabu hufanyika kwa upasuaji katika hatua za mwanzo za ugonjwa, mionzi na dawa za saratani.

Kwa upande wake Dk.Saraphina Mkuwa ambaye pia ni Rais wa MEWATA akizungumzia saratani ya mlango wa kizazi anasema ni aina ya saratani inayoshambulia chembehai zilizopo kwenye mlango wa kizazi(Cervix) na kwamba saratani hiyo husababishwa na virusi vya papiloma(Human Papiloma Virus). visababishi vya saratani hiyo ni kuanza ngono katika umri mdogo, kufanya ngono na wapenzi wengi, huvutaji wa sigara, tumbaku au ugoro, historia ya kubeba mimba nyingi na kwamba wenye virusi vya UKIMWI wana hatari zaidi ya kupata saratani ya mlango wa kizazi.

Ili kuepukana na saratani hiyo Dk.Mkuwa anasema ni muhimu kupata chanjo dhidi ya virusi vya papiloma, kuepuka ngono katika umri mdogo, kufanyiwa uchunguzi, kuwa na mwenza mmoja mwaminifu, kutumia kondomu kila unapofanya ngono, kuepuka bidhaa za tumbaku na kuepuka kubeba mimba nyingi.

Hata hivyo anasisitiza kuwa saratani hiyo inazuilika iwapo uchunguzi utafanyika mapema kwa lengo la kubaini mabadiliko ya awali ya saratani, ambayo yatawezesha kukinga saratani hiyo na kwamba mabadiliko yanaweza kutibiwa kwa njia ya ugandishaji na upasuaji mdogo kwenye sehemu husika.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema zaidi ya asilimia 70 ya visa vya ugonjwa wa saratani vinaweza kuzuiliwa na kwamba saratani hiyo inaweza kuzuilika ikiwa nchi zitaongeza uwezo wao wa ugunduzi na udhibiti wa saratani za mlango wa kizazi na matiti.

Kwa mujibu wa WHO nusu ya nchi, kote duniani hazina uwezo wa kukabiliana kikamilifu na ugonjwa huo, na wala hazina mpango tekelezi wa kuudhibiti , ambao unajumuisha kuzuia, kugundua mapema, kutibu na huduma za uuguzi.

Takwimu za WHO zinaonesha kuwa watu milioni 7.6 wanafariki dunia kila mwaka kutokana na saratani, huku takriban watu milioni 13 duniani kote wakiwa wanapatikana na saratani kila mwaka.

Scanned by CamScanner

Selous: Pori linaloongoza kwa viumbe adimu duniani

Na Albano Midelo

Pori la akiba la Selous ni moja kati ya vivutio vikubwa vya utalii hapa nchini na endapo lingetangazwa kwa nguvu zote lingeweza kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni na kuongeza pato la taifa.

Selous ni moja kati ya mapori 28 ya Akiba hapa nchini yaliyopo chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA). Pori la Akiba la Selous lenye ukubwa wa kilometa za mraba 50,000 ambazo sawa na asilimia tano ya ardhi yote ya Tanzania Bara linaangukia katika mikoa minne na wilaya kumi.

Mikoa hiyo kwa mujibu wa Meneja wa Pori la Akiba la Selous Mhifadhi Henock Msocha ni Ruvuma, Lindi, Pwani na Morogoro na wilaya ambazo zinapita katika Pori hilo ni Liwale, Kilwa, Rufiji, Kilombero, Morogoro vijijini, Malinyi, Namtumbo, Tunduru na Kisarawe.

Selous ni moja kati ya mapori mengi yaliopo hapa nchini likiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 50,000 likijumuisha maeneo ya ardhi oevu, misitu ya miombo, tambarare, nyasi za kuvutia, maziwa na mito inayotiririka na kuwa kivutio. Msocha anabainisha zaidi kuwa kutokana na ukubwa wa pori hilo, limegawanywa katika kanda nane ili kurahisisha shughuli za usimamizi na utendaji kazi.

Anazitaja kanda hizo kuwa ni Kanda ya Kaskazini (Matambwe), Kanda ya Kaskazini Mashariki (Kingupira), Kanda ya Mashariki (Miguruwe), Kanda ya Kaskazini Magharibi (Msolwa), Kanda ya Kusini (Likuyuseka maganga) na Kanda ya Magharibi (Ilonga).

Pori la Akiba la Selous lilianzishwa mwaka 1896 na Wajerumani likiwa pori la kwanza kutengwa kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori barani Afrika na la pili kwa ukubwa duniani baada ya pori la Marekani ambalo linaitwa Yellowstone National Park.

Historia inaonesha kuwa jina la Selous limetokana



na askari ambaye alikuwa ni mvumbuzi wa kiingereza aliyeitwa kapteni Fredrick Selous aliyefariki Januari 04, mwaka 1917 wakati anapigana vita ya pili ya Dunia na kuzikwa katika eneo la Behobeho lililopo ndani ya pori la Selous .

Pori la Akiba Selous lina utajiri wa viumbe adimu katika sura ya dunia kama vile nyani aina ya sanje, mbega mwekundu, faru mweusi ambaye yupo hatarini kutoweka na wanyama wengine wakiwemo ndege, wadudu na mimea ambayo haipatikani sehemu nyingine yeyote duniani.

Kutokana na umuhimu wa pori la Selous Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Utamaduni na Sayansi (UNESCO) limelihorodhesha pori hilo kuwa ni moja ya maeneo

Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe alisema Pori la Selous lenye idadi kubwa ya tembo ni mapito ya wanyama yaani ushoroba wa tembo ambao wanatoka katika pori hilo kupitia pori la Akiba la Liparamba na kuingia hifadhi ya Niassa nchini Msumbiji.

"Selous ndiyo pori la Akiba linalosifika kuwa na uoto wa kuvutia wa miombo na idadi kubwa ya wayama aina ya Tembo hali inayosababisha wakati mwingine wanyama hao kutoka nje ya pori na kwenda katika makazi ya watu na kusababisha uharibifu wa mali",anasema Challe.

Takwimu zinaonesha kuwa katika pori hilo hadi kufikia mwaka 2007 kulikuwa na Tembo zaidi ya 70,000 hata hivyo idadi ya tembo katika pori hilo ilishuka kutokana na kukithiri kwa ujangili hadi kufikia tembo 43,000 mwaka 2009.

Hata hivyo idadi ya tembo katika pori hilo hivi sasa inaongezeka kwa kasi baada ya kuwadhibiti majangili. Meneja wa Pori hilo Henock Msocha anasema ili kuhakikisha ujangili unadhibitiwa katika pori hilo, inafanyika doria ndefu na fupi katika kanda zote nane na kwenye maeneo ya pembezoni.

Kanda kwa ajili ya kutekeleza kazi za doria kwa kupishana na hivyo kuhakikisha kuwa pori lipo chini ya ulinzi wakati wote", alisisitiza Msocha.

Aliongeza kuwa doria za ushirikiano zimefanyika kwa kuhusisha askari wa Pori la Akiba Selous na askari wa Halmashauri za Wilaya zinazozunguka pori hilo kwa kushirikiana na askari wa kikosi Dhidi ya Ujangili (KDU), Wakala wa Misitu (TFS) na Jeshi la polisi. Mafanikio ambayo tayari yamepatikana katika uwindaji wa kitalii kupitia pori hilo ni pamoja na Tanzania kufikiwa na watalii wawindaji 662 katika pori hilo mwaka 2005, mwaka 2006 watalii 437 na mwaka 2007 watalii 549.

Kulingana na Msocha katika kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Juni 2017 jumla ya doria 2179 zilitekelezwa na kwamba ongezeko la doria hizo limetokana na uboreshaji wa miundombinu ya doria na vitendeakazi ikiwemo ongezeko la magari kwa ajili ya doria.

"Katika kipindi hicho tumekamata jumla ya majangili 520 kwa makosa mbalimbali kinyume cha sheria ya kuhifadhi wanyamapori na kanuni zake, vitendo hivyo vinajumuisha kuingia ndani ya pori bila kibali, kuwinda wanyamapori bila kibali, kutega wanyama, kuvua samaki na kuingiza mifugo na uvunaji haramu wa mazao ya misitu",alisema Msocha.

Kwa mujibu wa Meneja, idadi ya watalii wa picha 55,197 walitembelea katika pori hilo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka

Anabainisha zaidi k
Pori la akiba la Selou
viwanja vya ndeg
vinavyotumika na
huduma kwa watal
picha, wawindaji wa
na kazi za utawala.

Katika kipindi
walikamata
mbalimbali vya kuf
ujangili ikiwemo bu
20 za aina mbalimbali
747 za kutega wany
pikipiki 14, magari m
baiskeli 59, misume
kuchania mbao 16, m
tisa, nyavu za ku
samaki 204 na mitu
106.

Pamoja na mafanikio
pori la Akiba la S
linakabiliwa
changamoto mbali
zikiwemo baadhi
barabara zake kuto
kutokana na kutofa
matengenezo w
muafa
kunakosababishwa
ufinyu wa bajeti ya W
ya Maliasili na Utali

Meneja huyo anas
tathmini inaonesha
idadi ya maj
waliokamatwa mwa
fedha wa 2016/
imeongezeka kwa as
12 ikilinganishwa na
ya mwaka wa fedh
2015/2016.

Anasema ongezeko
limetokana na kuong
kwa idadi ya doria
1692 mwaka 2015/
hadi kufikia doria
mwaka 2016/201
kwamba jumla ya kes
zilifunguliwa katika
vya polisi vilivyopo k
wilaya zinazopakar
pori hilo.

"Juhudi hizi zimewe
kudhibiti vitendo
ujangili katika kiw
kikubwa,
iliyosababisha matul
vifo vya tembo kutok
ujangili yamepu
kutoka tembo 17 n
2015/2016 hadi k
tembo wanane m
2016/2017",ana
Msocha.

Akizungumzia usim
wa matumizi

Scanned by CamScanner

HABARILEO IJUMAA JUNI 9, 2017

Hatima ya dunia na mabadiliko ya tabianchi

Na Albano Midelo

DUNIA inakabiliwa na changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi, hali ambayo inatanya sayari hii kuwa nja panda.

Kutokana na hali hiyo viongozi wa nchi na serikali wa mataifa 150 duniani, Desemba 2015 walifanya mkutano wa kilele wa mabadiliko ya tabia mjini Paris nchini Ufaransa, wakajiwasha dhamana ya mpango wa kihistoria wa kuepusha maafa ya ongezeko la joto duniani.

Viongozi hao walipendekeza mpango wa kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotanywa na binadamu na kuepusha athari mbaya zaidi za mabadiliko ya tabia nchi ambazo zinaweza kuangamiza viumbe hai wote duniani.

Katika mkutano huo ulioshirikisha watu zaidi ya 900 walifikia makubaliano ya kupunguza joto duniani, baada ya jitihada za muukumo wa awali wa viongozi wa dunia kutoonesha matarajio ya kutosha.

Miongoni mwa vikwazo vilivyokwamusha makubaliano ya awali ni nafasi ya mataifa mawili makubwa yenye kuelezwa kufanya uchafuzi mkubwa wa mazingira China na Marekani kufanya jitihada ndogo katika utekelezaji wa jitihada za ustawi wa mazingira.

China imeahidi kutekeleza muukumu yake katika makubaliano yaliyowekwa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi licha ya kuwa Marekani hatoshiriki katika makubaliano hayo.

Akizungumza nchini Ujerumani, Waziri Mkuu wa China, Li Keqiang amekaririwa na vyombo vya habari vya kimataifa akisema kuwa nchi yake, inataka kuwa nchi ya kupegwa mfano katika harakati za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, hatua ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi imeingia dosari mwishoni mwa Mei mwaka huu baada ya Rais wa Marekani, Donald Trump kutangaza nia ya kujiondoa katika makubaliano ya Paris ya mwaka 2015 kuhusu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Nchi saba tajiri (G7) zenye maendeleo makubwa ya viwanda na demokrasia zimekutana katika mkutano wa kilele huko Sicily nchini Italia na kwamba kati ya viongozi wa nchi hizo ni viongozi sita tu ambao walikubaliana kuunga mkono mfumo wa makubaliano ya Paris

Marekani ambalo ni taifa kubwa lenye viwanda vingi limekataa kuunga mkono mkataba wa mabadiliko ya tabianchi ya Paris, yaliyotiwa saini miaka miwili iliyopita ili kupunguza hali ya joto duniani.

Kwa mujibu wa Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani, Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel amemkosoa Rais Trump kwa kutounga mkono makubaliano ya Paris.

"Mjadala mzima wa mabadiliko ya tabia nchi ulikuwa mgumu nashangaa kuona ni kwa nini Rais Trump pekee ndio hajakubaliana na makubaliano hayo", anasema Kansela Merkel.

Rais mstaafu wa Marekani, Barack Obama mwaka 2015 aliunga mkono makubaliano ya Paris licha ya bunge la taifa lake kukaidi, na nchi ya China imeahidi kudhibiti uzalishaji wa hewa chafu kwa kiwango kikubwa ifikapo 2030. Licha ya Rais Trump kujiondoa kwenye mkataba wa Paris lakini kimsingi mataifa mawili ya Marekani na China yanaongoza kwa kuchafua zaidi mazingira duniani.

Takwimu zinaonesha kuwa China inafanya uchafuzi wa mazingira kwa kutoa asilimia 30 ya hewa chafu duniani na Marekani asilimia 16.

Mataifa makubwa 20 yametangaza jitihada za kuongeza bajeti yake ya kufanya utafiti maradufu katika nishati mbadala.

Biliones mkubwa mfanyabiashara katika tasnia ya teknolojia wa Marekani Bill Gates amekwishaonesha azma ya kuunga mkono kazi hiyo ya tafiti.

Rais mstaafu wa Ufaransa, François Hollande, amekaririwa na vyombo vya habari akisema hali ya baadaye ya binadamu iko hatarini na kuonya kuwa serikali zitalaumiwa iwapo viongozi watashindwa kufanya maamuzi muhimu kwa kuwa kuongezeka kwa joto la dunia kunaweza kuangamiza viumbe hai wote duniani.

Tanzania tayari imaathirika na uwepo wa mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ukame wa muda mrefu unaojirudia rudia ambao unaambatana na athari kubwa katika kilimo, usafirishaji, nishati, biashara na sekta mbalimbali za uchumi wa jamii.

Hivi sasa zaidi ya asilimia 70 ya majanga yote ya asili katika Tanzania yanatokana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ukame na mafuriko.

Mifano ya matokeo ya mabadiliko ya tabianchi ipo mingi ikiwemo mafuriko yaliyotokea Dar es Salaam Desemba 21 hadi 23 mwaka 2011 na kuua zaidi ya watu 40, yakiharibu nyumba nyingi na miundo mbinu.

Ukurta wa mto Pangani ulivyoathiriwa na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Ongezeko la joto angani litokanalo na mabadiliko ya tabia nchi, limechangia uyeyukaji wa theluji katika mlima Kilimanjaro.

Matukio mengine ya Kilosa, mkoa wa Morogoro, Singida, Kilimanjaro, Geita na Mbozi, mkoa wa Mbeya katika miaka ya 2006 na 2008 na mkoa wa Kagera mwaka 2016.

Wataalamu wanasema ongezeko la joto duniani linalosababisha kuibuka kwa magonjwa mapya kwa mamilioni ya watu, hasa yale yanayoenezwa na vimelea na bakteria ikiwemo magonjwa kama vile malaria katika maeneo yenye baridi na milima ambako kwa asili hayakuwepo.

Takwimu za Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania, zinaonesha kuwa wastani wa joto kwa mwaka katika mikoa ya Mbeya na Iringa limeongezeka kwa nyuzi joto mbili za sentigredi katika kipindi cha miaka 50 iliyopita (1963 – 2007).

Kwa upande mwingine, ongezeko la joto angani na upungufu wa mvua, vimeendelea kuchangia uyeyukaji wa barafu au theluji katika mlima Kilimanjaro.

Inakadiriwa kuwa tangu 1912 hadi mwaka 2015, takribani kati ya asilimia tano hadi 85 ya kiwango cha theluji katika mlima Kilimanjaro tayari imeyeyuka na kupotea.

Inakadiriwa kuwa, kama hali ya hewa itaendelea kama ilivyo sasa, kiwango cha theluji kilichobaki katika mlima Kilimanjaro kitakwisha na kupotea kabisa hadi kufikia mwaka 2020.

Mabadiliko ya tabia nchi pia yamesababisha kuongezeka kwa usawa wa kina cha bahari, ambapo tayari kuta za kuzuia maji ya bahari zimeharibiwa na kusababisha maji kuingia maeneo ya watu katika sehemu za Pangani (Tanga) na Kunduchi (Dar es Salaam).

Ongezeko la joto pia limesababisha uzamaji wa maeneo na baadhi ya visiwa katika bahari ya India kama vile kisiwa cha Maziwe na Fungu la Nyani na uharibifu wa maisha katika mfumo wa bahari ikiwemo mimea inayolisha na kutumika kama mazalia ya samaki kwa viumbe wa baharini.

Tafiti mbalimbali zinazohusu mwelekeo wa joto wa muda mrefu katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa, zinaonesha ongezeko la joto katika maji ya kina kirefu kati ya nyuzi joto za sentigredi 0.2 mpaka 0.7 kuanzia mwanzoni mwa 1900.

Shughuli mbalimbali za binadamu zinasababisha ongezeko la viwango vya hewa ukaa inayoongeza joto kama vile carbon dioxide, methane, nitrogen dioxide, na chlorofluorocarbons.

Wataalamu wa mazingira wanasisitiza kuwa udhibiti wa muda mrefu wa ongezeko la viwango vya hewa ukaa katika anga ni wa muhimu kwa sababu ndivyo vinavyosharabu mionzi inayotoka duniani na kuinasa ili kuongeza joto la dunia mpaka kiwango kinachoruhusu maisha kuendelea.

Upunguzaji wa hewa ukaa kwa mujibu wa wataalamu ni jambo la lazima kwa kila sekta kuwezesha uwezo wa mataifa yote kustahimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mhumo asilia wa ikolojia unatoa fursa muhimu wa kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa kwa haraka na kutunza uwezo wa sayari dunia kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Ongezeko kubwa la hewa ukaa angani linasababisha mabadiliko ya tabianchi yenye uwezo wa kuangamiza nchi mbalimbali duniani.

Watalaamu wanasema mfumo wa nishati wa dunia unahusika kwa zaidi ya nusu ya hewa ukaa yote inayozalishwa duniani. Sehemu kubwa ya hewa joto hizi ni hewa ukaa (CO2) na methane.

Sehemu kubwa ya uzalishaji wa hewa joto hizi unatokana na matumizi ya mafuta ya petroli katika aina zake zote kama chanzo cha nishati.

Kuongezeka kwa hewa ukaa angani kunasababisha kuongezeka kwa joto la anga ambalo wataalam wamendhika linahusika na mabadiliko ya tabianchi na kuleta madhara makubwa katika mazingira.

Uchomaji na ukataji wa misitu kwa ajili ya malisho, makazi na shughuli zingine za kiuchumi ni chanzo kingine kikubwa cha uzalishaji wa hewa ukaa angani, vitendo hivyo vinachangia takribani asilimia 16 ya uzalishaji wa hewa ukaa yote duniani.

Hii ni sawa na hewa ukaa yote inayozalishwa na magari yote duniani, malori, melt, matreni na ndege vikiunganishwa pamoja.

Mwandishi ni Mchangiaji wa gazeti hili mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com,Simu 0784765917.

Scanned by CamScanner

Gesimasowa: Hifadhi yenye mazalio ya samaki wa kipekee

Na Albano Midelo

MKOA wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa nchini ambayo imebarikiwa kwa kuwa na neema ya vivutio lukuki na adimu vya utalii wa ikolojia na kiutamaduni.

Hifadhi ya Gesimasowa yenye ukubwa wa kilometa za mraba zaidi ya 700 ambayo ipo katika Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea, ni miongoni mwa vivutio adimu vya utalii.

Hifadhi hiyo ilianzishwa kama msitu wa hifadhi mwaka 1975 na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma wa zamani, marehemu Dk Lawrence Gama.

Mwaka 2015, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma katika kipindi marehemu Said Mwambungu alisimamia mchakato wa kupandisha hadhi msitu huo na kuwa hifadhi ya Taifa.

Moja ya vivutio vilivyopo katika hifadhi hii ni mapumziko ya ndege maarufu duniani wanazaliana katika Hifadhi ya Taifa ya Kitulo iliyopo Makete mkoani Njombe wanaitwa kitaalamu Derhams wenye uwezo wa kuruka toka bara moja hadi bara jingine.

Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe anabainisha kuwa ndege hao wanapumzika eneo hilo kwa miezi kadhaa kisha wanaendelea na safari kupitia Bonde la ufa hadi Ziwa Nyasa hatimaye wanasafiri hadi Afrika ya Kusini.

Kulingana na Challe, hifadhi ya Gesimasowa ni mapito ya ndege hao ambao wanatoka Kaskazini mwa Afrika kuelekea Afrika ya Kusini ambao wanafuata milima ya Livingstone iliyopo Ziwa Nyasa na kwamba ndege hao pia wanapumzika Mwambao mwa Ziwa Nyasa hasa katika eneo la Kihagara ambapo kuna mazingira ambayo yanavutia ndege hao kuishi.

Kwa mujibu wa Challe, Hifadhi ya Gesimasowa pia ina mfumo wa ikolojia wa pori la Selous kwa sababu ni mapitio ya wanyamapori wanaotoka katika Pori la Akiba la Selous wanapita kuelekea Bonde la Ziwa Nyasa kupitia pori la Liparamba hadi Hifadhi ya Niasa nchini Msumbiji ambapo wanyama wanakwenda nchini Msumbiji na kurudi Tanzania.

Wanyama ambao unaweza kuwaona katika hifadhi ya Gesimasoa ni tembo, simba, ndege, nyati, pofu na samaki adimu duniani aina ya mbelele na mbasa.

Hifadhi hii pia ni maingiliano ya mito miwili ya Hanga na Lutukira ambayo inatengeneza mto Ruhuhu unaomwaga maji yake ziwa Nyasa.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema akiweka jiwe la msingi katika uwekaji wa alama za kudumu katika hifadhi ya Gesimasoa.

Mto huo ndiyo mazalia ya samaki aina ya mbelele na mbasa ambao katika duniani nzima wanapatikana ziwa Nyasa pekee.

"Samaki hawa ni adimu sana kwa sababu utafiti umebaini samaki hawa wanapatikana ziwa Nyasa pekee na wanazaliana katika mto Ruhuhu ambao unachangia asilimia 20 ya maji katika ziwa Nyasa," anasema Challe.

Utafiti wa samaki aina mbasa na mbelele katika mto Ruhuhu na Ziwa Nyasa ulifanywa na Fransis Challe mwaka 2010 ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kitivo cha Sayansi, Teknolojia na Mazingira na chapisho la utafiti huo lilitolewa mwaka 2011.

Hata Challe anasema wavuvi katika ziwa Nyasa wanafanya uharibifu wa mazingira kwenye maingiliano ya mto Ruhuhu na ziwa Nyasa eneo la Folkland Lituhi ambapo wanaharibu vifaranga wa samaki hao ambao wanaingia katika ziwa Nyasa.

Uchunguzi umebaini kuwa katika hifadhi ya Gesimasowa ambako samaki wanazaliana wanachi wamefanya uharibifu mkubwa wa mazingira kwa kukata miti ambayo ni muhimu katika chanzo hicho cha mto Ruhuhu.

Kwa upande wake Meneja wa mapori ya Akiba ya Gesimasoa, Litumbandyosi na Liparamba, Richard Bwire anasisitiza kuwa eneo la maingiliano ya mto Hanga na Mto Lutukira lililopo katika Hifadhi ya Gesimasowa linatakiwa kulindwa na kuhifadhiwa.

"Samaki wanazaliana hapa kwenye Maingilio ya mito, kisha wanasafiri hadi ziwa Nyasa na kuendelea na maisha ambapo wakati wa kuzaliana samaki hao wanarudi tena hapa. Hivyo hili ni eneo muhimu sana kitaifa na kimataifa katika Uhifadhi na utalii kwa kuwa samaki hao hawapatikani sehemu nyingine yoyote Duniani," anasema Bwire.

Hata hivyo anasema mapori ya hifadhi ya Gesimasowa, Litumbandyosi na Liparamba bado ni mapya na kwamba lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa maliasili zilizopo katika mapori hayo zinalindwa ili ziwe endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

"Haya maeneo yote mwanzoni yalikuwa ni hifadhi ya mistu lakini hivi sasa ni hifadhi na mapori ya wanyamapori kulingana na sheria ya wanyamapori namba tatu ya mwaka 2009 na wananchi hawaruhusu kufanya shughuli zozote ndani ya hifadhi hizo."

Hata hivyo anasema kwa muda mrefu kumekuwa na mgongano na wananchi, wakulima kwa wafugaji wamekuwa wanavamia kwa makusudi mapori haya na kufanya shughuli kinyume cha sheria.

"Wananchi wanajua kabisa hizi ni hifadhi kisheria, hivi sasa tunatekeleza maagizo ya Waziri Mkuu kuhakikisha kuwa wavamizi wote wa maeneo ya hifadhi tunawaondoa," anasema Bwire.

Kwa mujibu wa Mhifadhi huyo hivi sasa wanyamapori wanahama toka pori la Selous, wakipitia hifadhi ya Gesimasowa, hifadhi ya Litumbandyosi, Liparamba na kuvuka mpaka hadi hifadhi ya Niassa nchini Msumbiji na kwamba wanyama wanapopita wanafanya uharibifu wa mazao ya wananchi ambayo bado hayajavunwa.

Anasisitiza kuwa mapito ya wanyamapori yamesababisha mgogoro na wananchi wenye mazao ambao wamechelewa kuvuna mazao yao hivyo kuharibiwa na wanyama kama tembo ambao wanakula mahindi na maboga.

Akizungumzia hatua ambazo Idara ya Maliasili na Utalii inazichukua ili kuhakikisha hifadhi hizo zinalindwa, Afisa Maliasili na Utalii, Afrikanus Challe anasema serikali imeanza kuchukua hatua ikiwemo kuweka alama kubwa za kudumu ili kutengenisha maeneo ya hifadhi na wananchi.

"Tumeanza kutoa elimu kwa wananchi wavue samaki kitaalamu bila kuathiri mazalio ya samaki kwa kufuata nyavu zenye matundu yanayokubalika kisheria na kwamba endapo mazalia ya samaki yataharibiwa samaki hao wanaweza kutoweka duniani," anasema.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema ambaye hifadhi ya Gesimasowa ipo katika wilaya yake anatoa rai kwa wananchi kuacha kukata miti kwenye kingo za mito na kuacha kuvua samaki kwa kutumia nyavu haramu kwenye maingiliano ya mto Ruhuhu ili samaki aina ya mbasa na mbelele wasitoweke duniani.

Mgema anasema tayari wametekeleza agizo la serikali la kuweka mipaka kwenye hifadhi za misitu, mapori na kwenye mapito ya wanyamapori ili kuwadhibiti wananchi wanaovamia maeneo ya hifadhi na kufanya uharibifu mkubwa.

"Vijiji vingi vinavyopakana na hifadhi vinakuwa havijui mipaka yao, ndiyo maana serikali imeamua kufanya zoezi la kuweka alama za kudumu zinazooneka kwenye maeneo yote ili kuondoa hisia za wananchi kuchukuliwa maeneo yao," anasema Mgema.

Anasisitiza kuwa baada ya kukamilisha kazi ya kuweka alama za kudumu katika hifadhi zote, serikali itaanza mara moja kuwaondoa wafugaji wote waliovamia maeneo ya hifadhi na kwamba jiwe la kwanza la alama ya kudumu limejengwa kwenye makutano ya mto Lutukira ili kutenganisha vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo ambayo ni mapito ya wanyamapori.

Samaki aina ya mbelele ambao mazalio yake yapo katika hifadhi ya Gesimasowa

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili, mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com, simu 0784765917

Scanned by CamScanner

Watu milioni 415 wanaugua kisukari

Na Albano Midelo

TAKWIMU za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonesha kuwa jumla ya watu milioni 451 duniani kote wanaugua ugonjwa wa kisukari.

WHO inabainisha kuwa tatizo la kisukari linaongezeka kwa kasi. Takwimu za mwaka 2007 zinaonesha kuwa kulikuwa na wagonjwa milioni 246 duniani kote.

Katika Afrika, mwaka 2015 kulikuwa na wagonjwa wa kisukari milioni 14.2. Idadi inatarajiwa kuongezeka hadi kufikia watu milioni 34.2 na dunia nzima inatarajiwa kuwa na wagonjwa wa kisukari milioni 642 ifikapo mwaka 2040.

Takwimu za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto zinaonesha kuwa mwaka 2015, Tanzania ilikuwa na wagonjwa wa kisukari 822,880.

Utafiti wa wizara uliofanyika katika wilaya 50 nchini ulibaini asilimia 9.1 ya watanzania wenye umri kati ya miaka 25 na 64 wanaugua kisukari.

Kulingana na utafiti huo, kila watu 100, watu 36 wanaugua kisukari. Hali hiyo inaonesha kuwa tatizo la ugonjwa huo linatakiwa kupatiwa ufumbuzi wa haraka.

Miongoni mwa ushauri wa kitaalamu ili kukabili ugonjwa huu, ni pamoja na kuwapo elimu ya mara kwa mara kupambana na ugonjwa huo.

Kufanya mazoezi na kupima magonjwa yasiombukiza yakiwemo kisukari na saratani, ni mambo muhimu ya kupambana na matatizo hayo ya kiafya.

Ili kuhakikisha inapambana na magonjwa yasiyoambukiza, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeongeza mpango wa kuboresha huduma za msingi za afya kuanzia ngazi ya msingi ili kuweka kinga na tiba.

Geofrey Mdede ni Daktari wa Magonjwa ya Kisukari katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma anasema kisukari ni ugonjwa sugu unaotokana na sukari kuwa juu kwa muda mrefu kwenye damu.

Kwa mujibu wa Dk Mdede, zipo aina mbili za kisukari. Katika aina ya kwanza, mtu anakuwa amezaliwa na kongosho lisilo na uwezo wa kutoa kiasi cha kutosha cha kichocheo cha insulin.

Wagonjwa wa aina hii kwa kawaida huhitaji kuwa wanachoma sindano za vichocheo vya insulin katika maisha yao yote.

Anasema katika aina hiyo ya kwanza ya ugonjwa wa kisukari, wagonjwa hugundulika mapema wakati wa utoto au wakati wa ukuaji.

Aina ya pili ya ugonjwa huu ni ile ambao huwapata watu kuanzia umri wa miaka 45. Aina hii ya kisukari husababishwa na aina ya maisha ya mtu na vyakula vyake.



Baadhi ya wananchi wakijitokeza kupimwa magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kisukari katika Uwanja wa Majimaji mjini Songea.

Licha ya kwamba tatizo la ugonjwa wa kisukari ni la kidunia, Daktari wa Magonjwa ya Moyo na Kisukari katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma, Dk.Mdede anasema hadi sasa wamesajili wagonjwa zaidi ya 500 wa kisukari ambao wanapata matibabu bure.

Anataja dalili kuu za mtu mwenye kisukari kuwa ni kunywa maji sana, kupata kiu mara kwa mara, kuwa na njaa mara kwa mara na kukojoa mara nyingi.

"Ugonjwa wa kisukari unaligharimu Taifa mabilioni ya shilingi, inakadiriwa mgonjwa mmoja wa kisukari anagharimu Sh 210,000 kwa mwezi, mzigo ambao unabebwa na serikali kwa sababu inatoa matibabu bure ya kisukari," anasema Dk Mdede.

> "Ugonjwa wa kisukari unaligharimu Taifa mabilioni ya shilingi, inakadiriwa mgonjwa mmoja wa kisukari anagharimu Sh 210,000 kwa mwezi, mzigo ambao unabebwa na serikali kwa sababu inatoa matibabu bure ya kisukari," anasema Dk Mdede.

Hata hivyo daktari huyo wa magonjwa ya kisukari anasema ugonjwa huo kwa kiasi kikubwa unasababishwa na uzembe na uleji mbaya.

Anatoa rai kwa watanzania kubadilika kimtazamo na kifikra, wale vyakula vinavyoshauriwa na wataalamu na kufanya mazoezi walau dakika 30 kwa siku ili kupunguza uwezekano wa kupata magonjwa ya kisukari, moyo na shinikizo la damu.

"Utafiti unaonesha kuwa kufanya mazoezi kwa dakika 30 kila siku kunapunguza uwezekano wa kufa kizembe kwa asilimia 14 kutokana na magonjwa yasiyoambukiza", anasema Dk Mdede.

Takwimu za WHO zinaonesha kuwa hadi kufikia mwaka 2016, kuna watu milioni 422 duniani wanaougua ugonjwa wa kisukari.

Zinaonesha mwaka 2013 kulikuwa na wagonjwa wa kisukari milioni 382 na mwaka 1980 wagonjwa wa kisukari duniani walikuwa milioni 108.

Kutokana na takwimu hizo, inaonesha kila mwaka kuna ongezeko la wagonjwa wa kisukari milioni 13.

Dk Mdede anasema kumekuwa na kubadilika kwa umri wa ugonjwa wa kisukari ambapo asilimia 8.5 ni watu wazima, ongezeko ambalo ni maradufu ukilinganisha na mwaka 1980 ilikuwa ni asilimia 4.7 ya watu wazima wenye kisukari.

Ugonjwa wa kisukari unazikabili nchi mbalimbali Tanzania miongoni mwa nchi 32 ambazo ni mwanachama wa Shirikisho la Kisukari Duniani (IDF).

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili, mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917

Kama Mzazi

Na Nicodemus Ikonko

Kampeni dhidi ya mimba za utotoni iimarishwe

SAFU hii wiki iliyopita ilizungumzia umuhimu wa kukabiliana na changamoto za mimba za utotoni kwa vitendo kutokana na uhalisia wa hali inayoisonga jamii yetu kwa watoto wetu wa kike kiasi cha kuacha kuzingatia ipasavyo elimu ambayo ni ufunguo wa maisha kwa kila binadamu.

Kama Mzazi ilisukumwa na taarifa kwamba mikoa mitano nchini ndiyo vinara wa kuwa na asilimia kubwa za watoto wa kike wanaopata mimba huku wakiwa na umri mdogo tena pia wakiwa bado wako shuleni wakisoma.

Mikoa hiyo na asilimia iliyonazo kwa tatizo hilo ambalo ni kero kubwa kwa wazazi,walezi na jamii kwa ujumla ni pamoja na Katavi (45), Tabora (43), Dodoma (39) Mara (37) na Shinyanga (34) . Kiwango cha mimba za utotoni kitaifa ni asilimia 27. Wengi wao hupata mimba hizo wakiwa na umri wa chini ya miaka 18.

Kama Mzazi wiki hii inapenda kuanza kwa kutoa pongezi kwa serikali kwa kuamua kwa makusudi kuagiza shule zote za msingi na sekondari nchini kuanzisha madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule zao kuwezesha kupata mahali pa kukimbilia kutoa taarifa pindi wakikumbwa na dhahama.

Sambamba na hatua hiyo, Kama Mzazi imekumwa zaidi na uzinduzi wa kampeni ya miaka 10 ya Tanzania Bara, kuhakikisha kwamba inatokomeza mimba za utotoni na kuhamasisha watoto wa kike kujilinda, kujithamini na kujipenda ili kufikia matarajio yao.

Hongera Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu kwa kutoa maagizo hayo muhimu wiki iliyopita katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Mara.

Inatia moyo kuona kwamba taarifa kwenye vyombo vya habari zilizokuwa zinatolewa kila mara na kuonesha kwamba hali ya watoto wa kike kupewa ujauzito na kisha kutimuliwa shule zimeleta hamasa ya kuchukuliwa hatua za kukabiliana na hali hiyo kwa vitendo bila kuleta ajizi.

Karibu kila wilaya na mkoa unakabiliwa na tatizo hilo kiasi cha kuiweka jamii katika kero kubwa ya kutokuwa na namna nyingine ya kufanya isipokuwa kuchukua hatua kwa kulivalia njuga tatizo hili kwa lengo la kulipatia suluhisho la kudumu.

Kuendelea kulikumbatia tatizo hilo ni sawa na kuukumbatia umasikini kwa sababu wanaopata ujauzito tayari wamepoteza ufunguo wa maisha yao ambao ni elimu na hivyo kujikita moja kwa moja katika lindi la umasikini. Kwa kasi hii, katika miaka 10 au 20 ijayo, tutakuwa na jamii ya aina gani?

Kama Mzazi inapenda kuwakumbusha wazazi,walezi na jamii kwa ujumla wake kushirikiana kwa kuhakikisha kwamba madawati ya ulinzi na usalama wa watoto yanaanzishwa katika shule zote za msingi na sekondari na pia kampeni ya kutokomesza mimba za utotoni inafanyika kwa umakini unaohitajika bila kufanya ajizi.

Scanned by CamScanner

Bustani ya wanyama ya Lugari ina vivutio vya aina zote

Na Albano Midelo

MILANGO ya utalii katika mkoa wa Ruvuma imeanza kufunguka baada ya serikali kujenga miundombinu ya barabara na kuanzisha usafiri anga unaovutia watalii na wawekezaji binafsi katika sekta ya utalii.

Uwepo wa miundombinu bora ya usafirishaji katika mkoa wa Ruvuma unavutia wawekezaji kuwekeza katika mkoa wa Ruvuma ikiwemo kuanzisha vituo vya utalii.

Sekta ya utalii sasa imeanza kupata mafanikio makubwa kwa sababu mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa michache yenye vivutio vya utalii wa ikolojia na kiutamaduni.

Moja ya maeneo ambayo yanavutia wengi kutembelea na kufanya utalii wa aina mbalimbali ni bustani ya wanyama ya Lugari (Lugari Zoo) yenye ukubwa wa hekta 200 iliyopo katika Kijiji cha Tugutu wilayani Mbinga takribani.

Bustani hiyo ya wanyama ilianzishwa na Samwel Ndomba mwaka 2013 baada ya kuomba kibali serikalini. Alipewa leseni ya daraja la 17 ambalo ni maalumu kwa ufugaji wa wanyamapori kwa ajili ya mafunzo na utafiti.

Meneja wa Lugari Zoo, Samwel Ndomba anasema eneo la mradi wa bustani hiyo lina jumla ya hekari 46 ambazo zinaweza kuhifadhi wanyama na ndege zaidi ya aina 200 wakiwemo tausi, njiwa, kasuku, tai na aina nyingine.

Anasema jina la Lugari limetokana na jina la kijiji ambacho amezaliwa mwanzilishi wa bustani hiyo. Anataja lengo la kutumia jina hilo kuwa ni kuenzi kijiji chake.

Ndomba analitaja wazo la kuanzisha mradi huo kuwa lilipewa kipaumbele baada ya kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa mkurugenzi wa wanyamapori Tanzania.

"Mkurugenzi alishauri kuwa na eneo la kutosha kwa sababu mwanzoni wakati tunataka kuanzisha mradi huu tulikuwa na eneo lenye ukubwa wa ekari tatu tu hivyo tulishauriwa eneo hili lipanuliwe ili kukidhi mahitaji," anasema Ndomba.

Anabainisha zaidi kuwa ujenzi wa bustani pia ulizingatia tathmini ya mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira ili kuhakikisha mradi huo unakuwa endelevu.

Madhumuni ya kuanzisha bustani hiyo yanatajwa kuwa ni kuhifadhi wanyamapori na mazingira yake, kutoa elimu ya uhifadhi na kukuza utalii wa ndani na nje.

Madhumuni mengine ni kuzalisha wanyama katika eneo hilo na wanyama hao wanapoongezeka wanarudishwa katika mazingira yao ya asili ili kuongeza idadi.

Idadi imekuwa ikipungua kutokana na uharibifu wa mazingira ambao unapunguza wanyamapori katika mazingira yao ya asili.

Akizungumzia namna mradi wa bustani unavyotekelezwa, Ndomba anasema umeanza kwa ujenzi wa mabanda ya kutunzia wanyama. Yana kilometa moja za mraba kwa mzunguko.

Luteni Jenerali mstaafu, Samwel Ndomba akimuonesha Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii na wakurugenzi eneo huru la wanyama waliopo bustani ya Lugari.

> "Eneo letu huru ambako tumeweka wanyama wakitembea huria, kulikuwa na nyoka wengi aina ya kobra ambao walikuwa wanawadhuru baadhi ya wanyama."

Anasema eneo hilo ni kwa ajili ya viumbehai waliodhibitiwa kitaalamu wasitoke. Wanyama waliopo katika eneo hilo ni chui, chatu, mamba, kobe, nyani na ndege wa aina mbalimbali.

Eneo lingine lenye ukubwa wa ekari 15 ambalo lipo katika bustani hiyo ni eneo huru kwa ajili ya wanyama walio huru na wenye uwezo wa kujitafutia chakula. Wanyama waliopo katika eneo hili ni swala, nyumbu, kuro, nyati maji na mbuni.

Katika kuimarisha uoto wa asili na utunzaji wa mazingira, tayari wamepanda zaidi ya miti 5000 ikiwemo ya asili, miti ya kisasa, nyasi za malisho ya wanyama na miti ya matunda mbalimbali.

Hata hivyo, Ndomba anasema mradi huo haujakamilika katika kiwango kinachotakiwa kwa sababu bado aina ya ndege na wanyamapori hawajaletwa katika bustani hiyo.

Baada ya kukamilika kwa mradi huo, bustani itatumika kutoa mafunzo kwa nadharia na vitendo juu ya namna ya uhifadhi wa maliasili wakiwemo wanyamapori na mazingira kwa ujumla.

Changamoto zinazoikabili bustani ya Lugari kwa mujibu wa meneja huyo ni gharama kubwa za wanyamapori ambazo serikali inatoza kwa wenye bustani za wanyama.

Anasema wanatozwa bei sawa na wanaosafirisha wanyama nje ya nchi au wawindaji wa kitalii.

Kutokana na changamoto hiyo Ndomba anatoa rai kwa Idara ya Wanyamapori nchini iangalie uwezekano wa kutofautisha bei hizo kati ya wenye bustani za wanyama na wanaosafirisha nje ya nchi.

Anataja changamoto nyingine kuwa ni gharama kubwa za kukamata wanyamapori na gharama za kusafirisha umbali mrefu kwa sababu wanyama wanafika wakiwa wamechoka na wengine kufa hivyo anashauri baadhi ya wanyama wangekamatwa maeneo jirani ili kupunguza umbali.

"Eneo letu huru ambako tumeweka wanyama wakitembea huria, kulikuwa na nyoka wengi aina ya kobra ambao walikuwa wanawadhuru baadhi ya wanyama," anasema.

Anaeleza kuwa, jitihada zilifanyika ikiwemo kumwaga mafuta machafu kwenye mashimo ya nyoka ili kudhibiti tatizo hilo. "Tumefanikiwa kuwadhibiti nyoka hao," anasema Ndomba.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Meja Generali Gaudance Milanzi ametembelea bustani hiyo ya wanyama ya Lugari na kueleza kufurahishwa na uwekezaji uliofanywa katika eneo hilo katika kukuza utalii wilayani Mbinga.

Katika ziara hiyo alipokea ombi la mwanzilishi wa bustani, Ndomba, la kuipatia simba kwa sababu wananchi wengi wanapenda kumuona mnyama huyo adimu ambao wengi wamemuona katika picha tu.

Bustani hiyo imeshaandaa eneo maalumu kwa ajili ya kumhifadhia simba.

Ndomba anaomba kupeleka wanyama katika bustani hiyo wakati wa maadhimisho ya Nanenane ngazi ya wilaya na mkoa kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi.

Licha ya bustani hiyo kutunza wanyama na ndege, pia ina eneo maalumu ambalo utalii wa kupiga picha unaweza kufanyika.

Aidha linaweza kutumika kwa sherehe mbalimbali. Kuna eneo la mapumziko na kwa ajili ya watoto kucheza.

Sekta ya utalii ni ya pili kwa ukubwa katika kuchangia pato la taifa ambayo inachangia zaidi ya asilimia 17.

Kutokana na mapato makubwa ya sekta ya hiyo, serikali imekusudia kuongeza mchango wa utalii ili kuongeza pato la taifa na kuinua uchumi.



Kibao kinachoonesha Lugari zoo Mbinga.

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili,mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com; simu 0784765917

Scanned by CamScanner

Zao la muhogo linavyoweza kupaisha uchumi wa wakulima

Na Albano Midelo

TANZANIA ina fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji wa muhogo hata kuongoza katika Afrika kutokana na kuwa na utajiri wa ardhi kubwa yenye rutuba.

Takwimu kutoka Wizara ya Kilimo zinaonesha mwaka 2005 Tanzania ilizalisha tani milioni 1.8 za muhogo mkavu, mwaka 2006 katika nchi nzima zilivurwa tani milioni mbili za muhogo mkavu.

Hivyo, ili kuingia katika biashara ya muhogo ambao una soko kubwa duniani inabidi kuzalisha zao hilo kwa wingi.

Hata hivyo, unga wa muhogo wenye ubora wa hali ya juu na unaokubalika katika soko la kimataifa ni ule ambao haujavundikwa na unaweza kutumika katika kutengeneza vitu mbalimbali kama vile ugali, biskuti, mikate, keki, maandazi, chapati na vyakula vingine.

Wataalamu wa kilimo wanasisitiza kuwa tangu kuvuna muhogo shambani kwa nja ya kisasa hadi kutengenezwa unga, inatakiwa muda uwe mfupi usizidi saa 24.

Kulingana na teknolojia ya hivi sasa, muhogo ukishavunwa husafishwa na kuingizwa katika mashine maalumu ili kukatwa katika vipande vidogo na hatua inayofuatia ni kwenda kukamua ili kupunguza maji kwa asilimia 80 na kuanika kwenye jua baada ya saa moja tu unga safi unakuwa umekauka.

Muhogo uliosindikwa ili uweze kuuzwa nje ya nchi ni lazima uwe mweupe, usiwe na mabonge, uwe na ladha nzuri, usiwe na uvundo kwa maana kwamba, unyevu upunguzwe hadi kufikia asilimia 11 na uwe umethibitishwa na Shirika la Viwango nchini(TBS).

Zao hili lina uwezo wa kuwakomboa wananchi kiuchumi kutokana na utafiti kuonesha kuwa bidhaa zaidi ya 300 zinaweza kuzalishwa kutokana na muhogo.

Mwambao mwa ziwa Nyasa mkoani Ruvuma ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa muhogo.

Hata hivyo, wameshindwa kufanya kilimo cha muhogo kuwa cha kibiashara kutokana na kukosa maelekezo ya kitaalamu na hivyo kufanya zao hilo libaki kuwa la chakula.

Nathaniel Lugongo ni kiongozi wa asasi ya Mwangaza Foundation katika Wilaya ya Nyasa ambaye anasema muhogo ndiyo zao kuu la chakula mwambao mwa ziwa Nyasa, wamedhamiria kulifanya zao hili kuwa la kibiashara.

Kwa mujibu wa Lugongo kinachohitajika hivi sasa ni kupata mashine ya kusaga mihogo mibichi kuwa unga badala ya mtindo uliozoeleka wa wakazi wa mwambao mwa ziwa Nyasa ambao wanailoweka mihogo baada ya kumenya maganda kwenye vyungu kisha kuianika juani kabla ya kuisaga kwa mashine au kutwangwa kwenye kitu.

"Soko la unga wa muhogo ndilo tatizo kubwa hivyo endapo mihogo mibichi itaanza kusagwa kwa mashine za kisasa itaweza kuwa na soko kubwa na kuinua hali ya uchumi kwa wakazi wa mwambao mwa ziwa Nyasa", anasisitiza Lugongo.

Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani ilikaririwa ikitangaza kuwa nchini Msumbiji kuna kiwanda cha kutengenezea pombe aina bia ya kisasa kutokana na muhogo.

Pombe hiyo inauzwa ndani na nje ya nchi ya Msumbiji, hali ambayo imesababisha muhogo katika nchi hiyo kuwa zao la kibiashara kwa kuwa wakulima wanapata faida kubwa kutokana na kuuza unga wa muhogo unaozalishwa kutokana na mihogo mibichi katika viwanda nchini humo.

Serikali kwa kutumia vikao vya ujirani mwema inaweza kwenda kujifunza nchini Msumbiji pamoja na wataalamu wa kilimo kwa kutembelea kiwanda cha bia zinazotokana na mihogo ili utaalamu huo utike nchini hatimaye, wakazi wa Nyasa na watanzania kwa ujumla waweze kufanya muhogo kuwa ni kilimo cha kibiashara.

Inakadiriwa ili kujenga kiwanda kidogo cha kisasa cha kusaga mihogo mibichi kwa ajili ya kupata unga, zinahitajika jumla ya Sh milioni 100 na kwamba wakulima kazi yao itakuwa ni kumenya mihogo na kupeleka kiwandani.

Utafiti unaonesha kuwa soko la unga wa mihogo mibichi inayomenywa na kutengeneza unga kiwandani ni kubwa nje ya nchi ikiwemo Afrika Kusini na nchi za Afrika Magharibi.

Ukitembelea mwambao mwa ziwa Nyasa kuna baadhi ya wakulima wamelima mihogo kati ya miaka mitatu hadi mitano iliyopita hadi sasa ipo shambani haijavunwa kutokana na kukosa soko la uhakika la unga ambao unazalishwa kwa kusindika badala ya kupelekwa moja kwa moja kiwandani.

Mkoa wa Mtwara unakadiriwa kuzalisha asilimia 28 ya muhogo nchini, lakini bado kiwango hicho kinachozalishwa hakimmulaisiki mkulima wa Mtwara kutokana na changamoto nyingi zinazozukabili mfumo mzima wa uzalishaji na usindikaji wa zao hilo.

Mikoa inayozalisha muhogo kwa wingi ni Mwanza, Mtwara, Lindi, Shinyanga, Tanga, Ruvuma, Mara, Kigoma, Pwani na karibu maeneo yote ya Zanzibar.

Kanda ya Ziwa ni wazalishaji wakubwa zaidi ikifuatiwa na ukanda wa Kusini, ambako Mkoa wa Ruvuma huzalisha asilimia 10 ya uzalishaji wote nchini.

Kwa mujibu wa Shirika la Chakula Duniani (FAO), muhogo ni zao la tatu kwa kuwa na kiwango kikubwa cha wanga katika nchi za ukanda wa joto, zikiwemo nchi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Takribani watu milioni 500 duniani hutegemea zao hilo kama chakula kikuu.

Kulingana na FAO, uzalishaji wa muhogo duniani ulikadiriwa kuwa tani milioni 184 mwaka 2002, kiwango ambacho baadaye kilitongezeka hadi kufikia tani milioni 230 mwaka 2008.

Katika Afrika, mwaka 2002 jumla ya tani milioni 99.1 zilizalishwa na Bara la Asia lilizalisha tani milioni 51.5 na tani milioni 33.2 zilizalishwa huko Latin America na Caribbean.

Takwimu za FAO zinaonesha kuwa Thailand ndiyo inayoongoza kwa kuuza nje zao la muhogo uliokaushwa. Asilimia 77 ya muhogo uliouzwa nje kwa mwaka 2005 ulitoka nchini humo.

Nchi ya Vietnam imewahi kuweka rekodi ya kuuza zao la muhogo kwa asilimia 13.6 ya mahitaji duniani, ikifuatiwa na Indonesia asilimia 5.8 na Costa Rica asilimia 2.1.

Takwimu za mwaka 2005 zinaonesha kuwa Tanzania ilizalisha muhogo kwa wastani wa tani milioni mbili kwa mwaka kwa hekta arobaio kwa wastani wa Bara la Afrika mwaka huo ulizalisha muhogo tani milioni 3.3 kwa mwaka na nchi ya Nigeria ilizalisha tani milioni 4.7 kwa mwaka.

Nchini Nigeria, serikali imetunga sheria kwa kila anayetengeneza mikate, biskuti na bidhaa nyingine achanganye na unga wa muhogo kama nja ya kulinda soko la unga wa muhogo na kuwapa wakulima hamasa ya kuendelea kulima zao hilo katika nchi hiyo.

Nchi za Afrika ambazo zina viwanda vikubwa vya kusindika zao hili ni Afrika Kusini, Nigeria na Ghana.

Hapa nchini, zao hili linaweza kutumika kutengenezea pombe, kwenye viwanda vya bia na dawa nyingine viwandani.

Kasam Maswaga ambaye ni mtaalamu wa kilimo anasema elimu ya kusindika muhogo ikienea katika maeneo mengi nchini miaka 10 ijayo zao la muhogo litakuwa ni kubwa na lenye heshima katika kuinua kipato cha mkulima kwa kulifanya kuwa la chakula na biashara.

"Sisi wataalamu wa kilimo na serikali kwa ujumla tumelenga kuhakikisha zao la muhogo kupitia usindikaji linatumika kama zao la chakula na biashara kwa sababu hivi sasa tunaendelea kutoa mafunzo ya namna ya kulisindika na kulitumia," anasema Maswaga.

Utafiti umebaini kuwa zao hili ni chakula kikuu kwa kuwa karibu watu bilioni moja katika nchi zaidi ya 105 duniani wanatumia. Muhogo huchangia theluthi moja ya mahitaji ya virutubisho vya kuongeza nguvu mwilini.

Zao la Muhogo kwa mara ya kwanza lililetwa na Wareno katika Afrika.

Zao hili hulimwa nchi zaidi ya 34 za Afrika kwenye eneo lenye ukubwa wa zaidi ya ekari milioni 200.

Tanzania inatajwa kuwa nchi ya nne kati ya wazalishaji wakubwa wa muhogo barani.

Karibu hekta 670,000 za ardhi ya kilimo zinatumika kuzalisha muhogo. Zao hili linachangia karibu asilimia 15 ya chakula kwa nchi nzima. Inakadiriwa kuwa takribani kaya 1,213,958 huzalisha muhogo nchini .

Hapa nchini muhogo unatajwa kuwa zao la pili kwa kuchangia pato la taifa kwa asilimia 19 baada ya mahindi. Wanga wa muhogo hutumika kutengeneza dawa za madoa, gundi katika semani, rangi za awali katika kuta za nyumba na sukari.

Muhogo una kiasi kikubwa cha vitamini A na kiasi kidogo cha protini. Ulaji wa mihogo husaidia walaji kuepukana na ugonjwa wa ukavu macho. Pia majani ya mihogo huweza kutumika kama mboga za majani yaani kisamvu.

Mpaka sasa wataalamu wanataja aina mbili za mbegu bora za muhogo ambazo zimethibitishwa baada ya kufanyiwa utafiti na kubaini kuwa mbegu hizo huvumilia magonjwa na kuzaa sana ukilinganisha na mbegu za kienyeji.

Mbegu hizo ni aina ya Naliendele na mbegu aina ya Kiroba ambazo huzaa kati ya tani 25 hadi 30 za muhogo kwa hekta moja, pia zinaweza kuvunwa kuanzia miezi 9 toka kupandwa.

Albano Midelo ni mchangiaji wa gazeti hili, anapatikana barua pepe albano.midelo@gmail.com, simu 0784765917

Wakazi wa Kijiji cha Nkali Wilaya ya Nyasa wakitayarisha unga wa mhogo.



Mihogo ambayo imevundikwa na kuandaliwa kienyeji kwa ajili ya kutengeneza unga.

Zao la muhogo katika Kijiji cha Nkali Wilaya ya Nyasa Mkoa wa Ruvuma.

Scanned by CamScanner

MAKALA

'Ngoro' inavyowezesha kilimo milimani bila mmomonyoko

Na Albano Midelo

NGORO ni aina ya kilimo kinachohifadhi mazingira kwa njia ya asili ambacho kinaaminika kilianza kutumika na wakulima wa kabila la Wamatengo Wilaya ya Mbinga Mkoa wa Ruvuma zaidi ya miaka 300 iliyopita.

Kilimo cha ngoro kilianzishwa na wazee maarufu wa kabila la Wamatengo waliotokea nchini Malawi katika karne ya 17. Vizazi zaidi ya 10 vimepita hivi sasa tangu kilimo cha ngoro kilipoanzishwa katika wilaya ya Mbinga.

Ngwatura Ndunguru ni Mbunge mstaafu wa Mbinga ambaye anataja moja ya madhumuni ya kuanzisha kilimo hiki ni kuudhibiti udongo wa juu wa ardhi ambao kwa kawaida huondolewa na maji au upepo kutokana na mmomonyoko wa ardhi.

Kitendo hiki huondoa udongo wenye rutuba nyingi ya kuifanya mimea iweze kustawi vizuri.

"Tunajua kuwa udongo ulio chini ya tabaka la juu hauna rutuba ya kutosha ya kuwezesha mazao kustawi vizuri, kutoweka kwa udongo wa juu kutoka shambani au bustani kwa njia ya mmomonyoko ni hasara kubwa, kwa vile kunasababisha upungufu wa mavuno," anasema.

Njia za kuhifadhi ardhi zinaweza kutumiwa kwa kutegemea hali ya hewa, mazingira ya eneo kama ni maeneo ya mwinuko au tambarare.

Hata hivyo, zinaweza kutumika njia mbili au tatu katika shamba moja. Ziko njia kuu mbili za kuhifadhi ardhi; Nazo ni njia za asili au za kienyeji na njia ya kisasa ambazo zimefanyiwa utafiti wa kina na wataalamu.

Taarifa za kihistoria zinaeleza kuwa Wamatengo walilazimika kutumia kilimo cha ngoro ili kuhifadhi udongo mzuri uliopo katika miteremko hiyo.

Katika mashimo ya ngoro hupandwa mazao kama vile maharage, mahindi na ngano kwenye kingo za mashimo hayo. Mkulima hufyeka shamba lake na kuzipanga nyasi zilizokatwa kwenye mashimo ya ngoro.

Mkulima akipindua udongo wa chini kuwa juu hukata nyasi na kwamba udongo wenye rutuba hugeuka kuwa mboji na rutuba huongezeka.

Maji ya mvua yakisimama katika mashimo ya ngoro hulinda unyevu wa ardhi na kukinga mmomonyoko wa ardhi.

Inaaminika kuwa kilimo cha ngoro kinahusishwa na shughuli za kuwepo kwa mapango ya kuishi. Historia ya Wilaya ya Mbinga inaonesha kuwa, zamani wananchi wa Wilaya ya Mbinga walikuwa na tabia ya kufanya kilimo cha kuhama hama.

Wakulima wakati huo walilima sehemu moja na wanapogundua sehemu hiyo rutuba imemalizika, walikuwa wakihamia sehemu nyingine yenye rutuba na kuendesha kilimo bila kujali athari za kimazingira ambazo zilikuwa zinajitokeza kutokana na aina hiyo ya kilimo.

Kutokana na kuwepo kwa mapango, wazee hao wa kabila la Wamatengo waliamua kuanzisha kilimo cha kufukia majani ili kupata mbolea ya asili hivyo kuendesha kilimo walichokiita ngoro katika sehemu moja bila kuhama huku wakirutubisha ardhi na kuzuia mmomonyoko wa udongo kutokana na ardhi ya Mbinga na milima yenye miteremko mikali.

Mbunge mstaafu wa Mbinga, Ngwatura Ndunguru akielezea kilimo cha ngoro.

Mbunge mstaafu wa Mbinga, Ngwatura Ndunguru anasisitiza kuwa Wamatengo tangu wameanza kutumia kilimo cha ngoro miaka 300 iliyopita hadi sasa wamekuwa wanazalisha vyakula kwa wingi na kuhifadhi mazingira kwa njia ya asili kwa kuzuia mmomonyoko wa udongo kutokea kwenye miteremko ya milima ya umatengo wilayani humo.

Anabainisha zaidi kuwa katika kilimo cha ngoro mvua zinaponyesha maji huingia kwenye mmea na majani yaliyowekwa chini yanaoza.

Katika msimu mwingine, majani yaliyoota kwenye shimo yatafyekwa, yaliyosalia yatavunwa na kutandazwa kwenye shimo na kufukuliwa majani ya mwaka jana ambayo tayari yanakuwa mboji.

John Mbunda (80) mkazi wa kijiji cha Kilanga Juu wilayani Mbinga anasema Wamatengo walianzisha mfumo maalumu wa kilimo cha ngoro uliowasaidia uliojulikana kwa kabila la Wamatengo kwa jina la Ingoro.

Anasema mfumo huo uliwawezesha kuendelea kulima kwenye maporomoko ya milima bila ya kusababisha mmomonyoko wa udongo au kuathiri vibaya rutuba kwenye mashamba yao.

Alex Ndunguru mkazi wa Kijiji cha Ilela anasema wenyeji wa Mbinga walilazimika kubuni kilimo cha ngoro ili kuhifadhi udongo mzuri ulio katika miteremko ya Umatengo na kwamba ngoro ndiyo mkombozi katika kilimo kwa kuwa kilimo kimekuwa endelevu badala ya mfumo wa zamani wa kuhamahama.

Utafiti umeonesha wazi kwamba teknolojia ya ngoro ni bora zaidi katika kilimo. Wakulima kutoka maeneo mbalimbali nchini wamekuwa wakifika katika Wilaya ya Mbinga kujionea wenyewe na kujifunza teknolojia hiyo inayohifadhi ardhi na kutunza mazingira kwa muda mrefu.

Moja ya faida ya kilimo cha ngoro ni kwamba hata kama mvua hazitanyesha, bado shamba litaendelea kuwa na unyevunyevu kutokana na maji yaliyomo ndani ya mashimo hayo.

Isitoshe wakati wa mavuno, mabaki ya nafaka yanayotupwa kwenye mashimo hayo, huwezesha shamba kustawi vizuri zaidi kutokana na mbolea iliyowekwa.

Kwa mujibu wa Ndunguru, wameanza kukitangaza kilimo hicho na kukiingiza kuwa ni miongoni mwa vivutio vya utalii ambavyo vinapatikana katika wilaya ya Mbinga pekee.

Baadhi ya wageni ambao wamekuwa wakitembea kwenye magari kupitia barabara ya Mbinga hadi Mbambabay Wilaya ya Nyasa pamoja na maeneo mengine ya milima ya umatengo wamekuwa wakisimama mara kwa mara kwenye milima hiyo na kuchukua picha za kawaida na video.

Ndunguru anasisitiza kuwa kilimo cha ngoro kimeonekana kuvutia watu wengi wa ndani na nje ya nchi hasa mimea inayochomoza na kuonekana mfano wa mapambo yaliyopambwa juu ya milima ya Umatengo.

Wizara ya Kilimo imeanzisha Mradi wa Kutunza Mifumo muhimu ya asili ya kilimo duniani (Global Importance Agricutural Heritage System-GIAHS) ili kuendeleza kilimo cha asili na kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji.

Taarifa kutoka Idara ya Matumizi Bora ya Ardhi Katika Wizara hiyo inaeleza kuwa mradi huo unatekelezwa na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) ambao unalenga kutambua mifumo ya asili na endelevu ya kilimo na ufugaji ili kumsaidia mkulima.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, katika Afrika Mashariki Tanzania na Kenya zilichaguliwa kufufua mifumo hiyo kwa kuwa na sehemu muhimu za kilimo.

Baada ya kuchaguliwa, Tanzania ilipendekeza mifumo mitatu ya kilimo asili ukiwemo mfumo wa ngoro ambao unatumiwa na kabila la wamatengo.

Mifumo ya asili ya kilimo ilianza kupendekezwa duniani tangu mwaka 2002. Baadhi ya nchi ambazo zimeanza kutumia mifumo hii ya asili katika kilimo ni Japan, Ufilipino, China na Ujerumani.

Albano Midelo ni mchangiaji wa gazeti hili anapatikana kwa barua pepe albano.midelo@gmail.com Simu 0754765917

Scanned by CamScanner

Nyotamkia ya kwanza kuonekana kwa macho

Mwandishi wa makala haya akiwa katika nyotamkia iliyoanguka katika kijiji cha Ndolezi wilayani Mbozi mwaka 1840.

Na Albano Midelo

NYOTAMKIA (meteorite) ya kwanza katika historia ya Tanzania kuonekana kwa macho ilianguka katika Kijiji cha Litowa, Peramiho wilayani Songea mkoani Ruvuma Oktoba 24 mwaka 1899.

Wananchi wa kijiji hicho waliiona kwa macho wakati nyotamkia huyo yenye uzito wa gramu 165 inaanguka kutoka angani baada ya kumeguka kwenye obiti yake.

Abate Mstaafu wa Abasia ya Peramiho Songea, Mhashamu Lambert Doerr (80) anasema nyotamkia hiyo ilionekana wakati inashuka angani. Hata hivyo ilikuwa ndogo sana ambapo wamisionari wa kijerumani wakati huo waliwafahamisha wenyeji kwamba hiyo ni nyotamkia (kimondo).

Joakim Soko (82) mzaliwa wa Kijiji cha Litowa, Mwalimu mstaafu na Mwenyekiti mstaafu wa kijiji hicho anasema wazazi wake waliiona kwa macho nyotamkia hiyo wakati inaanguka toka angani.

Hata hivyo, anabainisha kuwa wazee karibu wote walioshuhudia tukio hilo wamefariki na kwamba kutokana na tukio hilo, wageni toka nchi mbalimbali walikuwa wanafika katika kijiji hicho ambapo mwaka 1965 Baba wa Taifa Julius Nyerere aliweka jiwe la msingi kwa ajili ya kumbukumbu ya eneo hilo na kuanzishwa kwa kijiji cha ujamaa cha Litowa.

"Niliwasikia wazazi wangu na wazee wengine ambao sasa wamefariki wakisema kuwa nyotamkia ilianguka hapa kijijini na kutoa mwanga wa ajabu wakati inashuka kwa sababu waliiona kwa macho. Hata hivyo, kipindi hicho hakuna aliyefuatilia zaidi ya wamisionari waliokuwepo hapa kijijini," anasema Soko.

Anasema tangu zamani hadi sasa kuna raia wa kigeni ambao wamekuwa wanafika katika kijiji hicho ambao wanatembelea katika jiwe la msingi,miti wa msufi na mlima Litowa na kwamba raia tosa nchi za Marekani, Ujerumani, Ungereza na idadi kubwa ya Wanahindi wanafika [illegible] katika kijiji hicho.

Josephati Ndenji ambaye nyumba yake ipo eneo ambalo linaaminika kuanguka nyotamkia hiyo, anasema raia wa kigeni wamekuwa wanafika hapo, wamemuomba kutunza eneo hilo huku wakiahidi watarudi kwa ajili ya kujenga mnara wa kumbukumbu.

"Mara nyingi natembelewa na wazungu, kila baada ya miaka mitatu wanafika hapa wanapiga picha jiwe la msingi lililowekwa na Nyerere mwaka 1965, mwaka jana walipofika hapa walisema wanataka kujenga mnara wa Makumbusho," anasema Ndenji.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Litowa, Michael Komba anasema kuna taarifa kuwa nyotamkia ilianguka katika kijiji hicho na kwamba eneo ambalo ilianguka liliwekwa jiwe la msingi na Hayati Julius Nyerere mwaka 1965. Pia anakiri kwamba raia wa kigeni wamekuwa wanafika hapo na kupiga picha na kuondoka.

"Nyotamkia hiyo ilianguka miaka 113 iliyopita, pia inadaiwa ilikuwa ndogo sana. Hatujui kama kwenye mnara ndiyo imefukiwa chini, mwaka jana kuna raia wa kigeni walifika wanasema wanataka kujenga mnara wa Makumbusho katika eneo hili," anasema Komba.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo kijiji cha Litowa kilichopo katika Kata ya Parangu wilayani Songea mkoani Ruvuma, kijiji hicho kilianzishwa mwaka 1960 na kina wakazi zaidi ya 2,500.

Mhifadhi Kiongozi wa Makumbusho ya Taifa, Philipo Maligissu anasema hadi sasa zimeanguka nyotamkia nane katika sehemu mbalimbali nchini ambapo nyotamkia ya Litowa Peramiho ndiyo ya kwanza kuonekana kwa macho wakati inaanguka mwaka 1899.

Anazitaja nyotamkia nyingine kuwa ni Lichinga mkoani Mtwara ambayo uzito wake hauzidi kilo moja na ilionekana kwa macho wakati inaanguka mwaka 1949 na nyotamkia ya Mbulu mkoani Manyara ambayo haikuonekana wakati inaanguka toka angani.

"Kutinganza na mtatamu huyo nyotamkia nyingine ndogo ilianguka katika kijiji cha Ivuna Mbozi Mbeya ambayo ilionekana kwa macho wakati inachomoka kutoka angani mwaka 1938.

Nyotamkia nyingine ilianguka katika eneo la Malampaka mkoa wa Shinyanga ambayo ilionekana kwa macho wakati inashuka kutoka kwenye obiti yake mwaka 1930.

Nyotamkia ya Mbozi ilianguka mwaka 1840, ikiwa na uzito wa tani 12 ni ya nane kwa ukubwa duniani kati ya nyotamkia zaidi ya 600 zilizoanguka kutoka angani sehemu mbalimbali duniani.

Utafiti unaonesha kuwa nyotamkia hiyo inaongoza kwa ubora ukilinganisha na nyotamkia zilizoanguka sehemu mbalimbali duniani.

Nyotamkia ya Mbozi katika historia ya nyotamkia zilizoanguka duniani haikubahatika kushuhudiwa na mtu yeyote wakati inashuka kutoka kwenye obiti yake angani kuja duniani.

Hata hivyo, kinachowavutia wengi ni kwamba nyotamkia hii ilikuja kuonekana tayari ikiwa imeanguka chini wakati wa utawala wa Mjerumani mwaka 1930 ambapo wataalamu wa Kijerumani mwaka 1931 walikata kipande cha nyotamkia huyo na kukipeleka nchini Ujerumani ili kukitanya utafiti.

Mhifadhi Kiongozi wa Makumbusho ya Taifa, Philipo Maligisu anasema nyotamkia huyo bado ya kupimwa ilionaishia idadi ya mita tatu, unene wa mita 1.12, upana mita moja, ina uzito wa tani 12, nyotamkia hiyo ina aina tano za madini.

Anayataja madini yaliyomo katika nyotamkia hiyo kuwa ni chuma kipo kwa asilimia 90.45, madini ya nikel asilimia 8.66, shaba asilimia 0.69, sulfa asilimia 0.11 na madini ya fosiforasi ni asilimia 0.11.

Utafiti umebaini nyotamkia ya Mbozi ndiyo pekee yenye madini ya aina tano wakati nyotamkia nyingine ikiwemo iliyoanguka nchini Afrika Kusini yenye uzito wa tani 60 na ya nchini Uingereza yenye tani 30 hazina madini.

Kulingana na utafiti, nyotamkia zilizoanguka katika nchi nyingine hazina ubora wowote wala madini, zaidi ya kuwa ni mfano wa jiwe linalopasuka kirahisi hali ambayo inasababisha watalii kutembelea zaidi nyotamkia ya Mbozi.

"Nyotamkia zilizoanguka katika maeneo mbalimbali nchini ni vitega uchumi adimu vya utalii kwa kuwa watalii wengi wanasafiri na kuja hapa nchini ili kuona maajabu ya vitu ambavyo vimemeguka kutoka sayari nyingine katika anga za mbali na kushuka kama nyota hadi katika dunia tunayoishi," anasema Maligisu.

Hata hivyo, mtaalamu huyo wa mambo ya kale anasema lami inatakiwa kufahamu kuwa nyotamkia ni hazina ya kipekee inayotakiwa kulindwa na kuendelezwa ili kupata fedha za kigeni na kuongeza mapato.

Maligisu anasisitiza kuwa eneo ambalo nyotamkia imeangukia likiendelezwa linaweza kuwa chanzo cha kupunguza umaskini wa kipato kwa kuwa watalii wanapotembelea wanalipa kiingilio, watalipia chakula, usafiri na vifaa mbalimbali vya kutamaduni kama vinyago ambavyo wanaweza kuviuza kwa watalii hao.

Mhifadhi Msaidizi wa Idara ya Mambo ya Kale, Filmerick Bassange anasema serikali imeiingiza nyotamkia ya Mbozi kwenye sheria ya mambo ya kale mara baada ya uhuru mwaka 1964, hivyo kuitambua na kutoa ulinzi.

Basange anabainisha zaidi kuwa mwaka 1967 serikali iliamua kuchimba eneo ambalo nyotamkia ya Mbozi ilianguka na kujengea msingi ambapo kabla ya hapo nyota hiyo ilikuwa inaonekana sehemu ndogo ya juu.

Idara ya Mambo ya Kale kwa kushirikiana na Idara ya Makumbusho ya Taifa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii zina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa malikale zilizopo nchini zinahifadhiwa, kulindwa na kuendelezwa, kwa kuwa ni urithi wa Taifa katika kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

> "Miaka 113 iliyopita, pia inadaiwa ilikuwa ndogo sana. Hatujui kama kwenye mnara ndiyo imefukiwa chini, mwaka jana kuna raia wa kigeni walifika wanasema wanataka kujenga mnara wa Makumbusho katika eneo hili"

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili. Mwasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com, simu [illegible] 4765917

Scanned by CamScanner

Ugonjwa wa malaria bado ni pasua kichwa

Na Albano Midelo

Jumla ya watu 133 katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea Mkoa wa Ruvuma walifariki dunia mwaka 2015 baada ya kuugua ugonjwa wa malaria.

Takwimu za Idara ya Afya katika Manispaa ya Songea za Mwaka 2015 zinaonesha kuwa Manispaa hiyo ilikuwa na wagonjwa wa malaria 28,624 ambao ni sawa na asilimia 16.9 ya wagonjwa wote 169,266.

Takwimu zinaonesha kuwa watoto chini ya miaka mitano waliokufa kutokana na malaria katika Manispaa hiyo mwaka 2015 ni 57 sawa na asilimia kumi ya vifo vyote vilivyotokea kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano wapatao 572.

Takwimu zinaonesha kuwa idadi ya wagonjwa wa malaria wa nje katika Manispaa ya Songea imepungua toka 63,618 mwaka 2014 hadi wagonjwa 28,624 mwaka 2015 na kwamba Idadi ya vifo vilivyotokana na na malaria pia vimepungua toka 189 mwaka 2014 hadi vifo 133 mwaka 2015.

Ugonjwa wa malaria sio tu unawasumbua wakazi wa Manispaa ya Songea, takwimu zinaonesha kuwa malaria ndiyo ugonjwa unaongoza kwa kusababisha vifo kuliko magonjwa mengine yote hapa nchini.

Serikali imekuwa inatumia gharama kubwa za kuagiza madawa, vyandarua na gharama nyingine kujaribu kupambana na ugonjwa huu bila mafanikio ya kuutokomeza.

Watalaamu wa afya wanasema kuna njia tatu za kupambana na hata kuutokomeza ugonjwa wa malaria ni kupata tiba sahihi ambayo ni dawa yenye nguvu ya kuua wadudu wanaosababisha ugonjwa wa malaria.

Kuhakikisha watu wasiumwe na mbu wa malaria msisitizo mkubwa ukiwa ni matumizi ya vyandarua vilivyotiwa dawa ya kuua mbu hali ambayo itamwezesha mtu asipate malaria.

Akinamama wote wajawazito na watoto wanatakiwa kulala katika vyandarua vyenye dawa kwa kuwa malaria ni chanzo kikuu cha vifo vya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano hapa nchini. Vile vile kuhakikisha kuwa mbu wanaoambukiza malaria hawaendelei kuzaliana kwa kuwaua kwenye mazalia yao yote na sehemu zote ambazo wanatua ili kuwatokomeza kabisa mbu wanaoeneza malaria.

Utafiti unaonesha kuwa njia ya tatu ndiyo pekee ambayo inaweza kumaliza kabisa ugonjwa wa malaria kutokana na tafiti kuonesha nchi ambazo zimetumia njia hii na kufanikiwa kumaliza ugonjwa wa malaria kwa asilimia 100.

Teresia Nyirenda ni mtanzania ambaye anaishi nchini Marekani anasema mazingira ya Tanzania yamekuwa ni mazalio ya mbu hivyo kuchangia kueneza ugonjwa wa malaria ambao unamaliza maelfu ya watu kila mwaka.

Anasema hata kama vyandarua vitatumika kukabiliana na mbu, ugonjwa wa malaria hauwezi kumalizika kwa kuwa mazingira ni rafiki kwa mazalio ya mbu, ametolea mfano baadhi ya maeneo watu wamechimba mabwawa ya kufugia samaki ambayo hayana samaki badala yale yamekuwa mazalia ya mbu.

Hata hivyo anaitaja njia ya gharama nafuu ya kupambana na mazalia ya mbu ambayo inatumika nchini Marekani na nchi za Ulaya na kusababisha mbu kutoweka na hivi sasa malaria imebakia kuwa historia.

"Kuna aina ya maua na miti ambayo inatoa harufu inayofukuza mbu wa malaria, sio kwamba Marekani hakuna mbu, lakini mbu waliobakia wanauma na hawana uwezo wa kukuambukiza ugonjwa wa malaria",anasema.

Aliitaja baadhi ya mimea kuwa ni mmea unaojulikana kama nyonyo (cast oil) ukipandwa karibu na makazi una uwezo wa kufukuza mbu (repellent) na mbegu zake zikipondwa na kuchanganywa na maji na kisha kumwagwa huweza kufukuza wadudu kama mbu.

Omari Said na Godfrey Mwagu watunzaji wa maua bustani ya Abasia ya Peramiho Jimbo Kuu la Songea, wamethibitisha kuwepo kwa maua na mimea inayofukuza mbu wa malaria.

Hata hivyo wanasema watu wengi hawana elimu dhidi ya maua hayo, hivyo wanatakiwa waelimishwe kupanda maua hayo katika kila nyumba ili kumaliza tatizo la mbu wa malaria.

"Hapa hakuna mbu wa malaria, wazungu waliopo hapa hatujawahi kusikia wanaugua malaria, lakini sisi waafrika katika nyumba zetu hatujapanda maua kama haya tunasumbuliwa na ugonjwa wa malaria kila siku, nadhani wananchi wangehamasishwa kila nyumba inaweza kupata maua haya",anasisitiza Omary Said.

Ugonjwa malaria bado ni pasua kichwa kwa kuwa takwimu zinaonesha ndiyo ugonjwa unaoongoza kwa kusababisha idadi kubwa ya vifo ambapo watanzania 60,000 wanakufa kutokana na ugonjwa huo kila mwaka. Kwa mujibu wa takwimu hizo kila siku watu 291 wanapoteza maisha kutokana na ugonjwa wa malaria wengi wao ni watoto chini ya miaka mitano, kwa maneno mengine katika kila saa moja wanakufa watu 10 kwa ugonjwa wa malaria.

Kutokana na hali hiyo ugonjwa wa malaria umekuwa ni mzigo mkubwa kwa taifa kutokana na kurudisha nyuma mandeleo ya uchumi hasa baada ya nguvu kazi kubwa ya taifa mara kwa mara kudhoofika baada ya kuugua malaria.

Serikali imejitahidi kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Mapambano Dhidi ya Ugonjwa wa Malaria wa Miaka Mitano kuanzia mwaka 2008 hadi 2013 ambao ulilenga kupunguza vifo kwa asilimia 80.

Takwimu zinaonesha kuwa malaria bado ni tatizo kubwa nchini katika maeneo ya vijijini ikilinganishwa na maeneo ya mjini ambapo maambukizi maeneo ya vijijini ni asilimia 10.7 na mjini ni asilimia 3.4

Tofauti hiyo inaonesha kuwa maambukizi ya malaria yamepungua kwa asilimia 50 kutoka asilimia 18 mwaka 2007/2008 hadi asilimia 10 mwaka 2011/2012.

Tanzania imeweza kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa malaria kutoka asilimia 18 hadi 9.5 kwa Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar imefanikiwa kupunguza idadi ya wagonjwa hadi kufikia asilimia 0.6 .

Katika kuonesha Serikali ipo mstari wa mbele katika kupambana na adui malaria, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto Ummy Mwalimu alisema kuwa Tanzania inafanya kila juhudi kuhakikisha maambukizi ya malaria yanapungua hadi asilimia moja ifikapo mwaka 2020.

Itaendelea toleo lijalo

Scanned by CamScanner

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Dk Binilith Mahenge (wa pili kulia) akizindua tamasha la fursa za utalii Ziwa Nyasa.

Utalii wa kuona ndege kivutio cha utalii ziwa Nyasa

Na Albano Midelo

BATA aina ya tandawala machaka (Denihams bustard) wenye uwezo wa kuruka kutoka bara moja hadi jingine inaaminika wanapumzika kwa mwezi mmoja katika bwawa lililopo Kihagara mwambao mwa ziwa Nyasa, mkoa wa Ruvuma.

Mhifadhi kutoka hifadhi ya taifa ya Kitulo, Godfrey Kyando anasema katika tamasha la fursa za utalii mwambao mwa ziwa Nyasa, imebainika wakazi wa kijiji hicho kila Septemba, huwaona bata hao ambao huwapo wa muda kisha huondoka.

Wakazi wa kijiji cha Kihagara walioneshai eneo ambalo bata hao wanapumzika kabla ya kuendelea na safari.

Kyando anasema ndege hao hufika kwa ajili ya kutaga na kuangua vifaranga katika hifadhi ya taifa ya Kitulo iliyopo wilayani Makete, mkoa wa Njombe kuanzia Machi hadi Julai kila mwaka, kisha huruka kwenda katika maeneo mengine duniani.

Wakazi wa Kihagara wanapaja eneo ambalo bata hao hupumzika ni oevu lenye ukubwa wa karibu meta 500. Eneo hilo hujaa maji na kuwa kivutio cha wanyama na ndege mbalimbali.

Ndege ambao huvutiwa na eneo hilo ni bata wa aina yake, ndege aina ya yangeyange na chura wenye sauti tofauti na chura waliozoeleka.

Felician Komba ni mkazi wa kijiji cha Kihagara anayeelezea eneo hilo akisema linafanana na ziwa dogo au bwawa. Lipo umbali wa kilometa moja na nusu kutoka kijiji cha Kihagara.

Anasema miaka iliyopita, eneo hilo lilikuwa na maji muda wote hali ambayo ilisababisha idadi kubwa ya samaki wa aina mbalimbali kuzaliana kwa wingi na kulisha karibu kata yote ya Kihagara yenye vijiji vitano; Kihagara, Mango, Tumbi, Njambe, Ngehe.

Komba anasema uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji umesababisha bwawa hilo kuanza kukauka na kujaa maji kwa msimu.

"Mwezi wa tatu (Machi) hadi wa tano (Mei) kila mwaka, bwawa hilo hujaa maji ambayo hutoka kwenye mto Mbuchi, maji yanapopungua watu hufika katika bwawa hilo kukamata samaki," anasema.

Miongoni mwa viumbe wanaopatikana kwenye bwawa hilo wanatajwa mamba, ndege aina ya yangeyange, bata maji na bata wenye umbo la wastani wenye milio ya kuvutia.

"Katika hali ya kustaajabisha bwawa hili likijaa, lina aina fulani ya vyura, warefu, wana ngozi laini, weusi kidogo wana sauti nzuri ambazo huwezi kuamini kama ni za vyura, nyimbo hizo zinasikika umbali hata wa kilometa tano," anasema Komba.

Komba anasema vyura hao huimba kwa pamoja katika sauti ya kwanza na ya pili, ukiwasogolea wanaendelea kuimba lakini akipita mnyama ambao wanadhani kuwa ni adui, wote kwa pamoja wananyamaza.

"Sauti za vyura hao huendelea kusikika hadi Aprili kila mwaka wakati ambao maji yanakuwa yameanza kukauka.

Husubiri kipindi kingine ambacho maji yanaanza kujaa kwenye bwawa hilo. Katika kipindi ambacho huzaliana, hawaendelei kutoa sauti hizo.

Septemba ndipo bata wanaoaminika kutoka Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, hufika katika eneo hilo na kuwala vyura.

Adui mwingine mkubwa wa vyura ni ndege aina ya yangeyange ambao huwala huwadonoa wanapowaona katika bwawa hilo.

Komba anasisitiza umuhimu wa kuhifadhi bwawa hilo viumbe hai wapatikane wakati wote na wawe kivutio kikubwa cha watalii.

Anasema bata wanaopatikana katika bwawa hilo, nyama yake ni laini yenye ladha.

Mbunge wa Nyasa, Stella Manyanya anasema ongezeka mkakati kuhakikisha bwawa hilo ambalo ni kivutio cha utalii, halikauki badala yake linakuwa na maji wakati wote kama ilivyokuwa zamani.

Manyanya ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, anasema anaishukuru na Halmashauri ya Nyasa, Idara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha eneo hilo linafunguka.

Ulitaka wale wanaharibu kwa kuhifadhi vyanzo vyote vya maji na kupanda miti katika eneo hilo oevu ambalo linaweza kufungua milango ya utalii kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa.

Kijiji cha Kihagara kimekusudia kujenga vibanda vya asili katika eneo la bwawa hilo kuwawezesha watalii kukaa wafikapo kushuhudia vivutio vilivyopo. Hatua hiyo itawezesha kuongeza pato kwa kijiji.

Mhifadhi kutoka Hifadhi ya Taifa Kitulo, Godfrey Kyando, anasema hifadhi hiyo na eneo pekee duniani ambalo bata aina ya tandawala machaka wanazaliana.

Hifadhi ya taifa Kitulo inayopita katika mikoa ya Mbeya na Njombe ilitangazwa rasmi mwaka 2005 kuwa hifadhi ya taifa ikitumaisha sehemu ya eneo la shamba la mifugo,mstu wa Livingstone na bonde la Numbi.

Hifadhi hiyo na ukubwa wa kilometa za mraba 442 ndani ya mwinuko wa kati ya meta 2100 hadi 3000. Awali iliipiikana kama Elton Plateau baada ya Mvumbuzi Frederick Elton kupita eneo hili mnamo mwaka 1870.

Mwaka 1960 Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) liliichukua eneo hilo kwa ajili ya kilimo cha ngano na ufugaji wa kondoo.

Kyando anasema, kutokana na umuhimu wa eneo hili, wadau wa mazingira walipendekeza eneo litangazwe kuwa hifadhi ya taifa kulinda umaridadi wa maua, ndege na mimea adimu inayopatikana ndani ya eneo hili.

Utafiti unaonesha kuna bata aina ya tandawili, machaka ambao waliwekwa alama walipokuwa katika hifadhi ya taifa ya Kitulo, walionekana na alama zao katika hifadhi moja barani Australia.

Kyando anasema utafiti huu ndiyo uliothibitisha kuwa aina hiyo ya ndege husafiri umbali mrefu kwa kuruka kutoka bara moja kwenda bara jingine.

Utafiti umebaini hifadhi ya Kitula ina ndege aina ya abdims stock, denhams (tandawili machaka) na blue swallow ambao wametoka Afrika ya Kaskazini, Afrika ya Kusini, Australia na Ulaya ambao hifadhi ya Kitulo hutumika kama makazi yao katika misimu tofauti.

Mhifadhi huyo anasema watalii wakiwa ndani ya hifadhi, wanaweza kuangalia ndege hao katika ziwa Zambwe.

Pia wanaweza kuweka kambi kwa ajili ya malengo mbalimbali, utalii wa kutembea kwa miguu, kupanda farasi, michezo ya gofu na kukwea milima.

Sekta ya utalii hapa nchini ni ya pili katika kuchangia pato la taifa. Inachangia asilimia 17 ya pato.

Utalii ni muhimu siyo tu hapa nchini bali duniani. Takwimu za kimataifa zinaonesha mwaka 2010, mapato yatokanayo na utalii duniani yalifikia dola za Marekani milioni 919

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili, mawasiliano baruapepe albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917

Eneo la Kihagara mwambao mwa Ziwa Nyasa ambako bata wanaoaminika wanatoka Kitulo, wanafika mwezi Septemba kila mwaka.

Scanned by CamScanner

Mkoa wa Ruvuma unakabiliwa na upungufu mkubwa wa wauguzi...

Na Mwandishi wetu

Mkoa wa Ruvuma kama ilivyo katika mikoa mingine nchini, unakabiliwa na upungufu mkubwa wa wauguzi ikilinganishwa na idadi ya watu wanaotakiwa kuwahudumia.

Muuguzi Mkuu wa mkoa wa Ruvuma Hilda Ndambalilo alisema upungufu wa wauguzi umeathiriwa zaidi kutokana na nafasi za kazi zilizoachwa na watumishi waliondolewa kazini kutokana na kukosa sifa.

Mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) yanaonesha uwiano wa chini kabisa ili kuweza kutoa huduma salama ya uuguzi ni muhimu kuwe na muuguzi mmoja kwa kila idadi ya watu 500.

Hata hivyo kwa mujibu wa Muuguzi Mkuu huyo, uwiano wa sasa katika mkoa wa Ruvuma ni Muuguzi mmoja anahudumia watu 1500 katika jamii jambo ambalo ni hatari.

Takwimu za Juni 2017, zinaonesha kuwa Mkoa wa Ruvuma una jumla ya wauguzi 1058 sawa na asilimia 35 na kwamba ili huduma ya uuguzi iweze kutolewa kwa ufanisi, mkoa wa Ruvuma unahitaji wauguzi 3,026 ambapo hivi sasa mkoa una upungufu wa wauguzi 1968 sawa na asilimia 65.

"Hali hairidhishi katika vituo vya kutolea huduma, baadhi ya vituo vinaendeshwa na wahudumu na baadhi ya hospitali zamu za hospitali zinafanyika kwa saa 12 badala ya saa nane kwa mujibu wa sheria, jambo hili ni hatari kwa kuwa anayehumia zaidi ni mwananchi wa kawaida na muuguzi mwenyewe", alisema Katibu Mwenezi wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa Ruvuma (TANNA) Oraph Pili.

Pili alisisitiza kuwa kufanya kazi bila kupumzika kunaongeza uwezekano wa kutokea makosa ya kiutendaji yanayoweza kusababisha ulemavu wa kudumu na hata vifo kwa wagonjwa na kwamba hali hiyo inaweza kusababisha athari za kiafya kwa Muuguzi kutokana na kutopata muda wa kutosha wa kupumzika na kuwa na mzigo mkubwa wa kazi.

Katibu Mwenezi huyo wa TANNA mkoa wa Ruvuma alibainisha kuwa Halmashauri karibu zote mkoani Ruvuma hazitoi posho ya sare kwa wauguzi ambayo ni stahiki yao kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009.

"Wauguzi tunasikitika kusema kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Songea pekee ndiyo inatoa posho za sare, lakini halmashauri nyingine zote saba katika mkoa wa Ruvuma hazitekelezi agizo hili hali ambayo inachangia kushusha morali ya wauguzi katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku", alisema Pili.

Hata hivyo Pili alisema licha ya kuwepo kwa changamoto hizo, bado wauguzi wa Mkoa wa Ruvuma wanahudumia wagonjwa kwa upendo na ufanisi wa hali ya juu, wanatoa huduma kwa wagonjwa kwa kuzingatia miongozo ya serikali, kanuni na miongozi ya taaluma ya uuguzi.

Katika kukabiliana na upungufu mkubwa wa wauguzi katika Mkoa wa Ruvuma, Muuguzi Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Hilda Ndambalilo, wameanzisha mradi wa kuzalisha wauguzi 100 kila mwaka toka Chuo cha Uuguzi Kiuma na kwamba mradi huo utafanyika kwa miaka mitano. Alisema Mmiliki wa chuo cha Kiuma amekubali kusomesha kwa gharama zake mwenyewe wauguzi 50 na wauguzi wengine 50 watalipiwa kupitia maombi ya mradi huo ambayo yamewasilishwa Wizara ya Afya na kwamba mpango huo unatarajia kupunguza tatizo la upungufu wa wauguzi katika mkoa wa Ruvuma kwa asilimia 90.

Mkuu wa Wilaya ya Songea Pololet Mgema alisema wilaya ya Songea na Mkoa wa Ruvuma umedhamiria kuhakikisha kuwa hadi kufikia mwaka 2020 kila kijiji, kata na wilaya ziwe zimejenga kituo cha kutolea huduma za afya na kwamba changamoto kubwa ambayo inaathiri mpango huo ni upungufu mkubwa wa wauguzi.

"Tumepata taarifa kuna asilimia 65 ya upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta ya Afya katika mkoa wa Ruvuma kwa ujumla, kwa hiyo kwa vyovyote vile hata kama tutakuwa na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata na Wilaya ambavyo vitatekeleza sera ya afya ya msingi, upungufu wa wauguzi ni changamoto kubwa", alisisitiza Pololet

Alisema licha ya kuwepo kwa Vyuo mbalimbali vya serikali na binafsi vinavyotoa mafunzo ya afya katika ngazi ya wakunga na wauguzi, lakini kwa miaka mingi bado idadi ya wauguzi waliozalishwa haijafikia malengo ya muuguzi mmoja kuhudumia watu 500. Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dk. Gozibert Mutahyabarwa alisema licha ya wauguzi kukabiliwa na changamoto mbalimbali, alishauri wauguzi nchini kuacha mfumo uliozoeleka wa kusubiri wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya badala yake kuangalia uwezekano wa kuifikia jamii kwa kuwafuata walipo.

Dk. Mutahyabarwa alisisitiza kuwa hali hiyo itapunguza idadi kubwa ya wagonjwa wanaougua na kupoteza maisha kila mwaka kwa kukosa elimu ya afya na huduma za matibabu.

"Takwimu za kitaifa na zile za Shirika la Afya Duniani zinaonesha vifo vya mama, watoto, UKIMWI, kifua kikuu, kusukari, bado ni tatizo kubwa; tuangalie mfumo ambao tunautumia kama kweli unaweza kupunguza au kumaliza matatizo, mfumo wa kukaa na kusubiri wagonjwa hatutafika", alisisitiza Dk. Mutahybarwa.

Pia alisema kuwa matatizo yote ya kiafya yapo katika jamii, hivyo ni vema kwenda kuyaibua katika jamii na kwamba haitakiwi kusubiri kwenye zahanati, kituo cha Afya au hospitali badala yake kuweka mipango ya kusogeza huduma kwa wananchi ili kuifikia jamii kwa sababu matatizo yapo kwenye jamii.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Christina Mndeme alisema licha ya wauguzi kukabiliwa na changamoto mbalimbali anatambua wauguzi ni shina na mzizi katika utekelezaji wa huduma katika vituo vya afya.

Scanned by CamScanner

Ukweli kuhusu umeme wa REA mkoani Ruvuma

Naibu Waziri wa Nishati na Madini Dk.Medard Kelamani mwaka jana alifanya uzinduzi wa mradi wa umeme vijijini katika Mkoa wa Ruvuma.

Uzinduzi huo kimkoa ulifanyika katika kijiji cha Litapwasi wilayani Songea na kushirikisha wabunge wa mkoa wa Ruvuma, watendaji toka TANESCO makao makuu, Wakala wa umeme vijijini (REA), wakuu wa wilaya, wenyeviti wa Halmashauri na wananchi wa Jimbo la Peramiho.

Akizungumza kabla ya uzinduzi huo Naibu Waziri wa Nishati na Madini Dk. Kalemani aliitaja azima ya serikali kuwa ni kusambaza umeme katika vijiji vyote vya mkoa wa Ruvuma na mikoa mingine kupitia Wakala wa umeme vijijini (REA) ili umeme huo uweze kuchochea maendeleo hadi vijijini.

Dk. Kalemani alivitaja vijiji 440 kati ya vijiji 547 vilivyopo katika mkoa wa Ruvuma ambavyo bado havina umeme hivyo kupitia mradi wa REA awamu ya tatu vijiji vyote vitapelekewa umeme.

Alisema REA awamu ya tatu ilianza Agosti 2017 ambapo jumla ya vijiji 270 vilijumuishwa kwenye mpango wa kupelekewa umeme, hadi kufikia mwaka 2021 vijiji vyote katika mkoa wa Ruvuma vitakuwa vimepelekewa umeme.

"REA itapeleka umeme katika vijiji vyote, vitongoji vyote na Taasisi zote za umma zikiwemo shule, vituo vya afya, zahanati, masoko, magereza, misikiti na makanisa yote kwa bei ya shilingi 27,000 tu ya kuingiza umeme, lazima wapeleke umeme nyumba kwa nyumba", alisisitiza Dk. Kelamani.

Hata hivyo alisema wananchi wanapaswa kujenga nyumba bora na imara ambazo zinafaa kuingiziwa umeme na kwamba suala la kupeleka umeme kwa kila nyumba ni la lazima."Licha kuhamasisha ujenzi wa nyumba nzuri, haijalishi unaishi nyumba gani, iwe unaishi nyumba ya tembe tunakutundukia umeme humo humo, hata nyumba ya matope tunakutundukia umeme humo humo, tunachotaka umeme utumike na kila mmoja wetu", alisema Dk.Kelamani.

Mkandarasi ambaye anafanyakazi ya kujenga mradi wa umeme wa REA awamu ya tatu katika mkoa wa Ruvuma ni Namis Cooperative LTD (kipindi cha miezi 24 kuanzia 2017 hadi 2019). Mkurugenzi Mtendaji wa NAMISI Thomas Uiso anasema kampuni yake imeweka mikakati ya kuhakikisha wanakamilisha kazi hiyo mapema kabla ya muda wa mkataba wa kukamilisha kazi hiyo haujamalizika.

Uiso alibainisha kuwa Kampuni hiyo imeanza kazi katika Kijiji cha Litapwasi wilayani Songea mahali ambapo uzinduzi wa mradi huo umefanyika kimkoa na kusambaaa katika vijiji vyote vya mkoa wa Ruvuma ambavyo vipo kwenye mradi huo. Hata hivyo Naibu Waziri huyo wa Nishati na Madini alikiri kuwa mkoa wa Ruvuma haupati umeme wa kutosha kwa sababu wanatumia umeme unaotokana na nguvu ya umeme wa mafuta na nguvu ya maji kwa kiasi kidogo kutoka kwa wazalishaji wadogo wa umeme huo wa maji.

Alisema kutokana na hali-hiyo serikali hivi sasa inajenga mradi mkubwa wa kusafirisha umeme wa Grid ya Taifa kutoka Makambako mkoani Njombe, kupitia Madaba hadi Songea mjini umbali wa kilometa 250 ili umeme wa kutosha uweze kuwafikia wananchi na utumike kwa maendeleo endelevu.

Dk.Kelamani anasema serikali inajenga vituo vya kupoozea umeme huo wa Grid ya Taifa na kuuongeza nguvu kutoka kilovolti 132 hadi kilovolti 220 ambao utakuwa umeme mkubwa kwa matumizi ya viwanda.

Hata hivyo alisema umeme wa Grid ya Taifa, utatumika kusambaza umeme katika vijiji 120 vya mkoa wa Ruvuma na Njombe na kwamba umeme huo utatoa umeme kwa wateja wapya 22,700.

Waziri Kalemani aliwashauri watanzania kutumia umeme kwa kujenga viwanda vidogo na kusindika mazao mbalimbali ambayo yanalimwa katika mkoa wa Ruvuma yakiwemo Mahindi, Kahawa, korosho, alizeti na mazao ya matunda ili kuongeza thamani ya mazao wanayozalisha.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhandisi Stella Manyanya ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Nyasa mkoani Ruvuma alisema wananchi wa mkoa huo wataanza kuishi sawa na wananchi wengine wenye umeme wa kutosha baada ya kuzinduliwa mradi wa umeme vijijini. "Umeme utachochea na kuongeza kiwango cha ufaulu katika shule za msingi na sekondari, utachochea shughuli za uzalishaji ,na ukuaji wa uchumi kwa sababu wananchi wataanzisha viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ambavyo pia vitatoa ajira kwa vijana",alisema Manyanya.

Naye Mwenyekiti wa wabunge wa Mkoa wa Ruvuma ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Madaba Joseph Mhagama aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa kutoa ushirikiano mkubwa ambao ulisababisha vijiji vyote vya mkoa wa Ruvuma kuingizwa katika mpango wa kupelekewa umeme.

Mbunge wa Jimbo la Peramiho ambaye pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye ulemavu Jenista Mhagama anawaasa wananchi wote wa mkoa wa Ruvuma kujiandaa kutumia umeme huo kwa shughuli za maendeleo ya kiuchumi.

"Baada ya miaka miwili kuanzia sasa Jimbo la Peramiho libadilike, uchumi wetu ulingane na uwepo wa umeme ni nafasi nyingine nzuri ya kuanza kubadilisha ujenzi wa nyumba zetu kwa sababu umeme haukai kwenye nyumba za nyasi, weka bati", alisisitiza Mhagama.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa REA Mhandisi Gissima Nyamohanga alisema miradi ya umeme vijijini imekuwa inaendelea katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na sasa katika mkoa wa Ruvuma.

Hata hivyo Nyamohanga alibainisha zaidi kuwa Serikali kupitia REA inaendelea kufanya mradi wa kupeleka umeme wa Jua katika wilaya za Songea, Tunduru na Namtumbo mkoani Ruvuma ambapo umeme huo unawekwa katika zahanati, vituo vya afya na shule za sekondari lengo likiwa ni kuhakikisha mkoa mzima unapata nishati ya kutosha kwa maendeleo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa REA, serikali imefanya juhudi kubwa ya kuendelea kuongeza vyanzo vya umeme wa maji kikiwemo chanzo cha maji cha Tulila katika wilaya ya Songea na chanzo cha Andoya katika wilaya ya Mbinga ambavyo vinazalisha umeme na kuchangia kuboresha umeme katika mkoa wa Ruvuma.

Kulingana na Nyamohanga, katika awamu ya pili ya mradi wa umeme wa REA jumla ya vijiji 72 katika mkoa wa Ruvuma vilipatiwa umeme na jumla ya sh.bilioni 26.53 zilitumika katika mradi huo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO Dkt.Tito Mwinuka akizungumza kwenye uzinduzi huo alibainisha kuwa hadi kufikia mwaka 2021 katika nchi nzima zaidi ya vijiji 12,000 vitakuwa vimepelewa umeme na kwamba wananchi wanapaswa kulinda miundombinu ya umeme kwa kuwa serikali inatumia gharama kubwa kuwekeza umeme vijijini.

Sera ya Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata nishati ya umeme, ambapo takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watu wanaopata nishati ya umeme nchini imepanda toka asilimia 10 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 67 mwaka 2017.

Mwandishi ni Mchangiaji wa gazeti hili, mawasiliano yake ni albano. mdelo @ gmail. com, simu 078476591 .

Scanned by CamScanner

Ugonjwa wa malaria bado ni pasua kichwa

Inaendelea kutoka toleo lililopita

Na Albano Midelo

Takwimu kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2002 zinaonesha kuwa kila mwaka watu kati ya milioni 300 hadi 500 duniani wanapata ugonjwa wa malaria, kati yao watu milioni moja na nusu wanakufa kutokana na ugonjwa huo.

Kulingana na takwimu hizo katika Bara la Afrika watoto wadogo wenye umri chini ya miaka mitano ndiyo wanaathirika zaidi na ugonjwa wa malaria ambapo kila mwaka watoto milioni tano wanakufa kwa ugonjwa huo barani Afrika.

Kwa mujibu wa WHO idadi ya vifo vinavyotokana na ugonjwa wa malaria hadi kufikia mwaka 2013 vimepungua kwa takriban asilimia 20 tu duniani kote ambapo theluthi moja ya nchi 108 ambazo malaria ilikuwa imeenea zilitarajiwa kutokomeza ugonjwa huo katika kipindi cha miaka 10.

Malaria imetokomezwa katika nchi tatu tangu mwaka 2007 ambazo ni Morocco, Turkmenistan na Armenia ambapo Shirika moja la Roll Back , lilidhamiria kutokomeza malaria katika nchi nyingine 10 mwaka 2015, zikiwemo nchi za bara la Ulaya.



Mratibu wa Asasi ya ORES-Tanzania ambayo inashiriki katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria Dk.Hermengild Mayunga anasema ili kufanikisha mapambano dhidi ya ugonjwa huo inatakiwa kuongezwa ushiriki wa wanasiasa, viongozi wa serikali na jumuiya katika masuala mtambuka juu ya malaria.

Dk.Mayunga anasema kuwa ugonjwa wa malaria hauna mipaka hivyo msisitizo katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo ni lazima kasi iongezwe kila mwaka ili siku moja ugonjwa wa malaria utokomezwe.

"Tuanze kuhesabu siku za ugonjwa wa malaria kuwasumbua watanzania zinakwisha mbona wenzetu wameweza sisi tushindwe kuna nini hapa",anahoji Dr Mayunga.

Dr.Mayunga anashauri wanasayansi kuibua mbinu mpya, mikakati mipya na utalaam mpya wa kitafiti katika kutokomeza malaria na kujifunza kutoka katika nchi ambazo tayari zimetokomeza malaria.

WHO inaeleza kuwa Mwaka 2015 visa zaidi ya milioni 200 vya malaria viliripotiwa na zaidi ya vifo Laki Nne.Katika Bara la Afrika hususani nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara; mwaka 2015, kulikuwa na asilimia 89 ya visa vya malaria na asilimia 91 ya vifo.

Hata hivyo WHO imelenga kutokomeza ugonjwa wa malaria katika nchi 35 ifikapo mwaka 2030 na kwamba lengo hilo linaweza kufanikiwa licha ya kuwa ni la juu. Bara la Ulaya mwaka 2015 halikuwa na kisa chochote cha malaria.

Ripoti mpya ya WHO inaonesha kuwa vifo vilivyotokana na ugonjwa wa Malaria vimeshuka 438,000 hadi kufikia mwaka 2015, ikiwa ni idadi ndogo ikilinganishwa na mwaka 2000, ambapo watu 839,000 waliuawa na Malaria.

Kwa Mujibu wa WHO zaidi ya asilimia 35 ya vifo vyote vinavyotokana na Malaria duniani vinatokea katika nchi mbili za Kiafrika ambazo ni Nigeria na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Ripoti ya WHO inaeleza kuwa mwaka wa 2013, zaidi ya watu milioni 198, waliambukizwa ugonjwa wa malaria na ilikadiriwa watu 584,000 walikufa kutokana na ugonjwa huo ambapo watu bilioni 3.2 wanakabili hatari ya kuambukizwa malaria duniani kote.

Sote kwa pamoja tuungane ili kuendeleza mapambano ya kuushinda ugonjwa wa malaria ambao ni hatari kubwa kwa nchi nyingi barani Afrika ikiwemo nchi ya Tanzania.

Katika hospitali zetu hapa Tanzania malaria imeendelea kuwa pasua kichwa, kutokana na ukweli kwamba bado njia stahiki hazijachukuliwa kwa hoja ya kuutokomeza ugonjwa huo.

Kilichowakuta Babu Seya na Wanawe toka mwaka 2013.....!

Na Mwandishi wetu

Ukweli ni kwamba, Mwaka 2004 Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliwahukumu Nguza Viking, maarufu kwa jina la Babu Seya na watoto wake watatua mbao ni Papii Kocha, Nguza Mbanguna na Francis Nguza kifungo cha maisha jela kwa makosa ya kubaka na kulawiti watoto.

Kesi hiyo iliyuta hisia za watanzania wengi kutokana na umaarufu wa wasanii hao na kuhusika kwa familia nzima katika makosa mazito kama hayo. Rufaa mbalimbali zilikatwa na mawakili maarifu nchini lakini hawakuweza kuwatoa wasanii hao. Mwaka 2010, rufaa yao nyingine ilisikilizwa katika Mahakama ya Rufaa, na kuwaachia huru Nguza Mbangu na Francis Nguza kufuatia kutokukutwa na hatia katika makosa yote waliyoshitakiwa.

Baada ya rufaa hiyo, Babu Seya na mwanaye Papii Kocha walipatikana na hatia na hivyo kuendelea kutumikia adhabu ya kifungo cha maisha jela. Tarehe 30 Oktoba 2013, Mahakama ya Rufaa iliyoketi chini ya jopo la majaji watu, likiongozwa na Nathalia Kimaro, akisaidiana na Mbarouk Mbarouk na Salum Masati walisikiliza hoja za pande zote kuhusu ombi la kufanyika mapitio ya uamuzi wa awali wa mahakama hiyo.

Upande wa utetezi ukiongozwa na wakili wao Mabere Marando uliomba kupitiwa upya kwa uamuzi huo, ukidai kuwepo kasoro katika ushahidi uliowatia hatiani, ikiwemo kukosekana kwa mashahidi muhimu katika kesi hiyo.

Majaji walisema kuwa kuna uthibitisho kwamba warufani hao wawili waliwabaka watoto wa shule ya msingi mwaka 2003. Kesi hiyo iliwashtua mashabiki wa mwanamuziki Nguza Viking nchini Tanzania na ukanda mzima wa Afrika Mashariki. Mwanamuziki huyo ambaye ni mzaliwa wa DRC, ameishi Tanzania kwa miaka mingi na kuwa na mashabiki wengi.

Siku zote walipofikishwa mahakamani walionekana kuwa watulivu hata wakati majaji walipotupilia mbali ombi lao la kutaka hukumu yao kubatilishwa.

Juni 25, 2004 Mahakama ya Hakimu Mkazi Kusutu, Dar es Salaam, iliwatia hatiani Babu Seya na wanawe 'Papii Kocha', Nguza Mbangu na Francis Nguza kwa kupatikana na hatia ya kubaka na kulawiti. Januari 27 mwaka 2005, Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Thomas Mihayo alitupili ambali rufaa yao iliyokuwa ikipinga hukumu iliyotolewa na aliyekuwa Hakimu Mkuu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Addy Lyamuya ambaye aliwatia hatiani kwa makosa yote waliyo kuwa wameshitakiwa nayo Juni 25 mwaka 2004.

Babu Seya na wanawe walidaiwa kutenda makosa 10 ya kubaka watoto wa Shule ya Msingi Mashujaa wenye umri kati ya miaka sita na minane na makosa mengine 11 ya kulawiti watoto wa kike wenye umri huo huo kati ya Aprili na Oktoba 2003 katika maeneo ya Sinza kwa Remmy wilayani Kinondoni Dar es Salaam.

Kwa sasa wote wapo huru baada ya kukuachiwa, kwa msamaha wa Rais.

(Habariko)

Scanned by CamScanner

MAKALA

Na Albano Midelo

Makao Makuu ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Halmashauri Songea yang'ara na Benki ya Dunia

HOTUBA ya Waziri Mkuu mstaafu wa Tanzania, Mizengo Pinda aliyoitoa mwaka 2013 katika uzinduzi wa mradi wa kuimarisha halmashauri za miji na manispaa 18 Tanzania Bara, inathibitisha serikali ilivyojipanga kuendeleza halmashauri kiuchumi.

Mradi huo kuendeleza halmashauri za miji na manispaa (ULGSP) unatanyika kupitia Benki ya Dunia baada ya halmashauri hizo kukidhi vigezo vilivyowekwa kwa ajili ya safari ya miaka mitano inayohitimishwa mwaka 2018.

Tanzania ni nchi ya kwanza katika Afrika kuteuliwa kufanya majaribio ya mfumo wa kupima matokeo ya mradi.

Katika uzinduzi huo, Pinda aliasa watendaji kwenye halmashauri hustika kufanya kazi kwa uadilifu na uwajibikaji wa hali ya juu kwa kuzingatia vigezo na taratibu zote zilizowekwa, kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Serikali pia kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeandaa Mpango Kamambe wa Mipango Miji utakaoainisha matumizi bora ya ardhi na kuondoa migogoro ya ardhi nchini.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula anaeleza kuwa wizara inashirikiana halmashauri 18 kupitia ULGSP katika kuandaa mipango miji hiyo.

Anasema wizara yake inaandaa na kukamilisha programu ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi Tanzania itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2015 hadi 2025.

Mabula anasema serikali kupitia mradi huo ipo katika mchakato wa kununua vifaa vya upimaji ambavyo vitasambazwa katika kanda nane za wizara ili halmashauri zilizo ndani ya mradi zinufaike.

Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma ni miongoni mwa halmashauri zilizoingizwa kwenye mradi.

Halmashauri ya manispaa ya Songea ina jimbo moja la uchaguzi, tarafa mbili, kata 21 na mitaa 95 yenye jumla ya kaya 61,930. Manispaa hiyo inakadiriwa kuwa na idadi ya watu 237,843.

Mchumi Mkuu wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Raphael Kimary anasema wamepanga kutekeleza miradi minane chini ya mradi wa uendelezaji Miji na Manispaa katika kuanzia mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Kimary anasema manispaa itatumia zaidi ya sh bilioni 21.8 katika kutekeleza miradi hiyo ambayo inatekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Anataja miradi hiyo kuwa ni ukarabati wa kilometa 15 za barabara kwa kiwango cha lami kwa gharama ya zaidi ya Sh milioni 11.5. Pia wananunua magari ya kuzolea taka kwa gharama ya zaidi ya Sh bilioni 1.14

Miradi mingine ni ujenzi wa stendi mpya wa mabasi katika eneo la shule ya Tanga kwa gharama ya Sh bilioni tano, ujenzi wa machinjio [illegible]

Shughuli nyingine ni ukarabati wa dampo kwa Sh bilioni 1.5, kujenga uwezo watumishi na viongozi wa kisiasa Sh milioni 200 na ukarabati wa bustani ya manispaa Sh milioni 300.

Halmashauri ya Manispaa ya Songea tayari imepokea zaidi ya Sh bilioni 7.54 kwa ajili ya kutekeleza mpango huo wa ULGSP.

Mchumi mkuu huyo wa manispaa anasema fedha ambazo zimepokewa kutoka toka Hazina kwa mwaka wa fedha 2015/2016 zimeletwa kwa awamu mbili.

Awamu ya kwanza, Mei 2016, walipokea Sh bilioni 2.72 na ya pili, Oktoba mwaka huu wamepokea Sh bilioni 4.82.

Kimary anasema katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, manispaa kupitia mpango huo ilipanga kutekeleza miradi minne ukiwemo wa ujenzi wa kilometa 4.7 za barabara kwa kiwango cha lami.

Katika miaka mitano, wamepanga kutekeleza miradi minane yenye thamani ya zaidi ya Sh bilioni 21.

Hata hivyo, Kimary anasema, mradi umedhamiria kuongeza mapato ya ndani kwa kutumia mfumo wa mapato, kuimarisha uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya serikali.

Pia unahyusika na ujenzi wa miundombinu, kuongeza, uwajibikaji, usimamizi wa rasilimali za halmashauri na kuongeza uwezo wa halmashauri.

Ofisa Mapato na matumizi katika halmashauri ya manispaa ya Songea, Elems Salvatory anasema manispaa ilianza kutumia mfumo wa kielekroniki wa ukusanyaji mapato ya ndani kuanzia Septemba, 2015. "Mfumo huu unatumika kukusanyia mapato ya ndani ambao unadhibiti upotevu wa mapato",anasema Salvatory.

Anasisitiza faida za matumizi ya mfumo wa kieletroniki kuwa umerahisisha ukusanyaji mapato kwa kutumia mfumo mmoja, uturzaji wa kumbukumbu za makusanyo ya mapato na upatikanaji wa taarifa za mapato umerahisishwa.

Salvatory anataja faida nyingine ya matumizi ya mfumo kuwa umesaidia kutoa hati za madai kwa wateja wake kulingana na vyanzo vilivyopo sanjari na kudhibiti ubadhilifu wa fedha za makusanyo.

Kwa mujibu wa ofisa mapato huyu, katika kipindi cha mwaka 2015/2016, manispaa ilikusanya sh bilioni 1.4.

Katika mwaka huu wa fedha wa 2016/2017, ndani ya kipindi cha miezi sita, wamefanikiwa kukusanya mapato ya Sh bilioni 1.1.

"Hivyo hadi mwisho wa mwaka huu wa fedha tunaweza kukusanya shilingi bilioni mbili," anasema.

Anasema kutokana na faida za matumizi ya mfumo, halmashauri ilitenga fedha kwa ajili ya kuongeza mashine 30 za kukusanyia mapato kwenye bajeti yake ya mwaka 2017/2018 kupitia mradi wa ULGSP; ambazo sasa zinatumika.

Anasema upatikanaji wa mashine hizi utawawezesha ufanisi katika ukusanyaji wa ushuru wa mazao na katika maegesho ya magari.

Vyanzo vingine vya mapato ni ushuru wa misitu, ushuru wa masoko, ushuru wa matangazo,ushuru wa mabango, ushuru wa machinjio na ushuru wa stendi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Tina Sekambo anasema kutokana na ufanisi na tija kwa mfumo wa kieletrotiki wa kukusanya mapato, halmashauri imeamua kuunganisha mfumo huo katika Benki ya NMB kurahisisha kazi kwa wateja wa manispaa hiyo.

Anasema halmashauri imeanzisha tawi la NMB Ofisi kuu ya Manispaa ili kurahisisha wateja kulipa kodi na ushuru kwa urahisi badala ya kupoteza muda kwenda kwenye tawi la benki hiyo ambalo lipo mbali na ofisi za manispaa hiyo.

Anasema ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mfumo pia unafanyika katika kituo cha mabasi cha mjini kati ambacho kilifunguliwa rasmi Julai 29 mwaka huu baada ya kazi ya kukarabati kukamilika.

Sekambo anasema karabati wa kituo cha mabasi ulianza Novemba 25, 2014. Hatua ya kwanza imehusisha ujenzi wa eneo la kuegesha mabasi ulioghari[illegible] ioni 499. Hata hivyo, anasema hatua ya pili ya ukarabati wa kituo hicho utahusisha ujenzi wa majengo ya biashara utakaogharimu zaidi ya Sh bilioni 5.25.

Majengo hayo ya biashara yatajengwa na wafanyabiashara na wadau mbalimbali kwa njia ya jenga, endesha, kabidhi.

Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Abdul Mshaweji anasema wameweka mpango mkakati wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020.

Lengo ni kuwa na mwelekeo wa utoaji wa huduma za msingi za kuanzishwa kwa halmashauri ya jiji la Songea.

Mshaweji anabainisha zaidi kuwa manispaa inatarajia kufikia malengo ya kuwa jiji kwa kuzingatia sayansi, teknolojia, utawandawazi na soko huru kwa kufuata sheria,kanuni na taratibu.

Ili kuhakikisha uchumi unakua, Mshaweji anataja mwelekeo ni kuongeza uzalishaji na mauzo ya bidhaa, kukusanya mapato kwa njia ya kielektroniki pamoja na kuwa na miradi ya uzalishaji yenye tija na utendaji wenye maadili na nidhamu kwa kuzingatia kauli mbiu ya 'Hapa kazi tu' ifikapo mwaka 2017.

Albano Midelo ni mchangiaji katika gazeti hili anapatikana baruapepe:albano.midelo@gmail.

Scanned by CamScanner

Mpango wa TASAF wanusuru kaya masikini Songea

Na Stephano Mango, Songea

RUZUKU ya TASAF inayotolewa kwa kaya masikini katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma imebadilisha maisha ya baadhi ya kaya na kuweza kuendesha maisha bila utegemezi kama yaliyo malengo ya mpango huo kitaifa.

Hivyo kama zilivyo Halmashauri zingine nchini ndivyo Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma imeendelea kupokea fedha kwa ajili ya mpango wa kunusuru kaya masikini kupitia mradi wa TASAF III lengo likiwa ni kupunguza umaskini kwa watu wasiojiweza.

Taarifa zilizopo ni kuwa hadi kufikia mwezi Mei mwaka 2016 zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni 628 zilikuwa zimepokelewa ingawa mwezi Mei,2016 haikupolewa fedha yoyote kwa ajili ya kaya masikini.

Takwimu za mapokezi ya fedha za TASAF III kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya masikini zinaonesha kuwa kuanzia Julai 2015 hadi Mei 2016 zaidi ya shilingi bilioni 1.628 zilipokelewa na zimeendelea kutolewa kwa kaya masikini za wakazi wa mitaa 95 ya Manispaa ya Songea.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya manispaa hiyo uzinduzi wa TASAF awamu ya tatu ulifanyika Januari 5 mwaka 2015 ambapo uzinduzi ulifanywa na mkuu wa mkoa wa Ruvuma wakati huo, Said Thabit Mwambungu.

Wakihojiwa na timu ya maafisa wa TASAF wakiwa na wanahabari katika ziara ya kutembelea na kukagua kaya masikini ambazo zinapewa ruzuku na TASAF katika kata ya Mjimwema mjini Songea, baadhi ya wananchi waliopata ruzuku hiyo wamesema maisha yao yamebadilika kabisa tofauti na hali ambayo walikuwa nayo kabla ya kuanza kupata ruzuku hiyo.

Hawa Hassan (60) mkazi wa mtaa wa kijiweni, kata ya Mjimwema alisema kabla ya kupata ruzuku ya shilingi 36,000 kutoka TASAF alikuwa anaishi katika mazingira magumu kwa kuwa mume wake alimuacha mara ya baada ya kupata maradhi ya miguu.

"TASAF walinipatia ruzuku ya shilingi 36,000,niliamua kuanza biashara ya ndogo ndogo ya kuuza mafuta ya kula na nyanya, nilicheza upato nikapata shilingi laki moja mwezi Machi mwaka huu nilinunua kuku wa mayai 74 ambao sasa wamekua na maisha yanaendelea vema," alisema Hawa.

Hawa alisema hivi sasa ana uhakika wa maisha, hata kama serikali itasimamisha ruzuku inayotolewa na TASAF kwa kuwa miradi yake inaendelea vizuri, na kwamba kuku wake wanaanza kutaga mayai na majogoo aliyonayo anaweza kuuza Jogoo moja hadi shilingi 20,000.

Katerina Kayombo (85) mkazi [illegible] Kijiweni, Mjimwema yamekuwa bora zaidi kwa kuwa zamani alikuwa ombaomba lakini sasa anaweza kupata chakula na kwamba ameanzisha bustani ya mboga ambazo anauza na kujipatia walau kila siku shilingi 2000.

Wananchi wengine ambao wameipongeza serikali kupitia ruzuku ya TASAF katika kaya masikini ni Selina Njelekela (50) ambaye anasema kabla ya mradi wa TASAF alikuwa anakula mlo mmoja kwa siku ambapo hivi sasa ana uhakika wa kula milo mitatu huku akijishughulisha na biashara ndogo ndogo zinazomhakikishia chakula kila siku.

Halima Komba (40) anasema kwa miaka mingi alikuwa anaishi katika kibanda kibovu kilichoezekwa kwa turubai hivyo alikuwa anavujiwa ambapo kupitia mradi wa ruzuku ya TASAF ameweza kuboresha nyumba yake na kuanzisha biashara ndogo ndogo.

Kristopher Ngonyani afisa wa TASAF katika Halmshauri ya manispaa ya Songea anasema TASAF imeendelea kupokea fedha kwa ajili ya mpango wa kunusuru kaya masikini kupitia mradi wa TASAF awamu ya tatu lengo likiwa ni kupunguza umaskini kwa watu wasiojiweza.

Ngonyani alibainisha kuwa takwimu za mapokezi ya fedha za TASAF awamu ya tatu kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya masikini zinaonesha kuwa kuanzia Julai 2015 hadi Mei 2016 zaidi ya shilingi bilioni 1.628 zilipokelewa na zimeendelea kutolewa kwa kaya masikini za wakazi wa mitaa 95 ya manispaa ya Songea.

Alisema Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015/2016 kazi mbalimbali zimeendelea kufanyika ambazo ni kulipa kaya maskini 7,828 kati ya lengo la kaya 7,915 zilizopo kwenye mpango, ambapo kaya 88 hazikutokea siku ya malipo hivyo fedha zao kurudishwa TASAF Makao makuu kulingana na utaratibu.

Ili kuhakikisha kuwa TASAF awamu ya tatu inafikia ,malengo yake, Ngonyani alisema mfuko umetoa mafunzo kwa Watendaji wa Kata, Wauguzi, Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kuwajengea uelewa watumishi hao ili wasaidie katika kuondoa umaskini hasa katika kufuatilia masharti ya elimu na afya.

Alisema kuwa Mfuko pia umelenga kutoa elimu kwa kaya maskini (wananchi) kuhusu kilimo cha mazao mbadala ambayo hayatumii mbolea za viwandani.

Wananchi hao masikini walifundishwa kilimo cha mazao ya maharagwe, karanga, alizeti,ndizi, mtama. Wananchi hao masikini walifundishwa kuandaa mbolea ya asili.

Mafunzo haya yalifanyika mwaka 2015 katika mitaa ya manispaa ya Songea ikiwemo Mitaa ya Lilambo A, Mwanamonga na Sinai kata ya Mletele, Nonganonga na Mdundiko kata ya Mletele, Tanga na Mlete kata ya Tanga, Ndilimalitembo, Mahilo na Chemchem.

Hata hivyo, Timu ya ufuatiliaji ya Wilaya na Mkoa ilifanya ziara kwenye mitaa minne ya Mwengemshindo,Luhira kati, Mitendewawa na Chandarua ili kusikiliza kero za wanufaika wa kaya masikini na kuzitatua.

Uchunguzi umebaini kuwa mpango wa TASAF wa kuzinusuru kaya masikini umeleta mafanikio ikiwemo kuimarika kwa mahudhurio ya watoto shule za Msingi na Sekondari, kuongezeka kwa mahudhurio ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kliniki na wanufaika wengi kuanza kujiunga na Mfuko wa Afya wa Jamii.

Baadhi ya wakazi wa manispaa ya Songea wameipongeza Serikali kwa kuanza mpango huo wa TASAF III ambao wamesema utaleta manufaa kwa Kaya maskini na kusisitiza tangazo la siku ya malipo liwe linatolewa mapema ili kila mnufaika apate malipo kama inavyostahili, pia kwa walengwa ambao watathibitika kuwa na matatizo kwa siku za malipo, uandaliwe utaratibu maalum wa kuwalipa.

Katika hatua nyingine Taarifa ya idara ya fedha ya manispaa ya Songea inaonesha kuwa matumizi ya fedha za maendeleo kuanzia Julai 2015 hadi Mei 2016 yalikuwa ni zaidi ya shilingi bilioni nne na milioni 179.

Mchanganuo wa fedha hizo unaonesha kuwa zaidi ya shilingi milioni 33 zilitumika kwa ajili ya mipango, mfuko wa barabara zaidi ya shilingi milioni 560 na Benki ya Dunia zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni 581.

Matumizi mengine ni maji zaidi ya shilingi milioni 72,mfuko wa jimbo zaidi ya shilingi milioni nne, mfuko wa afya zaidi ya shilingi milioni 102, SEDP zaidi ya shilingi milioni 186 na mfuko wa TASAF III zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni 638.

Halmashauri ya manispaa ya Songea katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 iliidhinishiwa na Bunge kukusanya na kutumia zaidi ya shilingi bilioni 44 na milioni 937 kuanzia Julai 2015 hadi Mei 2016 ambapo mapato halisi yalikuwa ni zaidi ya shilingi bilioni 33 na milioni 152 sawa na asilimia 73 ya makisio kwa mwaka.

Awamu ya tatu ya TASAF ilizinduliwa rasmi Agosti 2012 Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete ambapo Mpango wa kunusuru Kaya Maskini unatekelezwa ili kujenga uwezo na kuwezesha kaya Maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu na kuboresha maisha.

Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa namba 0755-335051, 0715-335051, [illegible] 335051, 0778-335051

Wananchi hao masikini walifundishwa kilimo cha mazao ya maharagwe, karanga, alizeti,ndizi, mtama. Wananchi hao masikini walifundishwa kuandaa mbolea ya asili

Scanned by CamScanner

Songea waendelea kutathimini wajasiriamali, kaya maskini

Na Stephano Mango, Songea

HALMASHAURI ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma imetoa mkopo wa zaidi ya shilingi milioni 52 katika vikundi 107 vya wajasiriamali ili kuendeleza miradi yao.

Akizungumza wakati anafungua mafunzo ya vikundi hivyo kabla ya kutoa mikopo yalifanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea, Kaimu mkurugenzi wa manispaa hiyo Raphael Kimary aliwaasa wajasiriamli hao kuwa na nidhamu katika mikopo na kuhakikisha wanarejesha kwa wakati.

Kimary ambaye pia ni mchumi wa manispaa hiyo alibainisha kuwa mkopo huo wa fedha umetolewa na manispaa kwa lengo kusaidia vikundi vya wajasirimali katika shughuli za uwekezaji na kuhakikisha wanarejesha ili kusaidia vikundi vingine vya wajasirimali katika manispaa hiyo.

"Zingatieni taratibu zote za mafunzo ambayo mmepewa kabla ya kupewa mkopo, fedha hizo zisifanye mambo ambayo hayapo katika mradi huo, muwe wajasirimali wa kweli ili muweze kuondokana na umaskini, kumbukeni fedha tunazowakopesha zitafuatiliwa na mnatakiwa kurejesha mkopo kwa wakati ili tuendelee kuwakopesha wajasirimali wengine," alisisitiza Kimary.

Kwa upande wake afisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa hiyo, Naftali Saiyoloi aliaema mkopo huo unatolewa kwa vikundi vya wanawake na vijana na kwamba lengo ni kuinua hali ya uchumi katika makundi hayo mawili.

Kwa mujibu wa afisa maendeleo huyo,mfuko wa kukopesha wanawake na vijana ulianzishwa mwaka 1993 na kwamba mfuko huo licha ya kuwa na fedha kidogo ,umelenga kuongeza ajira,kuinua uchumi wa mwananchi wa kawaida na hasa vijana na wanawake.

"Masharti yanayomwezesha mjasiriamali kupata mkopo huo, awe mwanamke au kijana mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea, awe amejiunga kwenye vikundi vya kuanzia watu watano, kikundi kiwe na katiba,mkopo unalipwa ndani ya mwaka mmoja kwa riba ya asilimia 10 tu," alisema.

Akitoa mada ya kanuni za kikundi, akiba ya pamoja na umuhimu wake, afisa maendeleo ya jamii Scholastica Gowele aliwatahadharisha wajasirimali hao kuwa lengo la mkopo huo sio kuanzisha mradi au biashara mpya badala yake ni kuendeleza biashara ambazo wamezianzisha ili ziweze kuwaletea faida zaidi.

Naye afisa biashara wa manispaa hiyo Raymund Raphael aliwataka wanavikundi kuhakikisha kuwa wanafanya biashara ambayo itawapatia faida hivyo kabla ya kuendeleza biashara zao ni vema kwanza kufanya utafiti ili kufahamu wateja wao na masoko ya biashara zao.

Mada ambazo zimefundishwa katika mafunzo hayo ni historia fupi ya mfuko wa maendeleo ya wanawake na vijana, taratibu na masharti ya mkopo, usimamizi na ulipaji wa mikopo, namna ya kuunda vikundi, uendeshaji na usimamizi wa miradi ya vikundi, soko la biashara, mahusiano ya biashara, utunzaji wa kumbukumbu na ujazaji wa mikataba.

Pia Halmshauri ya manispaa ya Songea mkoani Ruvuma imeendelea kupokea fedha kwa ajili ya mpango wa kunusuru kaya masikini kupitia mradi wa TASAF III lengo likiwa ni kupunguza umaskini kwa watu wasiojiweza.

Ofisa habari wa manispaa ya Songea Albano Midelo alisema hadi kufikia mwezi Mei mwaka 2016 zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni 628 zilikuwa zimepokelewa ingawa mwezi Mei, 2016 haikupolewa fedha yoyote kwa ajili ya kaya masikini.

Takwimu za mapokezi ya fedha za TASAF III kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya masikini zinaonesha kuwa kuanzia Julai 2015 hadi Mei 2016 zaidi ya shilingi bilioni 1.628 zilipokelewa na zimeendelea kutolewa kwa kaya masikini za wakazi wa mitaa 95 ya Manispaa ya Songea.

Awamu ya tatu ya TASAF ilizinduliwa rasmi Agosti 2012 Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete ambapo Mpango wa kunusuru Kaya Maskini unatekelezwa ili kujenga uwezo na kuwezesha kaya Maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu na kuboresha maisha.

Kwa mujibu wa Ofisa habari wa manispaa ya Songea, katika Halmashauri ya Manispaa ya Manispaa hiyo uzinduzi wa TASAF awamu ya tatu ulifanyika Januari 5 mwaka 2015.

Amesema Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015/2016 kazi mbalimbali zimeendelea kufanyika ambazo ni kulipa kaya maskini 7,828 kati ya lengo la kaya 7,915 zilizopo kwenye mpango, ambapo kaya 88 hazikutokea siku ya malipo hivyo fedha zao kurudishwa TASAF Makao makuu kulingana na utaratibu

Ili kuhakikisha kuwa TASAF inafikia malengo yake mfuko umetoa mafunzo kwa Watendaji wa Kata, Wauguzi, Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kuwajengea uelewa watumishi hao ili wasaidie katika kuondoa umaskini hasa katika kufuatilia masharti ya elimu na afya.

Mfuko pia umelenga kutoa elimu kwa kaya maskini (wananchi) kuhusu kilimo cha mazao mbadala ambayo hayatumii mbolea za viwandani.

Wananchi hao masikini walifundishwa kilimo cha mazao ya maharagwe, karanga, alizeti,ndizi, mtama.

Wananchi hao masikini walifundishwa kuandaa mbolea ya asili. Mafunzo haya yalifanyika mwaka 2015 katika mitaa ya manispaa ya Songea ikiwemo Mitaa ya Lilambo A, Mwanamonga na Sinai kata ya Lilambo, Mitendewawa, Chandarua na Muhumbezi kata ya Mshangano, Mletele, Nonganonga na Mdundiko kata ya Mletele, Tanga na Mlete kata ya Tanga, Ndilimalitembo, Mahilo na Chemchem.

Hata hivyo Timu ya ufuatiliaji ya Wilaya na Mkoa ilifanya ziara kwenye mitaa minne ya Mwengemshindo, Luhira kati, Mitendewawa na Chandarua ili kusikiliza kero za wanufaika wa kaya masikini na kuzitatua.

Uchunguzi umebaini kuwa mpango wa TASAF wa kuzinusuru kaya masikini umeleta mafanikio ikiwemo kuimarika kwa mahudhurio ya watoto shule za Msingi na Sekondari, kuongezeka kwa mahudhurio ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kliniki na wanufaika wengi kuanza kujiunga na Mfuko wa Afya wa Jamii.

Baadhi ya wakazi wa manispaa ya Songea wameipongeza Serikali kwa kuanza mpango huo wa TASAF III ambao wamesema utaleta manufaa kwa Kaya maskini na kusisitiza tangazo la siku ya malipo liwe linatolewa mapema ili kila mnufaika apate malipo kama inavyostahili.

Pia kwa walengwa ambao watathibitika kuwa na matatizo kwa siku za malipo, uandaliwe utaratibu maalum wa kuwalipa.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Dk. Binilith Mahenge

SIMU: 0755-335051, 0715-335051, 0784-335051, 0778-335051, E-MAIL; stephano12mango@yahoo.com www.stephanomango.blogspot.

Scanned by CamScanner

Kalamu ya mwandishi yaleta mafanikio,milipuko mgodini yadhibitiwa

Na Greyson Mgol

WAKAZI wa Kijiji cha Ntunduwaro kilichopo kata ya Ruanda wilayani Mbinga mkoani Ruvuma, wamekiri kuwa kalamu ya mwandishi wa Habari inaweza kuleta mabadiliko chanya katika jamii, baada ya kushuhudia milipuko iliyokuwa ikifanywa na mgodi wa makaa ya mawe wa Ngaka wa kampuni ya TANCOAL na kusababisha nyumba zaidi ya 200 kupata nyufa kijijini hapo ikipatiwa ufumbuzi mara tu baada ya waandishi kufika na kuandika habari hizo.

Wakizungumzamakala haya hivi karibuni, baadhi ya wakazi wa kijiji cha Ntunduwaro walisema miongoni mwa kero walizokuwa wakikumbana nazo kutokana na kuwepo kwa mgodi huo jirani na makazi yao ilikuwa ni, kupasuka kwa kuta za nyumba zao kulikosababishwa na milipuko iliyofanywa mgodini mara kwa mara wakati wakitekeleza shughuli zao za uchimbaji makaa ya mawe.

"Kiukweli milipuko ilikuwa mikubwa kiasi cha kufikia kuharibu nyumba zetu, nyumba nyingi zimepata nyufa kutokana za zoezi la ulipuaji. walilokuwa wakilifanya wenzetu wa mgodini na hatukujua tutafanya nini", alisema, Erick Marunda mkazi wa kijiji hicho.

Akiendelea kuzungumza Marunda alisema,wanawashukuru waandishi wa habari kwa sababu wana hakika kuwa kutokana na kufika kijijini hapo kushuhudia madhara ya milipuko katika nyumba zao na kuandika habari hizo ndiko kulisababisha serikali kuwaagiza wamiliki wa mgodi kupunguza kiwango cha ukubwa wa milipuko jambo ambalo mgodi ulifanya hivyo na nyumba hazikupata tena nyufa.

"Tunashukuru sana juhudi za wenzetu waandishi wa habari,hasa ndugu yetu,Albano Midelo maana wakati amekuja hapa tulimpeleka akashuhudia nyumba zilizopatwa na madhara hayo,na akazichapisha habari hizo katika vyombo mbalimbali vya Habari,serikali ikamuagiza mwenye mgodi,ambayo ni kampuni ya TANCOAL kupunguza kiwango cha ukubwa wa milipuko na kufunga vifaa maalumu vya kupima milipuko kabla haijafanyika,nao wamefanya hivyo",alieleza Marunda.



Aidha Marunda alisema,yeye ndiye aliyechaguliwa na kijiji kufanya kazi kwa ukaribu na wafanyakazi wa mgodi wakati wa kupima kiwango cha milipuko kabla ya kulipua na kuandika kumbukumbu hizo kila wanapopima ambapo alisema kazi hiyo alianza kuifanya rasmi mwezi Agosti mwaka 2016 mara baada ya kupata semina elekezi kutoka mgodini.

Afisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Joseph Ghahi alimthibitishia mwandishi wa habari hizi kuhusu kukoma kuendelea kutokea kwa nyufa katika nyumba za wakazi wa kijijini hapo zilizokuwa zikisababishwa na milipuko iliyofanywa na mgodi.

"Milipuko inayofanyika saizi haina madhara,tumemteua kijana mmoja kwa ajili ya kushirikiana na wenzetu wa mgodini wakati wa kupima ukubwa wa milipuko kabla haijafanyika,na kwa sababu kuna kiwango ambacho kitaalamu wameambiwa na serikali kuwa mlipuko wowote usizidi kiwango hicho kwa hiyo huyo kijana kazi yake kubwa ni kuhakikisha anasoma kupitia vifaa maalumu vinavyotumika kupima kuwa kiwango kisizidi kile kinachokubalika kitaalamu",alisema,Afisa Mtendaji huyo.

Pamoja na hayo, Afisa mtendaji huyo alisema ana amini kazi iliyofanywa na mwandishi wa habari Midelo,ambaye alifika kijijini hapo mara kadhaa mwaka 2016 na kufanya uchunguzi juu ya masuala mbalimbali,ikiwemo kufuatilia madhara wayapatayo wananchi wa maeneo jirani na mgodi huo,ndio iliyoleta matunda na kusababisha kufanyika kwa hatua za kudhibiti milipuko isiendelee kuathiri nyumba za wananchi.

Alipoulizwa juu ya hatua zilizochukuliwa na serikali kuwasaidia wananchi ambao nyumba zao ziliathirika kwa milipuko hiyo awali,alisema tayari waliwatangazia wananchi wote waliopatwa na kadhia hiyo kufika ofisini kwake ili kujiandikisha na kuangalia utaratibu wa kuwasaidia lakini wachache tu ndio waliokwisha tekeleza agizo hilo.

Pia Afisa huyo alisema jambo lingine ambalo waandishi walilifuatilia na kuliandika akiwemo Midelo ni pamoja na madhara ya kiafya yanayodhaniwa kusababishwa na uwepo wa makaa ya mawe hususani katika vyanzo vya maji wanayotumia wananchi hao, nayo tayari yameanza kupatiwa ufumbuzi ikiwemo wamiliki wa mgodi huo kukubali kusaidia kujenga mradi wa maji toka kijiji jirani na kuyaleta kijijini hapo kwa matumizi ya wananchi.

"Vyanzo vilivyopo vya maji vinasadikika kuwa na kemikali hatari kutokana na makaa ya mawe, hakuna vyanzo mbadala mpaka sasa,ingawa tayari kuna mpango wa kuleta maji kutoka kijiji jirani na wenzetu wa mgodi wapo tayari kusaidia katika hilo',alisema.

Akizungumzia huduma za kijamii zinazotekelezwa na kampuni inayomiliki mgodi huo,alisema wanashiriki vyema katika kusaidia hususani kwenye afya na elimu, ambapo alisema katika elimu kwa mwaka 2016 walichangia madawati 80 na kujenga choo cha matundu 6 kwa shule ya msingi iliyopo kijijini hapo na kwenye afya walitoa bati 49 zilizotumika kuezekea nyumba ya daktari wa zahanati ya kijiji hicho.

"Kwa kweli uhusiano kati yetu na mgodi sio mbaya,wanasaidia kwa kiasi fulani masuala ya kijamii ya kijiji hiki na pia wana mpango wa kujenga ofisi ya kijiji", alisema Mtendaji huyo huku akiongeza kuwa "Kitu pekee muhimu cha kwanza ambacho nikiambiwa niombe kwa serikali au wadau ili tupatiwe kabla ya vingine ni, maji safi na salama".

Licha ya madini ya makaa ya mawe kulalamikiwa kuchafua mazingira sehemu nyingi duniani lakini utafiti umebaini kuwa umeme unaotokana na madini hayo ndio unaotegemewa zaidi na mataifa mengi yaliyoendelea duniani.

Kwa mujibu wa habari iliyochapishwa katika tovuti ya Gazeti la Habari Leo, tarehe 19 Oktoba 2016, yenye kichwa cha habari; Makaa ya mawe ya Tanzania bora zaidi duniani; Matokeo ya utafiti uliofanyika kuanzia mwaka 2008 ulionesha kuwa ubora wa makaa ya mawe yanayopatikana katika mgodi wa Ngaka, haufanani na madini ya makaa ya mawe yanayochimbwa katika nchi yoyote duniani.

Pia Utafiti huo ulibaini kuwa mgodi huo unakadiriwa kuwa na zaidi ya tani milioni 400 za makaa ya mawe. Kiasi hicho, kwa mujibu wa wataalamu waliofanya utafiti, kinaweza kuchimbwa kwa kipindi cha zaidi ya miaka 40.

Utafiti wa madini hayo ulifanyika kwa kuangalia wingi wa madini ya makaa wa mawe, unene wa mwamba na ubora wa makaa hayo. Utafiti umebaini kuwa kijiji cha Ntunduwaro kipo juu ya mwamba bora wa madini ya makaa ya mawe ambayo yamesambaa pia na maeneo mengine ya kata ya Ruanda.

Kijiji cha Ntunduwaro kipo katika kata ya Ruanda wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma,kina vitongoji vitatu na jumla ya wakazi katika kijiji hicho ni 2400.

Mwandishi wa kujitegemea, Albano Midelo, kati ya Julai na Oktoba mwaka 2016 kwa nyakati tofauti alifanya utafiti juu ya masuala mbalimbali katika maeneo yanayozunguka mgodi wa Ngaka,hasa kijiji cha Ntunduwaro na kuchapisha habari kadhaa zikiwemo za madhara wayapatayo wakazi wa jirani na mgodi huo,kama nyumba zaidi ya 200 kupata nyufa kutokana na milipuko na athari za kiafya zitokanazo na uchafuzi wa mazingira.

Scanned by CamScanner

Sada Hamadi: TASAF imeniondoa kwenye umaskini

Na Greyson Mgoi, Songea

SADA Hamadi (38), mkazi wa Mtaa wa Mabatini Kata ya Misufini katika Manispaa ya Songea, Mkoani Ruvuma anasema, Serikali kupitia TASAF imemsaidia sana kumkwamua katika lindi la umaskini lilikokuwa likimkabili na kumfanya kuishi maisha magumu yeye na familia yake.

Anasema kabla hajaingizwa katika mpango wa kaya maskini zinazosaidiwa fedha na serikali kujikwamua kimaisha kupitia TASAF, maisha yake yalikuwa magumu,alifanya kazi ngumu ili kujipatia kipato kidogo kuweza kumudu maisha ya kila siku.

Aidha anasema, mara baada ya kuingizwa katika mpango huo mwaka jana, alianza kufanya biashara ya kupika vitumbua vya mchele na kuuza, ambapo alipolipwa fedha ya kwanza alianza na mtaji wa kilo 2 za mchele lakini sasa mtaji wake umekuwa na kumfanya kuwa ananunua kilo 25 za mchele kwa mara moja na kuandaa vitumbua vya kutosha kwa ajili ya kuuza.

Mama huyo ambaye anakiri wazi kuwa kupitia mradi huo wa vitumbua ameweza kumsomesha mtoto wake, na kumnunulia mahitaji muhimu ambapo kwa sasa yupo kidato cha nne huko Sekondari ya Bombambili katika Manispaa ya Songea.

Pia anatoa wito kwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iendelee kuwasaidia watu masikini ili kuwakwamua katika lindi hilo.

"Mimi nawashukuru sana serikali,naomba wasituache waendelee kutusaidia ili tuweze kuwalea pia watoto tuliotelekezewa na waume zetu,kiukweli pesa haitoshi ila inatusaidia kupunguza baadhi ya mambo yanayotukabili",anasema mama huyo.

Hivi karibuni, akiwa kwenye ofisi za Mtaa wa Mabatini pamoja na watu wa kaya nyingine maskini za mtaa huo, wakisubiri kuja kupokea fedha zao za TASAF, awamu ya 3, Sada anasema anaamini bila kuwa kwenye mpango huo,maisha yake yangekuwa magumu sana na pengine angepata athari za kiafya kutokana na kufanya kazi ngumu mara kwa mara ili kujipatia kipato.

Naye, Mariam Rajabu mkazi wa mtaa huohuo wa Mabatini anakiri pia kupata maendeleo mazuri kupitia TASAF, ambapo ameweza kuwasomesha watoto wake watatu,wenye umri wa miaka 16,na 12 na wa mwisho mwenye miaka mitatu. Mbali na kusomesha watoto anasema kupitia fedha ya TASAF ameanzisha mradi wa kuuza mboga za majani na anapata kipato cha kumtosha kuendesha familia yake.

"Kabla ya kuanza kupewa fedha hii ya TASAF niliikuwa na maisha magumu,sikuweza kuwa hata na mtaji wa kuweza kununua mboga za majani kwa bei ya jumla na kuuza kwa rejareja mitaani jambo ambalo sahizi linaninufaisha sana",anasema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mabatini, Endrew Chilwa amemwambia mwandishi wa makala haya kuwa fedha ya TASAF imesaidia sana kupunguza idadi ya kaya maskini katika mtaa wake kwani wengi wakipata fedha hiyo wanaanza kujishughulisha na biashara ndogo ndogo baadae mtaji unakuwa mkubwa wanaweza kujimudu kimaisha.

Anasema katika mtaa wake kupitia kamati ya TASAF waliyoiunda wamekuwa wakigawana majukumu na kuzunguka kwatembelea wanufaika, ili kuona wanatumiaje fedha hizo ambapo alisema wengi wanatumia kuwahudumia watoto wao wanaosoma,na kuanzisha miradi midogomidogo ili kukuza mtaji na fedha hiyo iwasaidie baadae.

Anasema katika mtaa wake kwa sasa jumla ya kaya 21 zinanufaika na TASAF ambapo anasema kabla ya zoezi la uhakiki kufanyika mwishoni mwa mwaka jana,jumla ya kaya 49 zilikuwa zinanufaika.

"Sikujua vigezo gani hasa vilitumika kuwatoa wanufaika wengine kwani kwa jinsi nilivyo ona mimi kuna wengi waliotolewa baada ya zoezi la uhakiki walikuwa wanatakiwa kundelea kusaidiwa kutokana na hali zao duni za kimaisha",anasema.

Aidha anasema katika mtaa wake kuna wazee maskini wengi ambao wanatakiwa kuendelea kusaidiwa, lakini anashangaa wengine walitolewa kwenye kundi hilo na wengine hawakuandikishwa kabisa licha ya kuwa jamii inawaona kuwa wanatakiwa kusaidiwa na serikali ili kumudu maisha.

Ofisa mtendaji wa Mtaa wa Mabatini, Getrude Hiluka anasema kaya zinazonufaika na TASAF sasa ndizo zinazostahili kwani ndizo zilizochaguliwa baada ya zoezi la uhakiki mwaka jana mwishoni,ingawa anakiri kuwepo kwa kaya nyingine nyingi zinazostahili pia, lakini ziliachwa baada ya uhakiki.

"Baada ya uhakiki kaya nyingine ziliachwa na tulipata malalamiko kutoka kwa watu, sasa naiomba serikali ikiweza irudi tena katika mtaa wetu kuja kuhakiki kaya nyingine ili kuwaingiza kwenye mpango wa kaya maskini na kuanza kuwasaidia,"anasema.

Taarifa ya Afisa Habari wa Manispaa ya Songea, Albano Midelo inasema kaya maskini 260 kati ya kaya 2692 zilizoenguliwa katika mpango wa kunusuru kaya maskini katika Manispaa ya Songea zimeandika barua TASAF makao makuu kukata rufaa za kuenguliwa kwao.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa kaya 2692 kati ya kaya 7,695 zilizokuwa zinanufaika na ruzuku hiyo zimeenguliwa baada ya uhakiki wa nyumba kwa nyumba kufanyika mwaka jana,ambapo baada ya uhakiki huo kaya zenye sifa zimebakia 5003.

Taarifa ya Midelo Inafafanua kuwa kati ya kaya zilizoenguliwa ilibainika kuwa kaya 1599 katika Manispaa hiyo sio masikini,kaya 342 walihama katika maeneo yao,kaya 110 walifariki,kaya 417 zilibainika kuwa ni hewa na kaya 144 hazikuwepo kwenye uhakiki huo.

Pia inaeleza mara baada ya kaya zilizoenguliwa kupata barua za kuondolewa,yametokea malalamiko mengi katika kaya hizo hali ambayo imesababisha Manispaa ya Songea kupita katika mitaa ya walioenguliwa na kutoa elimu ya kukata rufaa kwa wale wanaodhani wameonewa na wale ambao wametolewa kihalali kuanza kulipa fedha walizokwisha pewa.

Aidha Taarifa imeeleza kuwa, Kaimu Mratibu wa TASAF Manispaa ya Songea, Mensa Ngerangera amekuwa akitoa elimu kwa nyakati tofauti katika mitaa ya Ruhuwiko Kanisani, Ruhuwiko Shuleni, Namanditi, Lilambo A na Sinai na kuwataka wale ambao wametolewa kwa kukosa sifa waanze kulipa kama ilivyoelekezwa kwenye barua.

Katika kutoa elimu huko Ngerangera,Amesema kaya maskini ambazo zimeondolewa kimakosa katika mpango huo zinatakiwa kukata rufaa kwa kuandika barua TASAF makao makuu na kwamba ambaye hataandika barua ya rufaa atatakiwa kuanza kulipa deni hilo.

Ngerangera amezitaja sifa za kaya zinazotakiwa kukata rufaa kuwa ni zile ambazo zinakula mlo mmoja kwa siku,kaya isiwe na zaidi ya heka moja,asiwe mfanyabiashara,mstaafu wala mwenye mtoto au ndugu wa karibu ambaye ni mtumishi wa umma na asiwe mwenye nyumba bora iliyoezekwa kwa bati na kupiga sakafu.

Sambamba na hayo taarifa inabainisha kuwa, Utafiti uliofanyika katika baadhi ya mitaa ambayo wameenguliwa waliokuwa wanufaika, umebaini kuwa kuna kaya ambazo zimeondolewa kwa makosa kwa kuwa zina sifa ya kaya maskini,ingawa pia zipo kaya ambazo hazina sifa ya kaya masikini hivyo zinastahili kuenguliwa.

Pia Taarifa hiyo inaeleza kuwa,Ngerangera amesema Novemba-Desemba 2016,kiasi cha Tsh.milioni 277 zilitolewa katika kaya masikini zenye sifa zilizopo katika mitaa 53 ya Manispaa ya Songea ambapo pia Januari-Februari 2017 Manispaa hiyo itatoa kiasi cha Tsh.milioni 256 kwa kaya maskini zenye sifa.

Hivi karibuni Ofisi ya TASAF Manispaa ya Songea imefanya malipo na kutoa elimu katika kaya maskini za mitaa kadhaa ikiwemo mitaa ya; Msafiri, Asiakovu, Pacha nne, Mabatini, Mfaranyaki, Chandarua, Oysterbay, Tanga, Ruvuma juu na Nonganonga.

(Greyson Mgoi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti hili, anapatikana kwa Simu namba: 0676041181 au kwa barua pepe: greysonmgoi@gmail.com)

Scanned by CamScanner

Misitu ya miombo inavyosaidia uchumi endelevu Ruvuma

Kitalu cha miti ya biashara wilayani Mbinga.

> Mradi huo wa panda miti kibiashara unatarajia kuanzisha kiwanda cha kupasua mbao katika eneo la Madaba wilayani Songea ili kuboresha karakana ya kutengenezea maboti ya kisasa katika mji wa Mbambabay wilaya ya Nyasa.

Na Albano Midelo

DK Ali Mohamed Shein alipokuwa Makamu wa Rais (sasa Rais wa Zanzibar), alifanya ziara katika Mkoa wa Ruvuma na moja ya mambo yaliyomvutia ni misitu minene ya asili ambayo ipo katika mkoa wa Ruvuma.

Anasema alianza kuiona misitu hiyo akiwa angani na kwamba ilimvutia sana kwa sababu mkoa ulionekana kuwa na rangi ya kijani katika maeneo mengi, tofauti na mikoa mingine ambayo inakabiliwa na uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na ukataji miti hovyo, hali inayasababisha ukame.

Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa nchini inayopatikana ukanda wa kusini ikiwa imetawaliwa na miti ya asili jamii ya miombo (Miombo woodland).

Ukubwa wa misitu mizito minene iliyopo katika mkoa wa Ruvuma inachangia kupunguza hewa ukaa (CO_2). Halikadhalika misitu hiyo ina umuhimu katika mchakato wa (Carbon sink) kwa maana ya hupokea mvua za kutosha kwa msimu mmoja tu kwa mwaka.

Miongoni mwa vivutio adimu ni uoto wa asili ya jamii ya miombo ambao haujaharibiwa umekuwa kivutio adimu kwa wanyamapori, ndege, wadudu na viumbe wengine waliopo katika mapori ya akiba ya Selous, Liparamba na Gesimasoa.

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya eneo la kilometa za mraba 67,550, kati ya hizo kilometa 63,968 ni ardhi na kilometa 3,582 ni maji yanayojumuisha ziwa Nyasa, mito na mabwawa.

Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe analitaja eneo la misitu ya asili ya miombo kuwa ni kilometa 41,567, sawa na asilimia 65 ya eneo lote la ardhi na kwamba misitu ya hifadhi ya serikali kuu ina eneo la kilometa 6,958, Halmashauri zina kilometa 170 na hifadhi za vijiji zina eneo la hekta 116,490.31.

Anabainisha kuwa jumla ya misitu yenye eneo la kilometa za mraba 41,507 zilizopo katika mkoa wa Ruvuma zinahusisha msitu wa Mhuwesi wenye ukubwa wa hekta 170,000, Mwambesi hekta 104,052, Sasawala hekta 39,424, Matogoro A hekta 32,900 na Matogoro B hekta 7,128.

Usimamizi shirikishi wa utunzaji misitu ya hifadhi umekuwepo karibu kila wilaya za mkoa wa Ruvuma ambapo takwimu za hifadhi za vijiji mkoani Ruvuma, zinaonesha kuwa katika wilaya ya Mbinga kuna vijiji 28 vyenye misitu yenye hekta 30,278.

Kwa mujibu wa Ofisa Maliasili huyo wa Mkoa wa Ruvuma, katika wilaya ya Songea kuna vijiji nane vyenye misitu nane yenye ukubwa wa hekta 34,228.21.

Anafafanua kwamba wilaya ya Namtumbo yenye vijiji 11 ina vijiji sita vyenye hekta 56,041.5, wilaya ya Tunduru ina vijiji viwili vyenye misitu miwili yenye hekta 26,578 ambapo katika mkoa wa Ruvuma kuna jumla ya vijiji 49 vyenye misitu 20 yenye jumla ya hekta 147,125.71.

Akizungumzia upandaji wa miti katika Mkoa wa Ruvuma, Challe anasema mwaka huu jumla ya miti 1,679,727 ya biashara imepandwa na miche ya miti 4,050,000 imeoteshwa kwa ajili ya kupandwa katika msimu ujao wa mvua wa mwaka 2018.

Anaongeza kuwa kupitia mradi wa panda miti kibiashara kwa kushirikiana na Wakala wa Mbegu Tanzania wameotesha miche 2,400,000 ambayo itasambazwa kwa wananchi binafsi kupitia vikundi vya upandaji miti.

"Mradi huo wa panda miti kibiashara unatarajia kuanzisha kiwanda cha kupasua mbao katika eneo la Madaba wilayani Songea ili kuboresha karakana ya kutengenezea maboti ya kisasa katika mji wa Mbambabay wilaya ya Nyasa," anasisitiza Challe.

Anabainisha kuwa misitu iliyopo katika mkoa wa Ruvuma pia inatumika katika ufungaji wa nyuki ambao unaonekana kuwa na nguvu hivi sasa baada ya watu kuonesha kuwa na mwamko wa kuhifadhi rasilimali misitu kwa njia ya ufugaji wa nyuki.

Challe anasema ufugaji nyuki umesaidia kuongeza pato katika familia na vikundi mbalimbali vinajihusisha na ufugaji katika mkoa wa Ruvuma ambapo takwimu zinaonesha kuwa katika mkoa mzima kuna vikundi 272 vya ufugaji nyuki vyenye jumla ya mizinga 7966 ambavyo vimeweza kuzalisha asali jumla ya lita 39,830.

Licha ya Mkoa wa Ruvuma kuwa na neema ya misitu mingi, Ofisa Maliasili na Utalii huyo anazitaja changamoto zilizopo kuwa ni pamoja na uchomaji moto misitu unaosababishwa na shughuli za kibindamu, ikiwemo wakati wa uandaaji mashamba na uwindaji unaotumia moto, hali inayosababisha uharibifu wa mazingira na kuchangia mabadiliko ya tabianchi.

Changamoto nyingine anaitaja kuwa ni uvunaji haramu wa mazao ya misitu kwa ajili ya mahitaji ya mbao na nishati ya kuni au mkaa, na uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa ajili ya kilimo cha kuhamahama, ufugaji holela na makazi yasiyo rasmi.

Licha ya kuwepo changamoto katika misitu, Challe anazitaja changamoto zilizopo katika ufugaji wa nyuki kuwa ni uchomaji wa moto katika mapori wakati wa maandalizi ya mashamba hali inayosababisha nyuki kuhama.

Changamoto nyingine anasema ni ukataji wa miti usiokuwa endelevu kwa ajili ya upanuzi wa mashamba na mahitaji ya nishati ya kuni na mkaa, elimu ndogo juu ya ufugaji na uhaba wa fedha za kuwezesha kuwa na vikundi vingi kwa sababu ufugaji unahitaji fedha za kutosha wakati wa maandalizi.

Mikakati ambayo imechukuliwa katika kukabiliana na changamoto hizo, Challe anaitaja kuwa ni kuhimiza uhifadhi wa misitu shirikishi ili kutoa fursa kwa jamii kutunza rasilimali hizo na kutoa elimu kwa jamii namna ya ufugaji wa nyuki ulio endelevu.

Mikakati mingine anasema ni wa Wakala wa Misitu Tanzania, tawi la Songea wa kuanzisha kituo cha kuzalisha makundi ya nyuki kwenye hifadhi ya asili ya Ruhira iliyopo Manispaa ya Songea.

Sambaba na hilo, Challe anasema Chuo cha Maliasili cha Likuyuseka kilichopo wilayani Namtumbo kina mpango wa kuanzisha utafiti wa ufugaji wa nyuki katika ukanda wa kusini.

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili, mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com, simu 0784765917

Moja ya bustani za miti ya biashara wilayani Mbinga mkoani Ruvuma.

Scanned by CamScanner

Liparamba, pori la wanyama wanaohamia kutoka Msumbiji

Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe.



Maeneo ya hifadhi ya Liparamba yaliyovamiwa na wakazi kwa kujenga nyumba za kuishi.

Richard Bwire, Meneja pori la Akiba la Liparamba.

Inatoka Uk. 13

Mambo hayo anasema ni upungufu mkubwa wa eneo la misitu kutokana na kilimo cha kuhamahama, kilimo cha mazao ya msimu kilichoendeshwa na wakulima toka eneo la milimani kwenda ukanda wa chini ili kulima mahindi kwa ajili ya chakula.

Bwire anayataja mambo mengine muhimu yaliyogundulika kuwa ni pamoja na upungufu wa maeneo yaliohifadhiwa kwa ajili ya kulinda miti muhimu na yenye thamani kubwa kama mininga, mahogani na kupotea kwa kasi kwa mimea ya asili ambayo ilihitajika na kuendelea kuhitajika kwa ajili ya chakula, dawa na ulinzi wa viumbe asilia.

"Kutoweka na kupotea kabisa kwa wanyamapori na wadudu asilia ambao miaka ya nyuma walishi katika misitu ndiyo iliyosababisha halmashauri ya wilaya kupitia idara yake ya maliasili kuamua kuwa na maeneo ya misitu ya kutosha kama misitu ya akiba," anasema Bwire.

Kwa mujibu wa Bwire, maeneo hayo yahzuiliwa yasiharibiwe ili kulinda misitu, miti, wanyama, wadudu na viumbehai kwa kuwa ni maeneo ya vivutio vya asili na misitu minene inayovutia.

"Lengo lilikuwa ni kuwezesha wananchi kutembelea, kuona na kujifunza historia na sayansi ya viumbehai katika vivutio vya utalii, makazi ya wanyamapori na hifadhi ya maji na mazingira katika pori la Liparamba," anasema.

Kwa upande wake, Ofisa Maliasili wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe anasema pori hilo lina kiwango cha juu cha hifadhi ambacho kinatiliwa mkazo kisheria katika ulinzi, usimamizi, uendelezaji na matumizi ya busara ya mali hai ikiwemo misitu, samaki na wanyamapori.

Challe anabainisha kuwa kuhifadhiwa kwa eneo hilo kumejumuisha sekta nzima ya maendeleo ya mazingira, maliasili na utalii kwa gharama nafuu.

Anasema wanyama wanapotoka katika pori la Akiba la Selous wilayani Namtumbo wanapita hadi pori la Gesimasoa wilayani Songea na kuendelea hadi pori la Liparamba kisha wanaingia au kutoka nchini Msumbiji.

"Eneo hili ni kivutio kikubwa cha watalii na wakazi wa ndani ambao watavutiwa kuona msitu mzuri wa asili usioharibiwa sanjari na wanyama adimu wakiwemo chui, simba, palahala na tandala wakubwa. Pia kuna tembo na kumbukumbu zinaonesha kuwa tembo mwenye uzito mkubwa aliwahi kupatikana katika pori la Liparamba", anasisitiza Challe.

Hata hivyo, anasema msitu mnene wa asili na wenye mandhari ya kuvutia katika pori la Liparamba ni eneo muhimu la kuhamia wanyamapori kati ya nchi za Tanzania na na Msumbiji na ng'ambo ya mto Ruvuma kwa upande wa wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.

Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imelenga kutenga eneo hilo kama kielelezo cha ukanda wa viumbehai katika mazingira yao ya asili kwa kupunguza kasi ya mabadiliko makubwa yatokanayo na maendeleo na uharibifu wa binadamu na kuweka sehemu ya utafiti wa mazingira, elimu ya uchunguzi wa miti, wanyama na samaki.

Malengo mengine ni kulinda na kutumia kwa busara zao la malihai, njia ya uvunaji, kuendeleza utalii, kulinda vyanzo muhimu vya maji, milima ya kuvutia na sehemu za mila na utamaduni.

Licha ya pori hilo kupakana na nchi jirani ya Msumbiji, kwa upande wa kusini pori hilo linapakana na mto Ruvuma, mashariki kuna mito Lumeme, Lunyele na Goma la Mpepo ambao ni moja kati ya milima mirefu katika wilaya ya Nyasa.

Pori hilo linapakana pia na vijiji saba vya Liparamba, Ndondo, Mipotopoto, Mitomoni, Mseto, Mtua na Mpepai.

Hata hivyo, changamoto kubwa ni kwamba wakazi wa vijiji hivyo hawana mifugo inayokidhi mahitaji ya kitoweo hivyo wanategemea kupata kitoweo kinachowapa protini kutokana na zao la wanyama pori.

Hali hiyo inaelezwa kwamba ndiyo inayosababisha baadhi yao kuendesha uwindaji haramu kwa kutumia silaha zisizoruhusiwa kisheria kama magobore na uwindaji wa kuchoma moto.

Meneja wa Pori hilo anawataja wanyamapori wanaopatikana katika pori hilo kuwa ni palahala, tandala wakubwa, ndogoro, viboko, pofu, tohekusi, mbawala, mbuzi mawe, ngolombwe, chui, simba, fisimaji, nyanimanjano, tumbili, nguruwe na ngiri.

Wanyama wengine ni tembo, pundamilia, nyati, nyumbu na mbwamwitu.

Anasema zipo taarifa kwamba baadhi ya wanyama hao wanahama kutoka hifadhi ya Niassa nchini Msumbiji na kuingia Tanzania kwa wingi.

Anasema lengo la serikali ni kuhakikisha rasilimali zote zinaendelea kulindwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kuwa endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho hivyo anasisitiza kwamba wamekusidia kuondoa migongano yote na wananchi wanaozunguka hifadhi.

"Baadhi ya wananchi wamevamia hifadhi kwa makusudi, tunatekeleza maagizo ya Waziri Mkuu kuwaondoa wananchi wote waliovamia hifadhi wakiwemo wafugaji ambao wanavamia hifadhi katika mkoa wa Ruvuma," anasema Bwire.

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili. Mawasiliano yake ni HYPERLINK "mailto:albano.midelo@gmail.com. Simu" albano.midelo@gmail.com. Simu 0784765917.

> "Wakazi wa vijiji hawa mifugo ili kupata kitoweo, hivyo wanategem wanyama pori."

Scanned by CamScanner

Milima miwili na visiwa viwili ziwa Nyasa kuwa hifadhi za wanyamapori



Hoteli ya kisasa ambayo imejengwa katika hifadhi ya Mbamba iliyopo mjini Mbambabay.

Na Albano Midelo

MILANGO ya utalii mwambao mwa ziwa Nyasa mkoani Ruvuma inaendelea kufunguka ambapo sasa serikali inataraji kuanzisha bustani ya wanyamapori katika milima miwili na visiwa viwili vilivyopo wilayani Nyasa mkoani Ruvuma.

Ofisa wa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe anasema mchakato wa kuendeleza Hifadhi ya mlima Mbamba na hifadhi ya mlima Tumbi iliyopo kijiji cha Ndengere ni maagizo ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Profesa Jumanne Maghembe ambaye aliagiza Nyasa iwe kitovu cha utalii kusini.

Waziri Maghembe alipofanya ziara mwambao mwa Ziwa Nyasa, aliagiza vivutio vyote vilivyopo katika mwambao huo kuibuliwa na kuendelezwa, ili watalii wa ndani na nje waanze kufika kusini badala ya kwenda kaskazini pekee.

Kutokana na hali hiyo, Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma anasema tayari mchakato wa kuendeleza Mbamba Hill iliyopo mjini Mbambabay kuwa hifadhi ya wanyama unaendelea vizuri na kwamba tayari bajeti imepitishwa.

"Tumeshapima eneo lote la Mbamba Hill, lina ukubwa wa hekta 420. Ndani ya hifadhi hiyo kuna wanyama kama nyani, nyoka, pimbi, chui na ndege wa aina mbalimbali," anasema Challe.

Challe anabainisha kuwa hifadhi hiyo imeunganishwa na kisiwa kinachoitwa Zambia ambacho kipo meta 300 kutoka ufukweni mwa Ziwa Nyasa na kwamba kisiwa hicho kina utajiri wa aina mbalimbali za samaki wa mapambo ambao ni kivutio cha watalii.

Anasema bajeti ya kujenga uzio kuzunguka Mbambabay Hill imepitishwa na kwamba ujenzi unataraja kuanza wakati wowote fedha zitakapoletwa na kwamba baada ya ujenzi wa uzio kukamilika wanyamapori wa aina mbalimbali wanataraja kuongezwa.

"Uzio utawekwa sehemu zote kuzunguka hifadhi hiyo isipokuwa sehemu ya kuingia ziwa Nyasa ambayo itaungana na kisiwa cha Zambia haitawekewa uzio, hivyo wanyama watakuwa huru kuzunguka hifadhi yote hadi kuingia kunywa maji ziwa Nyasa," anasema Challe.

Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) katika Mkoa wa Ruvuma, Richard Bwire amethibitisha TAWA kuhusika na kuongeza wanyama katika Mbamba Hill ili kuvutia watalii wengi watakakokuwa wanatembelea mwambao mwa Ziwa Nyasa.

Anawataja wanyama ambao wanataraja kuongezwa katika hifadhi hiyo kuwa ni swala, fisimaji, mbuzi mawe, digidigi, mbawala na kwamba wanyama watakaongezwa ni wale ambao wanaweza kuishi katika mazingira ya hifadhi hiyo ambayo imeunganaa na Ziwa Nyasa.

Anasema katika mlima huo pia serikali imetoa eneo kwa wawekezaji wa Kanisa Katoliki ambao ni watawa wa Mtakatifu Vincent , Jimbo la Mbinga ambao tayari wamejenga hoteli ya kitalii yenye vyumba 35 ambayo imeanza kutumika na wageni wa ndani na nje ya nchi.

Akizungumza katika hoteli hiyo iliyopo ufukweni mwa ziwa Nyasa, Mshauri na Mwakilishi wa Balozi wa Finland nchini Tanzania, Kari Leppanen anasema amesharngazwa na vivutio vya kipekee na adimu ambavyo havipatikani sehemu nyingine yoyote duniani vilivyopo katika ziwa hilo.

Anasisitiza kuwa iwapo vivutio hivyo vitaendelezwa vitafungua fursa za uwekezaji na utalii kwa wananchi wa eneo hilo na mkoa wa Ruvuma kwa ujumla wake hali ambayo inaweza kutoa ajira kwa vijana na kupunguza umaskini.

Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe anaseema baada ya kukamilisha mradi wa hifadhi wa Mbambabay uliopo mjini Mbambabay ambayo inaungana na kisiwa cha Zambia, mradi utakaofuata ni mlima wa hifadhi wa Tumbi.

Challe anasema mlima huo uliopo kijiji cha Ndengere utaunganishwa na kisiwa cha Lundo chenye ukubwa wa kilometa za mraba 20 hivyo kuwa na hifadhi mbili ambazo zimeunganishwa na visiwa viwili.

Awali visiwa viwili vya Zambia na Lundo vilimilikishwa kinyume cha sheria kwa mwekezaji mmoja kutoka nje ya nchi hali iliyosababisha kuchelewesha maendeleo katika sekta ya utalii ambayo hivi sasa inaongoza kwa kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Kutokana na umuhimu wa visiwa hivyo katika sekta ya utalii, Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa imemnyang'anya visiwa hivyo mwekezaji kutoka nje ya nchi ambaye alinunua kinyume cha sheria miaka mingi iliyopita.

Kisiwa cha Zambia kipo Mbambabay makao makuu ya Wilaya ya Nyasa na kisiwa cha Lundo kipo Kata ya Lipingo, visiwa vyote viwili viliuzwa kinyume cha sheria kwa mwekezaji kutoka nje ya nchi kati ya mwaka 2004 na 2005.

Cathbert Ngwata, diwani wa kata ya Lipingo yenye vijiji vitatu ambavyo ni Ngindo, Lundo na Lipingo anasema kisiwa cha Lundo kina maliasili za kuvutia zikiwemo wanyama, ndege, wadudu na mimea ya aina mbalimbali ambayo ni kivutio kwa yeyote ambaye anatembelea kisiwa hicho.

Baadhi ya wananchi wameipongeza hatua ya uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kumnyang'anya visiwa hivyo mwekezaji na kwamba tangu awali walikuwa hawaungi mkono hatua ya viongozi wao wa vijiji kumuuzia mgeni kisiwa hicho, kwa kuwa kina manufaa makubwa kwa wavuvi ambao wamekuwa wanakitumia kupumzika na kujihifadhi ziwa linapokuwa na dhoruba kali.

Viktor Komba, mkazi wa Nyasa anasema awali wavuvi walikuwa hawaruhusiwi kufanya uvuvi mita 100 kila upande kuzunguka kisiwa cha Lundo, hali ambayo ilikuwa ni kero kubwa kwa wavuvi ambao walikuwa wanapenda kupumzika inapokea dhoruba kali katika ziwa Nyasa.

Ofisa Maliasili wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Bugingo Bugingo anasema sheria za nchi haziruhusu mtu binafsi kumjilikishwa fukwe, milima au kisiwa na kusisitiza kuwa ni kosa kubwa kummilikishwa mtu binafsi na hasa tala wa kigeni eneo ambalo linatambulika kisheria kuwa ni eneo la hifadhi.

"Kulingana na sheria za Tanzania kisiwa chochote kilichopo ndani ya bahari au ziwa hairuhusiwi kummilikisha mtu yeyote isipokuwa sheria inaruhusu kuwekeza," anasisitiza mtaalamu huyo wa maliasili katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa.

Dk Ruggemeleza Nshala ni Mwanasheria na Mkurugenzi wa Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira Tanzania (LEAT) anabainisha kuwa kisheria mtu binafsi anaruhusiwa kumiliki ardhi lakini haruhusiwi kumiliki visiwa vidogo, fukwe, vilele vya milima, kingo za mito,maeneo yote oevu au chepechepe na nja za asili za wanyamapori.

Hata hivyo, anasema watu ambao tayari wametwaa fukwe na visiwa na kuwazuia watu wengine kuvisogelea au kuwalipisha pesa wanakiuka kanuni ya msingi za matumizi ya rasilimali za pamoja na kwamba ni jukumu la kila mwananchi kupinga kubinafsishwa kwa visiwa au fukwe ambazo ni zawadi tuliopewa na Mungu.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa, Stella Manyanya ambaye pia ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, anatoa mwito kwa wadau wote wa sekta ya utalii Mkoa wa Ruvuma kuhakikisha kuwa wanayalinda maeneo yote yaliyohifadhiwa hasa mwambao mwa Ziwa Nyasa ambako kuna rasilimali muhimu zinazoweza kufungua sekta ya utalii.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Isabela Chilumba anasema milango ya utalii mwambao mwa Ziwa Nyasa tayari imeanza kufunguka ambapo hivi sasa watalii kutoka nchi mbalimbali ikiwemo barani Ulaya wanafika kutembelea wilaya hiyo yenye vivutio adimu vya utalii.

Anatoa rai kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwenda kuwekeza katika Wilaya ya Nyasa ambayo ina aina mbalimbali za utalii ikiwemo ziwa Nyasa, visiwa, fukwe, samaki wa mapambo, mawe ya kihistoria,ngoma za asili na vyakula vya asili.

Ziwa Nyasa linapita katika wilaya za Nyasa mkoani Ruvuma,wilaya ya Ludewa mkoani Njombe na Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya. Ziwa hilo limezungukwa na nchi tatu ambazo ni Tanzania, Malawi na Msumbiji. Kina cha ziwa hilo ni karibu kilometa 1000.



Mshauri wa Balozi wa Finland, Kari Leppanen alipotembelea hifadhi ya Mlima Mbamba ambayo pia imejengwa hoteli ya kitalii ya St. Vincent.

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili, mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com, simu 0784765917.

Hifadhi ya mlima Mbamba ambayo imeunganishwa na kisiwa cha Zambia kinachoonekana kwa mbali.

Tanzania na China walivyo marafiki wa dhati

Inatoka Uk. 13

muhimu ni ule Mkataba wa Urafiki uliotiwa saini mwaka 1965 ambao ndio ulikuwa dira na msingi wa uhusiano baina ya nchi hizo. Baada ya mkataba huo, mikataba mingine zaidi ilifuatia katika nyanja za uchumi, biashara, afya, elimu na utamaduni, ulinzi na usalama.

Katika siasa za kimataifa, wakati China inapigania kurejeshwa katika Umoja wa Mataifa mwaka 1971, katika kikao cha 26 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Tanzania ilikuwa rafiki na mstari wa mbele katika kunga mkono jitihada hizo.

Azimio nambari 2758 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilieleza kuitambua Jamhuri ya Watu wa China kuwa mwakilishi halali wa China na kuwafukuza wawakilishi wa Chiang Kai-Shek katika nafasi waliyoichukua kinyume na sheria.

Inasemekana taarifa za kukubalia wa China kurejeshewa kiti chake katika Umoja wa Mataifa zilipotolewa, Balozi wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa wakati huo Balozi Salim Ahmed Salim alishindwa kujizuia na kuanza kucheza katika ukumbi wa Baraza la Kuu.

Safari ya miaka 57 ya uhusiano kati ya China na Tanzania imeshuhudia kuimarika kwa kiwango cha uhusiano na ushirikiano kati ya nchi hizi, hii imetokana na dira na dhamira ya Serikali na wananchi wa nchi hizi kutambua umuhimu wa uhusiano katika uhai wao na nchi zao.

Ni ukweli kuwa, wakati nchi hizo zinaanzisha uhusiano wao, China haikuwa na uchumi mkubwa wala maendeleo makubwa lakini viongozi na wananchi wa nchi hiyo walijuskua fahari kusaidia marafiki zake.

China iliweza kutoa msaada ya miradi mikubwa kwa Tanzania ili kujenga uchumi wake. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na uanzishwaji wa viwanda kama vile: Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, Kiwanda cha Viatu Zanzibar.

Kama alivyoeleza Balozi Dk Lu wakati akiagana na waandishi wa habari anasema katika miaka ya hivi karibuni, maeneo yote ya ushirikiano kati ya nchi yake na Tanzania yameongezeka sana. Mathalani, ukiangalia elimu, tangu miaka ya 1960 vijana wa kitanzania wamekuwa wakienda nchini China kwa mafunzo mbalimbali ambapo idadi yao imekuwa ikiongezeka kutoka vijana 80 mwaka 2003 hadi kufikia 700 mwaka huu wakichukua mafunzo mbalimbali.

Kwa upande wa sekta ya afya, timu za madaktari wa Kichina zimekuwa zikija nchini tangu mwaka 1964 na zaidi mwaka 1965 China na Tanzania zilitia saini makubaliano ambayo yamewezesha madaktari wa China kuja nchini. Hadi mwaka 2005 madaktari 990 kwa mzungutko 18 walikuja Tanzania kufanya kazi katika sekta ya afya.

Huko Zanzibar, mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika sekta ya afya hauwezi kupimika kwa kuwa tangu Mapinduzi, Zanzibar imekuwa ikifaidika na uhusiano wake na China kwa kupatiwa madaktari na watumishi wengine wa afya lakini zaidi hivi karibuni imeenga hospitali ya kisasa huko Pemba ambayo imenyanyua kiwango cha upatikanaji na utoaji wa huduma za afya kisiwani Pemba.

Agosti 28, 2015 wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa hospitali hiyo ambayo imegharimu Sh billioni 26, Dk Shein alisema, "hawa (Wachina) ni marafiki zetu wa kweli kwani akuofaaye kwa dhiki ndie rafiki."

Wakati wa uzinduzi rasmi wa hospitali hiyo ulofanyika Novemba 26, 2016, Dk Shein aliwarleza wananchi wa Zanzibar kuwa: "Watu wa China na 'marafiki wa dhati' Wametuunga mkono kujenga nchi yetu mara baada ya Mapinduzi katika sekta za mundombinu, maji, kilimo, viwanda na kwa upande wa afya wameituwa wakileta timu za watataalamu na mabingwa wa utabibu sasa na timu ya 31."

Uhusiano kati ya nchi hizo wakati wote umekuwa ukizingatia mabadiliko na changamoto zinazoambatana na mabadiliko hayo, lengo likiwa na kuhakikisha mabadiliko haya hayatoi nafasi ya kuzorotesha uhusiano wao.

Inaelezwa kuwa bushara na uwekezaji umeongezeka baina ya nchi hiyo ambapo hadi sasa zaidi ya makampuni ya China 800 yameweketza na kufanya kazi Tanzania. Inakadiriwa kuwa ajira zaidi ya 200,000 zilizalishwa kwa apli ya Watanzania na zaidi ya Watanzania 350,000 wamekuwa wakishirikiana na kazi zinazohusu biashara kati ya China na Tanzania.

Tanzania na China zimekuwa zikiendesha miradi ya pamoja kama vile Shirika la Meli ya Tanzania na China (SINOTASHIP) na Kiwanda cha Nguo cha Urafiki ambapo tangu mwaka 1996 kiwanda kinamilikiwa kwa pamoja kati ya nchi hizo.

Ni dhahiri kuwa maendeleo ya haraka ya sayansi na teknolojia ikiwemo ongezeko kwa kasi ya upatumizi ya teknolojia ya habari imeleta Mapinduzi makubwa katika uhusiano kati ya nchi na nchi hata katika ngazi ya mtu na mtu.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na aliyekuwa Balozi wa China nchini, Dk Lu Youqing wakikagua miradi.

Pamoja na maendeleo na changamoto iliyokuja nazo teknolojia hii, pia imetoa fursa na kupanua zaidi uhusiano wa nchi na wananchi wao. Matumizi haya ya teknolojia yameyaweka uhusiano kati ya China na Tanzania kuwa karibu zaidi na kuwaleta karibu wananchi wa nchi hizi.

Hivi sasa, Watanzania wengi wanazo habari za China hukkadhalika Wachina wengi wanapua Tanzania. Hata hivyo, jitihada zaidi zinapaswa kuchukuliwa ili kuimarisha mahusiano maongezi mwa wananchi. Katika hili suala muhimu ni hile alilolizungumzia Balozi Dk Lu kuwa vyombo vya habari vina nafasi ya pekee ya kuwaleta Watanzania na Wachina karibu zaidi.

Na jambo jema kuona kuwa, umuhimu huo alouleza Balozi Dk Lu unazwekana kwa vitendo kutokana na Serikali ya nchi yake kuchukua hatua za makusudi kusaidia kupenga urafiki na kuviweka karibu vyombo vya habari vya Tanzania na vya China kwa nja mbalimbali, ikiwemo kutoa mafunzo na kuandaa mikutano na makongamano ambayo yanashirikisha vyombo vya habari vya China na Tanzania ama kupisha taasisi za kikanda ambazo Tanzania ni mwanachama.

Katika kuonesha urafiki na ukaribu wa watu wa China na Tanzania, mbali ya kuagana na uongozi wa nchi ambao ndio utamaduni uliozoeleka katika ngazi ya kidiplomasia, Balozi Dk. LU, alitumia kila fursa iliyokuwa mbele yake kuagana na makundi mbalimbali ya Watanzania wakiwemo waandishi wa habari.

Katika mikutano na makundi hayo, Balozi Dk Lu aleleza furaha yake kuona nchi hizo mbili zinazidi kukuza uhusiano na ushirikiano wao kwa manufaa ya serikali na wananchi wa China na Tanzania.

Mwalimu Nyerere aliwahi kunukuliwa akisema kuwa, 'Tanzania ina marafiki wengi, lakini China ni zaidi'. Historia imeonesha kuwa nchi hizo mbili ni marafiki wa kweli, marafiki wa wakati wote- iwe wakati wa jua au wakati wa mvua- ndio maana uhusiano huo umeweza kuhimili mabadiliko ya mifumo ya kisiasa na kuchumi katika nchi huzo na kuthibitisha usemi kuwa ndege wa rangi moja huruka pamoja.

Scanned by CamScanner

hewa, na hivyo miti zaidi inapaswa kupandwa kwani husaidia mengi kama kuvuta mvua, kutoa kivuli na pia kunasa hewa chafu inayopita juu lakini jamii isiache tabia ya kupanda miti kwa ajili ya uzio.

Wanasisistiza kwamba nafasi ya uzio wa miti ni kitu kuzuri kwa ajili ya mazingira ingawa ni jambo ambalo halitiliwi maanani na jamii kubwa siku hizi kulinganisha na dhana ya miti.

Ni kwa mantiki hiyo wanasema hata wanaojenga ua wa kuta wanaweza bado kupanda miti inayofaa kuwa mbele ya kuta hizo.

Wanasisitiza kwamba hakuna kanuni yoyote kuhusu upandaji wa miti ya uzio alimradi iwe ni ile inayoota vizuri na pia kupendezesha nyumba ingawa bado wanatafiti aina nzuri ya miti au maua yanayofaa kwa ajili hiyo.

Sambamba na hilo wanasema kupanda maua nyumbani ni jambo zuri pia kwani nayo yanasaidia kunasa hewa chafu ikiwemo vumbi kabla ya kufikia pua za mwanadamu.

Dk Kumar, wa Chuo Kikuu cha Surrey, aliliambia Shirika la Habari La Uingereza (BBC) kwamba: "Kitu muhimu ni kwamba miti ya kwenye uzio hunasa uchafu katika eneo la usawa wa mabomba ya kutolea moshi wa magari.

"Uzalishaji wa hewa chafu kutoka kwenye magari huanza kuchanganyika na hewa haraka sana - hivyo uzio au miti kama inayotumika kwenye uzio inapopandwa barabarani hupunguza kasi ya hewa kwenda katia makazi ya watu," anasema.

inga
vumbi

kwa ajili ya afya zetu.

Fukwe za Ziwa Nyasa zitafungua utalii Kusini

Inatoka Uk. 13

chanzo cha mapato katika sekta ya utalii.

Ukitembelea katika fukwe za Ziwa Nyasa, ni jambo la kawaida kuwakuta wafanyabiashara wanaharibu fukwe hizo kwa kwenda kuchimba mchanga na kuacha mashimo makubwa ambayo yanasababisha uharibifu katika Ziwa Nyasa.

Kuna taarifa kuwa baadhi ya fukwe katika Ziwa Nyasa zimeuzwa kiholela bila kufuata taratibu za kisheria ikiwemo ujenzi ambao hauzingatii umbali unaokubalika kisheria kutoka katika fukwe hizo.

Hata hivyo, Fukwe ya Bayi iliyopo katika eneo la Ndengere Kata ya Mbambabay na fukwe ya Pomonda Kata ya Liuli wilayani Nyasa ndizo fukwe pekee ambazo zimeanza kuendelezwa na wawekezaji binafsi, hivyo kuvutia wageni wengi wanaoingia Ziwa Nyasa.

Uchafuzi mazingira katika fukwe za Ziwa Nyasa hasa uchimbaji wa mchanga utupaji taka na utiririshaji wa maji machafu ziwani ni jambo linalostahili kupigwa marufuku kunatokana na athari za mazingira zinazoweza kutokea hivyo kuchafua vyanzo vya maji.

Fukwe wa Ziwa Nyasa zina mchanga mdogo wa rangi ya kahawia ambao ni kivutio adimu cha utalii kwa wageni, hivyo ni muhimu kutumika sheria zinazosimamia mazingira ili kuzinusuru fukwe hizo muhimu katika uchumi kupitia sekta ya utalii.

Sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004 inakataza kufanyika kwa shughuli zozote za kibinadamu katika maeneo ya fukwe, shughuli ambazo zinaweza kuathiri vibaya uhifadhi na ulinzi wa fukwe za bahari na ukanda wa Ziwa, kingo za mito, mabwawa ya maji, au hifadhi ya maji ndani ya mita sitini (60) za eneo hilo.

Kulingana na sheria hiyo, Waziri wa Mazingira anatakiwa kutunga mwongozo wa shughuli zipi za kibinadamu zinazoweza kufanyika katika maeneo hayo kutokana na ukweli kuwa hivi sasa tumeshuhudia jinsi vitendo vya kuchukua maeneo ya karibu na fukwe na kujenga hoteli na nyumba za kuishi bila kujali sheria.

Kwa mujibu wa sheria, watu waliotwaa maeneo ya fukwe kwa kuzuia watu wengine kuyafikia au kuwalipisha pesa wanakiuka kanuni ya msingi ya matumizi ya rasilimali za pamoja kwa sababu fukwe ni zawadi ya Watanzania wote toka kwa Mwenyezi Mungu.

Joseph Ndomondo, mkazi wa Liuli anasafirisha watalii toka fukwe ya Liuli kwenda jiwe la Pomonda, anasema uchafuzi wa mazingira ya fukwe unasababishwa na wananchi kutofahamu umuhimu wa kutunza fukwe, ambapo baadhi yao wanafanya biashara ya kuuza fukwe na mchanga uliopo ufukweni mwa ziwa Nyasa.



Ufukwe wa Bayi Ndengere Mbambabay wilayani Nyasa mkoani Ruvuma.

"Mimi nasafiri nchini Malawi mara kwa mara, katika nchi hiyo fukwe zao zimeendelezwa hawana fukwe nyingi za asili kama ilivyo Tanzania, sekta ya utalii Malawi imewaletea fedha nyingi za kigeni, vijana wengi wamepata ajira, wenzetu wamelitendea haki Ziwa Nyasa kiasi kwamba wazungu wanaamini hilo ni Ziwa Malawi," anasema Ndomondo.

Mwandishi wa makala haya ameshuhudia magari ya mizigo yakibeba mchanga ambao unachimbwa katika eneo la fukwe ya Liuli na kusababisha uchafuzi mkubwa ikiwemo kusababisha mmomonyoko wa fukwe jirani na bandari ya Liuli.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Liuli, Menasi Nkwera amekiri mchanga kuchimbwa katika fukwe na kudai kuwa mchanga huo unatumika kwa ajili ya ujenzi na kwamba Mkandarasi anayechota mchanga amepewa kibali na kulipa ushuru katika kijiji hicho.

Uchunguzi umebaini kuwa baadhi ya fukwe zinazozunguka Ziwa Nyasa hazina vyoo hali inayosababisha baadhi ya wananchi kujisaidia katika fukwe zilizopo na kusababisha kutapakaa kwa vinyesi.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani, Alto Komba anasema zipo sheria ndogo ndogo ambazo zimewekwa katika jitihada za kuhakikisha fukwe zote zinakuwa safi wakati wote ikiwa ni pamoja na uundaji wa vikundi vya ulinzi wa mazingira kila kitongoji.

Sera ya Taifa ya mazingira ya mwaka 1997 kifungu cha 18(a) na (b) kinayataja malengo ya jumla ya sera hiyo kuwa ni kuhakikisha upatikanaji ulinzi na matumizi sawa ya rasilimali bila kuharibu mazingira au kuhatarisha afya au usalama wa binadamu, kuzuia na kudhibiti uharibifu wa ardhi, maji, mimea na hewa ambavyo ndivyo vinashikilia mifumo ya maisha.

Kutokana na sera hiyo, imeundwa sheria ya usimamizi wa mazingira namba 20 ya mwaka 2004 katika kifungu cha 187 ambacho kinabainisha kuwa kwa makosa yanayohusu uchafuzi wa mazingira ya vyanzo vya maji, ardhi na hewa kinataja adhabu ya jumla ni faini isiyozidi milioni 50 na kifungo kisichozidi miaka saba au vyote viwili.

Gorge Ngolo wa Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira (LEAT) akizungumzia tatizo la uvamizi wa fukwe za bahari na maziwa nchini, anasema vivutio vilivyopo kwenye fukwe nchini vimekuwa vikitoweka kutokana na ongezeko la ujenzi wa hoteli na nyumba za kifahari pembezoni mwa bahari na maziwa.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, suala la uvamizi wa fukwe nchini Tanzania haliwezi kutenganishwa na ongezeko la rushwa na ufisadi nchini, ambapo baadhi ya maeneo ya wazi na fukwe nchini yamevamiwa na kufanyika uuzaji holela wa maeneo ya wazi na fukwe.

"Uchimbaji holela wa mchanga kwa ajili ya ujenzi nao ni kichocheo tosha katika ongezeko la uvamizi wa fukwe. Serikali za mitaa zimeruhusu uchimbaji wa mchanga wa kujengea katika baadhi ya maeneo ya fukwe, uchimbaji wa mchanga husababisha mmomonyoko mkubwa wa udongo," anasisitiza Ngolo.

Utafiti unaonesha kuwa uvamizi wa fukwe una athari nyingi kwa binadamu na mazingira ukiwemo uchafuzi wa vyanzo vya maji hasa vya bahari, maziwa na mito unaochangiwa na utililishaji wa maji taka kutoka hotelini na kusababisha kupata magonjwa mbalimbali kwa binadamu na viumbe wa majini kama samaki.

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 inamtaka mjenzi kujenga mradi wowote umbali wa mita 60 kutoka ziwani au baharini, lengo likiwa ni kuwalinda wananchi kuwa na uwezo wa kuzifikia fukwe.

Hata hivyo, katika hali halisi majengo mengi yanajengwa umbali wa takribani mita mbili tu kutoka baharini au ziwani.

Licha ya serikali za mitaa na vijiji kupewa nguvu ya kisheria chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kulinda uvamizi wa fukwe, uzoefu unaonesha kuwa serikali za mitaa na vijiji zimekuwa zikishiriki katika uporaji na uvamizi wa fukwe.

Sekta ya utalii ni kati ya maeneo matatu ya kwanza yanayoliingizia taifa fedha za kigeni. Hivyo ni wakati mwafaka kwa sekta ya utalii kuhakikisha inafanya juhudi za makusudi ili kuwekeza na kulinda fukwe zilizopo katika maziwa na bahari, ambazo zinaweza kuchangia maendeleo katika sekta ya utalii.

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili, mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com, simu 0784765917

Scanned by CamScanner

Haya ndiyo malengo ya tamasha la utalii Nyasa

Na Albano Midelo

TAMASHA la utalil litakuwa likifanyika kila mwaka wilayani Nyasa katika Mkoa wa Ruvuma. Lengo la tamasha hili ni kuhakikisha kuwa, vivutio vya utalii na uwekezaji vilivyopo katika wilaya hii vinatangazwa ili vifahamike.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Isabela Chilumba, tamasha la kwanza la utalii lilifanyika mwaka 2016. Kutokana na matokeo chanya ya tamasha hilo, uongozi wa serikali wa wilaya na mkoa, umekubali lifanyike kila mwaka.

Malengo ya tamasha ni kuhifadhi na kutangaza mila na desturi za makabila ya wilaya ya Nyasa na hivyo wilaya hiyo kuingizwa kwenye mradi wa kufungua utalii Kanda ya Kusini.

Malengo mengine ni kutoa elimu kwa umma kuhusu uhifadhi wa maliasili, kutunza, kulinda na kuyatangaza maeneo ya matukio muhimu ndani ya wilaya hiyo.

Anafafanua kwamba, kulinda maliasili zilizopo ndani ya Ziwa Nyasa, wakiwemo samaki wa aina mbalimbali pamoja na kutunza hifadhi ya milima ili kuhifadhi vyanzo vya maji na kutoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira na uchomaji moto ni mambo yenye kipaumbele.

Anasema makusudio mahususi ya tamasha la vivutio vya utalii kuifanya wilaya kuwa kituo cha utoaji huduma bora za elimu katika nyanja za kihistoria na kiutamaduni, kufanya utafiti wa kina katika maeneo ya kihistoria na mchango wake katika taifa.

"Tumekusudia Nyasa kuwa kitovu cha vivutio vya utalii wa kiikolojia na kiutamaduni kusini mwa Tanzania, kuongeza vyanzo vipya vya mapato ili kuleta maendeleo na kuifanya wilaya yetu imudu kutoa huduma mbalimbali kwa jamii," anasema Chilumba.

Makusudio mengine ya tamasha ni kuitangaza na kuitambulisha wilaya ya Nyasa ndani nan je ya nchi. Mengine ni kutangaza na kudumisha amani na utulivu .

Hata hivyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Dk Oscar Mbyuzi, anataja changamoto zinazoikabili sekta ya utalii katika wilaya ya Nyasa kuwa ni pamoja na ukosefu wa wataalamu wa mambo ya utalii, hali ambayo inazorotesha sekta hiyo.

Changamoto nyingine ni ukosefu wa miundombinu bora hasa barabara za ndani na viwanja vya ndege.

Nyingine ni ukosefu wa wawekezaji binafsi wa kampuni za utalii katika wilaya ambazo zitatoa huduma za utalii.

Uelewa mdogo wa jamii katika masuala ya utalii na utunzaji wa mazingira na vivutio vya utalii katika wilaya ya Nyasa ni changamoto nyingine.

Ngoma ya mganda ikitumbuiza katika tamasha la utalii Nyasa.

Lakini kubwa anasema ni vivutio lukuki vya wilaya ya Nyasa kutotangazwa kikamilifu ndani na nje ya nchi.

Ili mazingira ya utalii yawe mazuri, Dk Mbyuzi anaitaja mikakati mbalimbali ambayo inachukuliwa kuwa ni pamoja na kuhakikisha vivutio vilivyopo, hususani fukwe vinakuwa safi wakati wote kuwavutia watalii na wawekezaji.

Sambamba na hilo, anasema wanajitahidi kuhakikisha milima ya Livingstone inakuwa ya kijani na kunapandwa miti ili kurejesha hali ya kijani na hewa safi.

"Tunafanya juhudi kulinda maeneo ya kihistoria na kiutamaduni kwa kushirikisha wananchi, kuufanya mji wa Mbambabay kuwa mji wa kitalii, kushirikisha sekta binafsi kwenye utalii na kuvitangaza vivutio vya utalii kwa wananchi ili kutoa fursa ya kuvilinda na kuvihifadhi," anasisitiza Mbyuzi.

Kwa upande wake, Ofisa Maliasili na Utalii wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Bugingo Bugingo, anasema kwamba wilaya ya Nyasa ina aina kuu mbili za vivutio vya utalii ambazo ni utalii wa kiikolojia na utalii wa kiutamaduni.

Anataja baadhi ya vivutio vya utalii wa kiikolojia kuwa ni wanyamapori, ndege, wadudu, milima, mabonde, misitu, visiwa, maporomoko, mapango, chemchemi na fukwe.

Vivutio vya kiutamaduni ni pamoja na ngoma, nyimbo za asili, lugha, michezo ya jadi, sanaa, vyakula na mavazi.

Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa aliyekuwa mgeni rasmi katika kilele cha tamasha la utalii Nyasa akisalimia wananchi.

"Wilaya ya Nyasa ina fursa nyingi za utalii ambazo wananchi wamenufaika katika kiwango kidogo, baadhi ya fursa hizo ni pori la akiba la Liparamba, samaki wa mapambo, fukwe za ziwa Nyasa na maporomoko ya maji," anasema Bugingo.

Bugingo anataja Ziwa Nyasa kuwa ni mgodi wa utalii kwa kuwa lina vivutio vingi wakiwemo samaki wa aina mbalimbali . Ripoti ya utafiti ya mwaka 2011 inaonesha kuwa katika ziwa hilo asilimia 15 ya aina ya samaki wa maji baridi duniani wanapatikana ziwa Nyasa ambapo kuna aina zaidi ya 600 za samaki.

Ziwa Nyasa ni la tisa kwa ukubwa duniani, likishika nafasi ya tatu kwa ukubwa katika Afrika. Pia lina kina cha kati ya meta 426, hadi 758. Kwa upande wa Tanzania, mito mingi inayomwaga maji yake ziwa Nyasa inapita katika wilaya ya Nyasa. Mito hiyo ni Ruhuhu, Chiwindi, Ruhekei, Mbambabay, Lumeme na Likumbo.

Wilaya ya Nyasa yenye ukubwa wa kilometa za mraba 6790, ilianzishwa Machi 8, 2012 kwa tangazo la Serikali namba 87.

Halmashauri ya wilaya ya Nyasa ilianzishwa baada ya kuigawa Halmashauru ya Wilaya ya Mbinga. Wilaya ya Nyasa inapakana Malawi na Msumbiji.

Wilaya ya Nyasa bado ina maliasili za kutosha zikiwemo misitu, wanyamapori, samaki, mito, ziwa, fukwe na mali zake ambazo bado hazijaharibiwa hivyo zinaweza kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa na wananchi kupitia utalii na uwekezaji.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme anasema serikali inatambua umuhimu wa tamasha hilo la utalii. Hivyo imeamua kila mwaka lifanyike kuhakikisha kuwa vivutio vya utalii na uwekezaji vinatangazwa ndani na nje ya nchi ili kuvutia wawekezaji.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza wakati anafunga tamasha hilo mjini Mbambabay hivi karibuni, aliagiza uongozi wa wilaya na mkoa kuweka mikakati ambayo inasaidia vivutio vya utalii kutangazwa ili kuvutia wawekezaji kwa maendeleo ya Nyasa na mkoa mzima wa Ruvuma.

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili, mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com, simu 0784765917

Scanned by CamScanner

Maajabu ya Jiwe la Mbuji Mbinga

NA ALBANO MIDELO

JIWE la Mbuji ambalo lipo katika wilaya ya Mbinga, mkoani Ruvuma, ni miongoni mwa vivutio adimu na vya kipekee vilivyopo katika Bonde la Ziwa Nyasa ambalo linajumuisha mikoa ya Mbeya, Ruvuma na Njombe.

Tayari Wizara ya Maliasili na Utalii imeliingiza jiwe hilo katika orodha ya vivutio vya utalii katika Mkoa wa Ruvuma hatimaye kazi ya kutangaza eneo hilo na vivutio vingine ifanyike kwa tija.

Maana ya neno mbuji ni 'kitu kikubwa.' Jiwe hili lipo katika kijiji cha Mbuji, kata ya Mbuji na limekuwa kivutio adimu kwa wageni wa ndani na nje ya nchi.

Maajabu ya jiwe hili ni kwamba ni kubwa kuliko mawe yote mkoani Ruvuma, lina vyanzo vingi vya maji chini yake, na ni vigumu kulipanda bila kuwaona wazee wa kimila. Tahadhari imetolewa kuwa mtu asithubutu kupanda jiwe hilo kabla ya kuwaona wazee, maana huenda akapata matatizo makubwa. Pia inadaiwa kuwa ni vigumu kulizungu ka bila kufuata mila na desturi za Wamatengo.

Unapofika katika jiwe hilo inakulazimu kuwatafuta wazee wanaotoa maelekezo kwa yey ote anayetaka kupanda. Jiwe holo linaheshimika sana kwa wakazi wanaolizunguka. Hakuna mtu aliyewahi kulipanda wala kulisogelea jiwe hilo kwa hofu ya kupoteza maisha.

Mzee Sixmund Ndunguru (90), anasema kuwa ili kupanda jiwe hilo ni lazima uwe na mwongozaji ambaye ni mzee anayezifahamu vizuri mila na tarat ibu za Wamatengo zitakazokuwezesha kupanda jiwe bila matatizo.

"Ninayafahamu maajabu ya Jiwe la Mbuji tangu nikiwa na umri wa miaka mitano, mwonekano jiwe hili haujabadilika wala kuharibiwa tangu nilipolifa hamu," anasema mzee Ndunguru.

Anabainisha mimea aina ya matete ambayo imekuwepo katika jiwe hilo tangu miaka ya 1940 alipopanda juu ya jiwe hilo kwa mara ya kwanza akiwa na baba yake mzazi na kwamba kila mtu anaruhusiwa kulipanda kwa kuzingatia maelekezo ya wazee wa mila.

Wamatengo wanaamini kuwa katika jiwe hilo kuna viumbe vinavyoitwa *Ibuuta* ambavyo ni mfano wa binadamu na kwamba ni vifupi na vya ajabu ambavyo majira ya usiku vinadaiwa kuonekana. Hata hivyo, vinapatikana katika mataifa mbalimbali ambayo yamekuwa yanavipa majina mbalimbali.

Historia inaonyesha kuwa Jiwe la Mbuji tangu zamani lilikuwa linatumiwa na wazee kwa ajili ya kutambika. Katika mila na ikiwemo kujipaka unga wa muhogo kabla ya kuanza kupanda.

Taratibu hizo sio tu zinatumika kwa ajili ya wenyeji bali hata watalii wanaotaka kupanda jiwe hilo ni lazima wajipake unga huo kinyume na hapo mtu anaweza kupata matatizo mengi ikiwemo kupoteza maisha.

"Iwapo mtalii ataamua kupanda jiwe hilo bila kuwaona wazee atakuwa amevunja mila na desturi na anastahili kupata adhabu na hata kushindwa kulizunguka jiwe hilo", anasisitiza mzee Ndunguru. Akizungumzia maajabu ya jiwe, hilo Ndunguru anasema, inachukua kati ya saa 12 hadi 14 kulima' iza kulizunguka ingawa muonekana wake kwa macho mtu hudhani anaweza kulizunguka kwa nusu saa tu "ndiyo maana tunaliita jiwe la maa jabu", anasema Ndunguru.

Uchunguzi umebaini kuwa unapoliangalia Jiwe la Mbuji kwa mbali linaonekana kwamba ni fupi lakini kadri unavyolikaribia ndivyo jiwe hilo linavy oonekana kuwa refu. Hali hii inasababisha watalii wengi wanaotembelea jiwe hilo kuona hayo ni maa jabu ambayo yanatakiwa kufanyiwa utafiti zaidi kwa kushirikiana na wazee wa mila.

"Jiwe la Mbuji linatumika kuwaombea watu wanaosumbuliwa na mapepo ambao hupandishwa juu yake jiwe hilo na kuombewa kimila na mapepo hayo huondoka na wanaposhuka chini ya jiwe wag onjwa wa mapepo wanakuwa wamepona kabisa", anasema Stella Hyera(80) mkazi wa Mbinga.

Takwimu zinaonyesha kuwa kila mwaka idadi kubwa ya watalii kutoka ndani na nje ya nchi wamekuwa wanatembelea

Jiwe la Mboji lililoko Mkoani Ruvuma

Baadhi ya Wazee wa mila katika kijiji cha Mbuji chenye jiwe lenye maajabu wilayani Mbinga mkoani Ruvuma.

umbali wa kilometa 150 kutoka makao makuu ya mkoa wa Ruvuma mjini Songea.

Leodigar Kumburu (97) mkazi wa Kijiji cha Mbuji, anasema wazazi wake kabla ya kusafiri walikuwa wanakwenda kuhiji katika jiwe hilo pamo ja na kuomba mambo mbalimbali na kwamba kupanda jiwe hilo bila kibali cha wazee wa mila kunaweza kusababisha kifo ambapo hadi sasa watalii wawili wamekufa kutokana nkukiuka tarati bu za kimila.

Amemtaja mtu wa kwanza kupoteza maisha katika jiwe hilo ni mama mmoja ambaye alikuwa na mapepo alipanda peke yake na akiwa kileleni alian guka na kupoteza maisha. Alisema kuwa mtu wa pili alikuwa mtalii mmoja raia wa Marekani ambaye alipanda jiwe hilo bila mwongozo wa wazee wa mila. Alianza kusinzia akiwa juu ya jiwe hilo akaa mua kushuka lakini alianguka kabla ya kufika chini na kupoteza maisha.

Mtalii huyo alikuwa na mke wake, alikataa kupanda baada ya kuanza kujisikia vibaya lakini mumewe aliamua kuendelea kupanda huku akiwa anasali rozari ambayo haikumsaidia kwani alipoteza

Mwili wa Mzungu huyu ulitolewa katikati ya mawe ambapo serikali ya kijiji ilishirikiana na wazee wa mila na kwamba kutokana na kifo hicho idadi ya watalii wengi kutoka nje ya nchi imekuwa inamimini ka kwenda katika jiwe hilo ili kufanya utafiti na kubai ni jiwe hilo lina nguvu za aina gani.

Hata hivyo, serikali ya kijiji hicho kwa kushirikina na wazee wa mila wameamua kuboresha mazingira ya eneo la kivutio hicho cha utalii kwa kujenga nyum ba za mila za Wamatengo, kupika vyakula vya asili na ngoma za jadi ili watalii wakishaona jiwe hilo waweze kupata vyakula na ngoma za asili ya wamatengo na kujipatia kipato.

"Tuna wageni wengi wanatembelea wilaya ya Mbinga kutoka nchi za Marekani na Ujerumani, waki wa wamisionari ambao hupenda kwenda kutalii hapo. Sababu kuu ni kutokana na vifo viwili vya watalii wa kigeni vinavyotajwa kuwahi kutokea hapo Juu ya jiwe," anasema Ngwatula Ndunguru mbunge wa zamani wa Mbinga.

Anasema hapo zamani, babu zetu walikuwa wakipanda juu ya jiwe hilo na kucheza ngoma za asili ikiwemo Mganda, Muhambo, Chioda na

wageni wengi kujijengea shauku ya kutaka kujua jiwe linafananaje ndiyo maana idadi ya wa inaongezeka kila mwaka.

Jiwe hili ukiliangalia kwa mbali utaona kama "kibiongo, lakini cha ajabu zaidi jiwe hili lina sehe maalumu ya kuanzia safari ya kukwea.Hata hiv kinachoshangaza zaidi ufikapo hapo juu Mwonek wa jiwe hilo ambao hubadilika na hapo unakut kama uwanja ambao michezo huweza kufanyika.

Sheria ya Mambo ya Kale ya Mwaka 1964 ki gu cha 16 (1) (2) na marekebisho yake ya mw 1979, inazipa Mamlaka za Miji na Halmashauri Wilaya uwezo wa kuweka sheria ndogo nd ambazo zitatumika kuhifadhi, kulinda na kuratibu giaji katika maeneo yenye historia kama ilivyo jiwe la Mbuji.

Serikali kwa kupitia Halmashauri ya Wilaya Mbinga imeanza kazi ya kupiga picha za kawaida maeneo ya kihistoria na vikundi vinavyoshughulika utamaduni Wilayani Mbinga. Hatua itakayofuata kutengeneza filamu itakayoonesha Utamaduni watu wenye, kazi ambayo inaratibiwa na A Utamaduni wa Wilaya.

Scanned by CamScanner

Meli ikipakia Mkaa wa mawe katika bandari ya Ndumbi unaathiri maji katika bandari hiyo,meli hiyo inasafirisha mkaa nchi jirani ya Malawi.

Vumbi la mkaa wa mawe linaathiri wakazi Ruvuma

NA ALBANO MIDELO

WAKAZI wa mkoa wa Ruvuma wanaendelea kupata athari za kiafya na kimazingira kutokana na vumbi linalotokana na madini ya mkaa wa mawe ambayo yanachimbwa katika eneo la Ngaka wilayani Mbinga mkoani Ruvuma.

Utafiti umebaini kuwa mgodi wa madini ya mkaa ya mawe ya Liyombo na Ngaka wilayani Mbinga umekadiriwa kuwa na zaidi ya tani milioni 400 za mkaa wa mawe,kiasi ambacho kinaweza kuchimb wa kwa zaidi ya miaka 100.

Wananchi wanaathirika na vumbi hilo kwa njia mbalimbali zikiwemo za usafirishaji mkaa wa mawe toka kwenye mgodi kwa njia ya barabara na majini kupi tia ziwa Nyasa.

Kuna taarifa za baadhi ya wananchi kuugua mafua na kifua kisichopona baada ya kuathirika na vumbi la mkaa wa mawe ambao unasafirishwa kila siku na kuathiri wananchi wanaoishi katika vijiji vya kan dokando mwa barabarani katika maeneo yote ambayo mkaa huo unapita.

Utafiti wa awali umebaini mkaa huo unaanguka kidogo kidogo karibu barabara yote ambayo magari hayo yanapita kupitia barabara kuu ya Songea –Njombe.

Wataalamu na wanasheria mara kwa mara wamekuwa wanatoa ushauri kwa serikali na wawekezaji kuzingatia kikamili fu hatua za tathimini ya mazingira ili kuepuka athari za kimazingira ambazo zinaweza kujitokeza wakati na baada ya mradi.

Utafiti unaonyesha afya za wakazi wa vijiji katika kata ya Rwanda wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma ziko hatarini kufuatia kuvuta hewa chafu iliy ochanganyika na vumbi linalotokana na shughuli ya uchimbaji wa mkaa ya mawe.

Kampuni ya Tancoal inayojishughul isha na kazi ya uchimbaji wa mkaa wa mawe imeshindwa kudhibiti hali hiyo, jambo linalosababisha uchafuzi wa mazin gira kuzunguka vijiji vilivyopo jirani na mgodi huo.

Idara ya Mazingira katika halmashauri ya wilaya ya Mbinga iliiagiza kampuni hiyo kudhibiti uchafu na uharibifu wa mazingira ili kunusuru afya za wananchi, ushauri ambao haujazingatiwa na wananchi wanaendelea kuathirika na vumbi la mkaa wa mawe.

Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Charles Kitwanga hivi karibuni ametembe lea mgodi wa mkaa wa mawe Ngaka pamoja na mambo mengine ameuagiza uongozi wa kampuni hiyo kudhibiti hali hiyo ili kuepusha madhara makubwa ya kiafya yanayoweza kutokea kwa wananchi wanaoishi kuzunguka mgodi huo.

Kitwanga amesikitishwa kuona kam puni ya Tancoal imeshindwa hata kutekeleza mambo muhimu yaliyopo ndani ya mkataba, ikiwemo kuzalisha umeme kiwango cha megawati 200 kabla ya kuanza kwa shughuli za uchimbaji wa mkaa huo.

Mkuu wa wilaya ya Mbinga, Senyi Ngaga amesikitishwa kuona licha ya serikali ya wilaya kutoa maagizo mara kwa mara kwa uongozi wa kampuni Tancoal, hakuna hatua iliyochukuliwa na bado wananchi wa eneo hilo wanaendelea kute seka na hewa chafu inayotokana na ucha fuzi wa mazingira.

Uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa makala haya umebaini kuwa vumbi kali la mkaa wa mawe limekuwa likienea kati ka vijiji vilivyokuwa jirani na mgodi huo pale unaposafirishwa kwenda bandari ya Ndumbi iliyopo katika ziwa Nyasa,na kusafirishwa mkoani Mbeya kwa njia ya barabara ya MbingaSongeaNjombe.

Pengine ni muhimu kwa wadau wa mazingira kufanya utafiti wa kina kuhusu madhara ya vumbi la mkaa wa mawe kati ka maeneo yote ambayo mkaa unasafirishwa kwa njia ya barabara kwen da katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na nchi jirani.

Baadhi ya wananchi wa kijiji cha Ntunduaro wilayani Mbinga wamedai kuchoshwa vumbi la mkaa pamoja na uchafuzi wa maji ya mto Nyamabeva, ambao maji yake yamechafuliwa na vumbi la mkaa wa mawe.

Ofisa mtendaji wa kata ya Ruanda wilayani Mbinga Matilda Nchimbi anase ma wananchi wamemtaka mwekezaji katika kampuni ya Tancoal kutimiza mambo ya msingi ili kumaliza mgogoro baina ya wananchi.

Huko mwambao mwa ziwa Nyasa katika bandari ya Ndumbi wakazi wa kijiji hicho kwa miaka minne mfululizo wamekuwa wakiathirika na vumbi la mkaa mawe kutokana na kampuni ya Tancoal kutumia bandari hiyo kusafirishia mkaa nchini Malawi na Afrika ya kusini.

"Kwa miaka minne mfululizo maelfu ya tani za mkaa wa mawe umekuwa una sombwa na maji toka katika kijiji changu hadi ndani ya ziwa Nyasa, wananchi wana tumia maji hayo kwa ajili ya kunywa",anasema mwenyekiti mstaafu wa kijiji cha Ndumbi James Mbawala

Anasema kampuni ya mkaa wa mawe ya TanCoal ndiyo inayoitumia bandari ya Ndumbi ziwa Nyasa kwa ajili ya kusafirishia mkaa wa mawe kwenda maeneo mbalim bali ya ndani na nje ya nchi.

Mbawala anasisitiza kuwa kijiji hicho hakina huduma ya maji ya bomba badala yake wananchi wanatumia maji ya ziwa Nyasa yalioathirika na vumbe la mkaa kwa kunywa pamoja na matumizi mbalimbali.

"Mvua zinaponyesha mkaa wa mawe unasombwa na kuingia ziwani, tuna wasi wasi mkubwa kutokana na kutumia maji haya kwa miaka mingi ambayo yamechanganyika na vumbi la mkaa wa mawe, tunaweza kupata madhara ",alidai Mbawala.

Ametoa wito kwa serikali kupitia mkemia mkuu wa serikali kupima maji katika eneo hilo ili kujua kama yanafaa kuendelea kutumika ingawa anasisitiza kuwa hata kama hayafai bado wananchi wataendelea kutumia maji ya ziwa kwa kuwa kijiji hicho tangu uhuru hadi sasa hakina maji safi na salama ya bomba wala kisima.

Hata hivyo mwenyekiti mstaafu huyo anadai kuwa katika eneo ambalo ulilundik wa mkaa wa mawe jirani na bandari ,wali uona mkaa huo unatoa moshi na kwamba kuna baadhi ya vijana waliokuwa wanafanyakazi ya kujaza mkaa kwenye mifuko walitapika damu.

Kwa mujibu wa sheria,serikali inapokusudia kuanzisha miradi mikubwa kama ya madini,katika tathimini ya mazin gira yaani Environmental impact assess ment (EIA) inatakiwa serikali kuwashirik isha wananchi katika eneo husika ili kubai ni faida na hasara za mradi.

Mwenyekiti mstaafu huyo anadai kuwa serikali haikuwashirikisha ilipoamua kuitumia bandari ya Ndumbi kwa ajili ya kusafirishia mkaa wakati wa utafiti na sasa wakati wa uchimbaji na uuzaji.

"Mimi nilipata barua kutoka kwa mku rugenzi wa Halmashauri nikaambiwa kuna wageni niwaonyeshe sehemu ya bandari, lakini sisi kama kijiji hatukukaa pamoja kuelezwa athari zinaweza kutokea kutokana na mkaa wa mawe,hatuna elimu yoyote kuhusu madini hayo,"alisema.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa ni vigumu mtaalamu au msomi kukaa meza moja na mwenyekiti wa serikali ya kijiji ambaye ameishia shule ya msingi kuzungumzia suala la kitaalamu ameshauri katika tathi mini ya mazingira kushirikisha wataalamu wenye uzalendo .

Sera ya mazingira ya mwaka 1997 ambayo imetumika kutunga sheria mama ya mazingira ya mwaka 2004 katika kifun gu cha 4(1) na kifungu cha 5(1) inaeleza wazi kuwa kila mtu Tanzania ana haki ya kuishi katika mazingira safi,salama na afya njema hivyo hatua za uchimbaji wa madi ni iwapo sio salama inaweza kutumika she ria hii kudai haki.

albano.midelo@gmail.com.simu 0784765917

"Mkuu wa wilaya ya Mbinga, Senyi Ngaga amesikitishwa kuona licha ya serikali ya wilaya kutoa maagizo mara kwa mara kwa uongozi wa kampuni Tancoal, hakuna hatua iliyochukuliwa na bado wananchi wa eneo hilo wanaendelea kuteseka na hewa chafu inayotokana na uchafuzi wa mazingira.

Scanned by CamScanner

Usiyoyajua kuhusu Pori la Akiba la Liparamba

Na Albano Midelo

Pori la Akiba la wanyamapori la Liparamba linapita katika wilaya za Songea, Mbinga na Nyasa mkoani Ruvuma; limejaaliwa kuwa na vivutio ambavyo havipatikani katika hifadhi nyingine nchini.

Liparamba ni hifadhi iliyopo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji ambapo wanyama wake pia huwa wanavuka hadi hifadhi ya Niassa nchini jirani ya Msumbiji kisha kurudi Tanzania kupitia pori la Liparamba hadi Pori la Akiba la Selous.

Meneja wa Pori hilo Richard Bwire anasema pori la Akiba la Liparamba lipo katika ukanda wa misitu maarufu duniani ya miombo (woodland) inayokadiriwa kuwa na tembo zaidi ya 60,000 kulingana na utafiti ambao ulifanywa mwaka 2011 na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii za mwaka 2003 zinaonesha kuwa idadi ya tembo nchini iliongezeka na kufikia 120,000 ambapo nusu ya tembo hao walitoka katika pori la Akiba la Selous ambapo Liparamba ni ushoroba wa tembo toka Selous ambao wanavuka hadi nchini Msumbiji.

Hata hivyo sensa ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) ya mwaka 2009 ilionesha idadi ya tembo nchini ilikuwa 109,051 ambapo kutokana na kukithiri kwa ujangili mwaka 2014 idadi ya tembo ilishuka hadi kufikia 43,330 sawa na asilimia 60 ya tembo wote.

Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Africanus Challe anasema pembe za tembo wa Liparamba zimebainika kuwa na uzito wa kilo karibu 140 kwa pembe moja ,wakati katika hali ya kawaida pembe za tembo zina uzito wa kilo 100 kwa kila moja. Tembo anakadiriwa kuwa na kilo 7000 sawa na tani saba.

Kwa mujibu wa Mhifadhi huyo, tembo anaweza kuishi kati ya miaka 60 hadi 70, tembo jike hubeba mimba kwa miaka miwili, tembo mtoto huzaliwa na kilo kati ya 80 hadi 120, chakula cha tembo kwa siku ni kilo 300 na maji kwa siku tembo anakunywa lita 40.

"Ni mara chache sana hapa duniani kuwepo kwa hifadhi moja ya wanyamapori ambayo inatumika na nchi mbili tofauti. Tanzania tuna bahati kwa kuwa kuna na hifadhi ya wanyamapori ya Liparamba inayotumiwa na wanyama upande wa Tanzania na nchi jirani ya Msumbiji", anasema.

Meneja wa Pori hilo Richard Bwire anabainisha kuwa pori hilo lilikabidhiwa rasmi Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya usimamizi wa Idara ya Wanyamapori serikani Juni 5 mwaka 2006 ambapo pori hilo lina ukubwa wa kilometa za mraba 571 likiwa na eneo la kilometa za mraba 11,396.

Anasema ukubwa wa misitu mizito minene iliyopo katika pori hilo inachangia kupunguza hewa ukaa(CO_2) na kwamba pori hilo ni eneo muhimu katika mchakato wa (Carbon sink) ambao hupokea mvua za kutosha kwa msimu mmoja tu kwa mwaka.

Bwire anabainisha zaidi kuwa pori hilo lina mito mikubwa miwili ambayo ni mto Lunyere na mto Lumeme ambayo inamwaga maji yake katika mto Ruvuma unaomwaga maji yake Bahari ya Hindi na kwamba pori lipo katika ukanda wa madini hivyo pori linaangaliwa dhidi ya uvamizi wa uchimbaji madini.

"Miongoni mwa vivutio adimu ni uoto wa asili ya jamii ya miombo zikiwemo aina 60 za miombo, nyasi adimu aina 35, aina 80 za ndege na wanyama wa aina mbalimbali wakiwemo tembo, simba, chui, parahali, tandala, pundamil.a, nyati, kuro, pofu, kima, mamba, kiboko, ngiri na wanyama wengine", alisema Bwire.

Kwa mujibu wa Mhifadhi huyo, pori hilo lina uoto wa asili ambao haujaharibiwa katika ukanda wa wilaya za Mbinga na Nyasa na kwamba pori hilo linatoa matunzo ya tembo wanaohamia kutoka Msumbiji na kuja Tanzania na kurudi Msumbiji na kwamba utafiti umebaini wanyama wengine wakifika Tanzania hawarudi Msumbiji.

Anazitaja shughuli za uhifadhi ambazo zimefanywa katika kipindi cha Julai 2016 hadi Agosti 2017 kuwa ni doria za kawaida ndani ya pori, kazi za intellijensia, usuluhisho wa migogoro ya mipaka, kutoa elimu ya uhifadhi kwa umma na kupandisha hadhi mapori tarajiwa ya Gesimasowa na Litumbandyosi.

Shughuli nyingine ni zoezi la uwekaji wa alama za kudumu kwenye mipaka ya hifadhi, doria maalum ya kupambana na kilimo cha bangi hifadhini, kuhamisha wavamizi kwenye ushoroba wa pori la Selous na Gesimasowa, doria ya kudhibiti wanyama waharibifu na kikao cha ujirani mwema kati ya mikoa ya Ruvuma na Mtwara upande wa Tanzania na mikoa ya Niassa na Cabodelfado nchini Msumbiji.

Hata hivyo Bwire alitaja pendekezo la kuhifadhi pori la Akiba Liparamba lilitokana na utafiti uliofanywa na Idara ya Maliasili wilayani Mbinga katika miaka ya 1980 hadi 1982 ambapo mambo kadhaa yaligundulika.

Mambo hayo ni upungufu mkubwa wa eneo la misitu kutokana na kilimo cha kuhamahama na kilimo cha mazao ya msimu kilichoendeshwa na wakulima toka eneo la milimani kwenda katika ukanda wa chini kulima mahindi kwa ajili ya chakula.

Mambo mengine ni upungufu wa maeneo yaliohifadhiwa kwa ajili ya kulinda miti muhimu na yenye thamani kubwa kama mininga, mahogani na kupotea kwa mimea ya asili ambayo ilihitajika na kuendelea kuhitajika kwa ajili ya chakula, dawa na ulinzi wa viumbe asilia.

Hata hivyo Meneja Mwanzilishi wa mradi wa pori la Akiba la wanyama Liparamba, Hashim Sariko anasema kutoweka na kupotea kabisa kwa wanyamapori na wadudu asilia ambao miaka ya nyuma waliishi katika misitu ndiko kuliisukuma Halmashauri ya wilaya hiyo kuamua kuwa na maeneo ya misitu ya kutosha kama misitu ya akiba.

Sariko anabainisha zaidi kuwa maeneo hayo yalizuiliwa kwa kulinda misitu, miti, wanyama, wadudu na viumbe wasiharibiwe kwa kuwa na maeneo ya vivutio vya asili kwa lengo la kuwawezesha wananchi kutembelea, kuona na kujifunza historia na sayansi ya viumbehai katika vivutio vya utalii, makazi ya wanyamapori na hifadhi ya maji na mazingira.

Afisa Maliasili wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe alisema kuwa pori hilo lina kiwango cha juu cha hifadhi ambacho kinatiliwa mkazo kisheria katika ulinzi, usimamizi, uendelezaji na matumizi ya malihai ikiwemo misitu, samaki na wanyamapori hivyo kuhifadhiwa kumejumuisha" sekta nzima ya maendeleo ya mazingira,m aliasili na utalii kwa gharama nafuu.

"Hili eneo ni la kipekee katika ukanda wa juu wa misitu ya miombo, lipo karibu na ziwa Nyasa, wengi watavutiwa na eneo hili kuona msitu mzuri wa asili usioharibiwa sanjari na wanyama adimu wakiwemo chui, simba, palahala na tandala wakubwa", anasema.

Anasema pori la Liparamba ni kielelezo cha ukanda wa viumbehai katika mazingira yao ya asili ambapo anayataja malengo mengine ambayo yamesababisha serikali kuweka pori la akiba la Liparamba kuwa ni kulinda vyanzo vya maji na milima ya kuvutia.

Pori la Liparamba linapakana na vijiji saba ambavyo ni Liparamba, Ndondo, Mipotopoto, Mitomoni, Mseto, Mtua na Mpepai na kwamba wakazi wa vijiji hivyo baadhi yao wanafanya ujangili kwa ajili ya kupata kitoweo hali inayosababisha askari wa wanyamapori kufanya doria siku 20 kila mwezi.

Albano.midelo@gmail.com, simu 0784765917

Scanned by CamScanner